ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa na Rais
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
43.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
44.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
45.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
47.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
48.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
49.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake

50.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa Jimbo la Kikwajuni

51.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk Jimbo la Kitope

52.Mhe. Marina Joel Thomas Kateuliwa na Rais

53.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Jimbo la Mkwajuni

54.Mhe. Mgeni Hassan Juma Nafasi za Wanawake

55.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

56.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

57.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

58.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

59.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

61. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

65.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

66.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

67.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

69.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

70.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

71.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

72.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

76.Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Kumi – Tarehe 23 Oktoba, 2012

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mahmoud Muhammed Mussa) alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 60

Kikosi Maalum cha Uokozi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Zanzibar katika kipindi cha miezi 20 tumeshuhudia ajali tatu kubwa za boti kuzama baharini na watu kupoteza maisha na wengine kuokolewa.

(a) Serikali ina mpango gani wa kuanzisha kikosi maalum cha uokozi baharini Zanzibar.

(b) Kwa kuwa Mamlaka ya Usafiri baharini Zanzibar inakabiliwa na uhaba wa wakaguzi wa meli na vifaa vya mawasiliano, lini matatizo hayo yatapatiwa ufumbuzi na kuimarisha sekta hiyo.

(c) Ni sababu gani hadi sasa Mamlaka hiyo imeshindwa kutunga kanuni tangu kutungwa kwa sheria ya kuanzisha Mamlaka ya usafirishaji baharini Zanzibar (ZMA).

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru Allah kwa kutupa uhai na uzima, naomba kwa ruhusa yako nijibu swali namba 60 la Mhe. Jaku Ayoub wa Jimbo la Muyuni kama hivi ifuatavyo:-

(a) Serikali inao mpango kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kuunda kikosi maalum cha uokozi, lakini kikosi hiki kinatarajiwa kuwa na uwezo kamili na vifaa kamilifu. Kwa hivyo kwa muda huu tumo katika kujitayarisha kwa kusaidiana na Jumuia ya Kimataifa ya *IMO* (*International Maritime Organization),* kwa muda huu kikosi cha KMKM kimewekwa ili kiweze kufanya shughuli za uokozi rasmi.

(b) Mamlaka ya Usafiri baharini kweli inayo upungufu wa wakaguzi lakini jitihada kubwa zinachukuliwa sasa hivi kwa kushirikiana kama ambavyo miongozi ilitolewa baada ya kupatikana ajali kwa kushirikiana na Jumuia ya Sumatra tayari karibu hivi litatolewa tangazo la kuajiri wakaguzi wa Melini wa kimataifa wenye viwango ambavyo vitaweza kukidhi haja ya kimataifa.

(c) Ni kweli kwamba bado Shirika au mamlaka hii haijaweza kanuni rasmi lakini zimeshaanza kufanyiwa kazi na tayari wiki iliyopita kulikuwa kuna semina muhimu sana iliyoandaliwa pamoja na shirika la kimataifa la usafiri baharini yaani International Maritime Organization ambayo inapelekea kuanzishwa kwa utaratibu wa ukaguzi na usafiri wa baharini. Kwa si muda mrefu tutaona kwanza marekebisho ya sheria zilizopo ambazo tunategemea katika kikao kijacho yatajadiliwa marekebisho ya sheria ya usafiri baharini, lakini pia kwa kupatikana kwa kanuni ambazo zitaweza kusaidia usalama kwa usafiri baharini kwa abiria wote.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri dhamana wa Wizara hii, kwa kuwa malalamiko yamekuwa ya muda mrefu na hiki chombo ni muhimu sana kwa wananchi, kuna malalamiko karibu miaka miwili hivi sasa. Idara, Mamlaka inayoshughulika dhamana hii imelia miaka miwili kuomba waajiriwa

waajiriwe hao wataalam wa Taasisi hii, lakini Wizara yako bado haijawa *serious* miaka miwili si kidogo Mhe. Waziri. Hapa wananchi wanatusikiliza, chombo chao muhimu kama Mhe. Spika, anavyosema miaka miwili mpaka leo lini wataajiriwa mimi nataka unipe kauli lini wataajiriwa.

La pili, tumekuwa tukipitisha sheria nyingi Barazani hata Mhe. Hamza akisema hizi sheria zishafika wakati angalau tuzipumzishe kidogo tulizokuwa nazo tuzitumie. Leo Wizara kweli inashindwa na milioni 570 kuweza kuimarisha kitengo hiki ikiwemo kuongeza wakaguzi, kituo cha mawasiliano na kuajiri wataalamu. Hata hiyo milioni Sabini mpaka leo mwaka wa pili tunashindwa kuja kutunga kanuni hapa Mhe. Waziri naomba unipe jawabu ni lini wataajiriwa wataalamu hao, na lini kituo hicho cha wataalamu kitajengwa Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kitengo hiki au mamlaka hii ilikumbwa na tatizo kubwa pale ambapo ilitokezea ajali ya Spice Islander ambapo uongozi wake karibu wote wa juu uliingizwa katika ile ripoti ya Spice Islander. Kama mwezi mmoja uliopita tu ndio mamlaka imepata Mkurugenzi wake Mkuu na ninaamini kazi anayoifanya sasa hivi hali itakwenda vizuri sana katika siku chache zijazo.

Ama kuhusiana na ajira kuna ajira za aina mbili katika mamlaka. Kuna ajira ile niliyoitaja mwanzo ya wakaguzi, hii inatolewa tenda na kama haijatolewa basi mwezi huu hautomaliza itatolewa tenda ambayo ni ya kimataifa ya kuwapata wakaguzi watakaokidhi haja ya kukagua vyombo vyetu. Ajira nyengine ni kutimiza ile *structure* ya mamlaka ambayo tayari tunazungumza na Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kuweza kupata ruhusa ya kuweza kuwaajiri wale wafanyakazi ambao kuna mapengo katika nafasi za kazi.

Kwa hivyo mimi naamini sana kwa Mkurugenzi ambaye tayari ameshachukua nafasi yake uwezo wake ni mzuri, mkubwa, na si muda mrefu mamlaka itabadilika na kwenda katika hali ambayo inatambulika katika hali nzuri.

Swali la upatikanaji wa fedha kama ambavyo tunaona sote bajeti zetu ni finyu, kwa sana tunategemea tuende kidogo kidogo na kadri ambavyo tutapata uwezo, hali ya mambo itatengenea. Lakini nataka nihakikishe kwamba vifaa vya mawasiliano ni suala la kipaumbele sana katika kujenga mamlaka hii ya usafiri baharini. Kwa sababu hivi ni vifaa ambavyo vinatoa taarifa katika utaratibu wa usafiri wa vyombo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi kuweza kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri wangu mpya katika wizara hii. Pamoja na majibu yake mazuri sana hata Mhe. Jaku anapiga kofi kwa majibu aliyofurahikiwa na Mhe. Waziri, lakini na mimi inanipasa kumuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri hivi sasa tuna wakaguzi kutoka Bara na Zanzibar, lakini kwa muelekeo ulivyo kuwa wabara ndio wenye Sauti zaidi kuliko wazanzibari je, huoni sasa hivi wakaguzi wako wa kitengo hiki kuona kuwa wanadhalilishwa.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti sio kweli kwamba wakaguzi wa hapa wanadhalilishwa, isipokuwa utaratibu huu ulikuwa ni wa muda pale ambapo ajali ya Pili ilitokea, na ilitokea baina ya Dar es Salaam na hapa Unguja ilionekana kwamba basi kuna haja ya kuimarisha huu ukaguzi kuingiza vyombo vyote viwili vya *SUMATRA* kwa upande wa Bara na hiki chetu cha *ZMA* kwa hapa ili ziweze kufanya kazi kwa pamoja. Lakini napenda kuhakikishia kwamba vyombo hivi vinafanya kazi kwa kujitegemea na vinatoa nafasi ya wakaguzi bila ya kuwa na shindikizo lolote.

Lakini la Pili ni kwamba baada ya kuona kwamba sheria ziko katika huyu anazungumza hivi na huyu anazungumza hivi, tayari imeshafanyika mikutano miwili mikubwa iliyowakusanyisha watendaji pamoja na viongozi wa taasisi hizi mbili; *ZMA* na *SUMATRA* ili kuweza kupata sheria ambazo zinalingana baina ya *SUMATRA* na hapa katika usafiri wa baharini. Sheria hizi sasa zitakuwa hazina tena manung'uniko ya kwamba hawa labda wana hivi na hawa wana hivi. Lakini kila chombo kitashughulikia na utaratibu wake bila ya kuingiliana katika utendaji wa kazi. Na mkaguzi ambaye ataajiriwa atafanya kazi kwa niaba ya maagizo ama ya *ZMA* au *SUMATRA* bila ya kuingiliwa na chombo chengine kwa mujibu wa taratibu za kisheria.

Kwa hivyo hakuna njia ya kusema kwamba kuna udhalilishaji.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaomba nimuulize Mhe. Waziri swali lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti Mhe. Waziri amekiri kwamba serikali ina mpango wa kuunda kikosi maalum kwa ajili ya waokozi, anaposema hivi anakusudia kuwaambia wazanzibari kwamba KMKM na Zimamoto wameshindwa kazi.

Pili, kwa nia njema kabisa serikali baada ya kutokezea ajali waliamua kuwasaidia ubani wananchi walioathirika, na tulipata taarifa kwamba baadhi ya majimbo kuna wananchi kwa bahati mbaya sana hawajafikiwa na sadaka hiyo, je kama wapo katika majimbo yetu ya Zanzíbar tukiwagundua tuwapeleke wapi.

Tatu ilipozama meli ya karibuni *SUMATRA* na watendaji wa Bara walisema hawahusiki, lakini leo kwenye ukaguzi ndio wanahusika huoni wafanyakazi wa zanzibari, kwa sababu kwenye lawama walisema hawahusiki lakini kwenye ukaguzi kwa sababu kuna maslahi wanasema wanahusika. Huoni hili si kuwafanyia haki wakaguzi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti ninakushukuru, kikosi maalum cha uokozi baharini kinahitajika peke yake kwa sababu boti ambazo zinatumika kwa uokozi wa majini ni tofauti na hizi ambazo wanatumia KMKM zile zaidi ni za ulinzi. Lakini boti za uokozi ni maalum zina vifaa maalum, na ziko zinatarajiwa ziweko chini ili wakati zinapofika pale ziweze kusaidia haraka haraka uokozi. Ni suala la muda na ni suala la fedha lakini kuweko kikosi cha baharini cha uokozi ni suala muhimu na ni suala la lazima.

Kwa hivyo sio kwamba KMKM na Zimamoto na Uokozi wameshindwa kazi, lakini wao zaidi KMKM ni ulinzi na hii Zimamoto na Uokozi ni juu ya ardhi zaidi. Lakini cha baharini kwa sababu usafiri wetu ni wa kila siku ni lazima kiwepo katika hali hiyo.

Swali la sadaka na malipo nafikiri lipo Ofisi ya Makamo wa Rais, mimi sina jibu hapo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano naomba kuongeza jibu la nyongeza la Mhe. Hija kama ifuatavyo kuhusu sadaka ya wahanga waliopata matatizo ya MV Spice Islander. Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe serikali imechukua hatua sana katika kufanya tathmini ya wahusika ili wapate malipo yao wote waliohusika na ajali hii. Na nia ni kuwasaidia wananchi wetu waliopata ajali ile.

Hatua za kwanza kulikuwa na orodha maalum iliyotayarishwa na Tume Teule na serikali ilichukua hatua ya kuwalipa wale wote walio kwenye lile buku la orodha lililotayarishwa na Tume Teule. Baadae kukawa na orodha iliyofanywa na Wilaya kupitia masheha na hao wote walioleta majina yao ya awali, majina yao yalishughulikiwa na kupewa sadaka yao. Lakini wapo watu waliojiandikisha mwisho baada ya zoezi zima ambayo hii kidogo ilileta utata na ilibidi Idara inayoshughulikia na maafa wafanye utafiti.

Kwa wale walioona kuna uhakika kwamba hawa wamekutwa na maafa hayo malipo yamefanyika. Na hata hivi sasa tunatoa matangazo mara kwa mara kwa wale ambao majina yao yalikuwemo kwenye orodha, ama wale majina yao yaliyokuwemo katika majina yaliyotengenezwa orodha na masheha kupitia Wilaya vile vile tuliwatangazia sana na wengi walijitokeza wakapata fedha zao.

Sina uhakika kama wapo bado ambao hawajapata malipo, kwa wale ambao wanao ushahidi kwamba walikutwa na ajali ile. Kwa wale ambao wamekutwa na ajali ile tukipata ushahidi wa kutosha basi serikali itafanya malipo kama ambavyo wamefanyiwa wenzao, kwa wale ambao wameumia na wakapata kuokolewa wanalipwa laki nne elfu kumi na mbili mia tano, na wale ambao walipoteza maisha wanapata sadaka ya laki tano na nusu. Jambo hilo siku zote litapewa kipaumbele kwa sababu tunajua ni jambo la kitaifa.

Baada ya maelezo hayo nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Nam. 70

Ujenzi wa Daraja la Mkia wa N'gombe

Mhe. Suleiman Hemed Khamis – Aliuliza:-

Wanakijiji wa Mkia wa Ng'ombe wana matumaini ya ujenzi wa Daraja kwa kutumia *Culvert* na kifusi kwenye kivuko cha mto wa maji ya chumvi tangu kipindi kilichopita. Daraja hili lingewasaidia wanakijiji kwa ajili ya kuvushia bidhaa na vifaa mbali mbali lakini ujenzi huo hadi leo haujafanyika.

Je, ni lini daraja hili litajengwa ili kuwaondoshea usumbufu wananchi.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kabla sijamjibu Mhe. Suleiman Hemed Khamis swali lake namba 70 naomba niweke nyongeza ya mwisho ya suali (c) la Mhe. Hija Hassan Hija. Chombo kile ambacho kilizama Skagit kilikuwa kimesajiliwa na Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar. Yale maneno mengi yaliyotoka ni maneno ya gazeti, maneno ya gazeti yanakuwa yanatoka katika lugha tofauti, lakini kila upande ulikuwa unahusika kwa sababu boti ile iliondokea Dar es Salaam na wanaopaswa kuchunga usalama wa chombo kinapoondoka ni wale ambao gati ile au bandari ile inafanya kazi.

Kwa hivyo wote sehemu mbili walikuwa wanahusika, na ndio maana baada ya tokeo lile ndio wakaona sasa ipo haja ya kufanya kazi kwa pamoja badala ya kusingiziana au kukanushiana. Kwa hivyo napenda niseme kwamba hali ambayo tunayokwenda mbele, tunaitarajia itakwenda kwa uzuri na kwa kila hali. Kwa sababu wote wameshakubaliana kuendesha kazi kwa pamoja.

Swali la Mhe. Hemed Khamis wa Jimbo la Konde nimjibu kama hivi ifuatavyo:-

Tayari Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kupitia UUB ishapanga bajeti ya ujenzi wa daraja hili na kama tunavyojua kwamba njia zetu zinajengwa kwa bajeti ya misaada, mikopo, lakini hili limewekewa bajeti ya mfuko wa barabara. Kupitia utaratibu wa *PPP* yaani *Public Private Partnership* Wizara imeanza kutoa kazi za tenda kwa ujenzi wa madaraja na *Calvert* kwa watu binafsi au kampuni binafsi. Kwa hivyo tayari utaratibu huu ushaandaliwa na si muda mrefu tayari daraja hili litakuwa limeshapatiwa tenda ili kuweza kujengwa katika kipindi hiki cha bajeti hii.

Kwa hivyo ninakuhakikishia Mhe. Suleiman Hemed Khamis kwamba daraja hili limepangiwa katika kipindi hiki ujenzi, lakini kama nilivyoeleza kwamba ujenzi utafanywa na kampuni binafsi kwa sababu ya utaratibu ambao tunakwenda nao.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Mwenyekiti naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa ujenzi huu wa daraja la maji ya mto ambayo ni maji ya bahari inapita kwenye mto huo ni daraja muhimu sana kwa wananchi wa Mkia wa Ng'ombe. Wananchi wa Mkia wa Ngo'mbe kwa kweli ombi lao lilikuja muda mrefu sana lakini nategemea kama hivyo alivyozungumza Mhe. Waziri pengine ataweza kulifanikisha. Ajue kwamba ni suala muhimu daraja hii kuwepo kwa sababu wananchi wa Mkia wa Ngo'mbe wanakosa kupeleka mahitaji yao ya Chamula, vifaa vya ujenzi kwa ajili ya skuli pamoja na madawa ya hospitali kwa sababu gari haziwezi zikapita. Na gari ndio zinazoweza kufanya kazi za kubeba mizigo.

Kwa hivyo ningependa kumuuliza Mhe. Waziri ni lini hasa, maana yake kwa kipindi hiki inaweza kuwa mwisho wa mwaka pia ni kipindi hiki hiki, ili kutuwekea wazi ni lini hasa kwa wakati ambao ulopangwa baada ya miezi mingapi tutegemee daraja hili litaanza.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti kwa kuwa bajeti ya mfuko wa barabara hutegemea na ukusanyaji wake wa uuzaji wa mafuta, sasa naomba Mheshimiwa aamini kwamba katika bajeti hii daraja limo, na tutahakikisha tukijaaliwa linajengwa. Lakini lini kwa sasa sina uwezo mkubwa wa kumwambia ni lini ila naweza nikapata muda nikamuandikia kwa maandishi kwamba ni lini hasa limepangiwa kujengwa.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti ninashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti kwa fununu nilizonazo ni kuwa fedha zilizotengwa kwa Idara ya Ujenzi na Utengenezaji wa Baraza kwa asilimia kubwa sana zimepangiwa kutumika katika kumaliza barabara ya Mkapa ambayo iko siku nyingi sana. Na fedha zitakazotumika kumaliza barabara ile ni kubwa kiasi ambacho naona Wizara haina mpango wa kuwa na mfuko mwengine, kutokana na umuhimu wa daraja hili ambalo Mhe. Suleiman kalieleza na ahadi aliyoitoa Mhe. Waziri kama ikifeli je haitakuwa kama kulidanganya Baraza.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti sijalisikia swali lake.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Kutokana na umuhimu wa daraja hili la Mkia wa Ngo'mbe na ahadi ambayo Mhe. Waziri ameshaiweka, na kutokana na maelezo yako ya nyuma kuwa fedha za mfuko huu wa barabara zimetengwa kwa kumaliza barabara ya Mkapa je, Mhe. Waziri si ataona Wizara yake imetoa kauli ambayo si ya kweli kwa umalizaji wa barabara hii ya Mkia wa Ngo'mbe.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti bajeti huwa inapangwa kutokana na yale makadirio ya ukusanyaji, ninaamini kwamba madhali daraja hili limeingizwa katika bajeti kupitia mfuko wa barabara, basi ni imani yangu kubwa kwamba litajengwa ama hizo nini nyengine kwamba zitumike huku na huku ni masuala ya kubuni na kufikiria tu, lakini daraja limeingizwa katika bajeti ya mfuko wa barabara na *inshaallah* nitasimamia kwamba lijengwe.

Nam. 42

Uongezaji wa Vituo vya Kuuzia Umeme

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Shirika la Umeme la Zanzibar ni Shirika linaloendeshwa kibiashara, na moja kati ya majukumu yake ni kuhakikisha wateja wote wanaotumia umeme wanapata huduma hiyo karibu na maeneo wanayoishi, lakini hadi hii leo vituo vya kuuzia umeme vipo mbali na maeneo wanayoishi watu.

Je, Shirika lina mpango gani wa kuongeza vituo zaidi ili kuwarahisishia wananchi kutotaabika kuvifuata vituo vilivyopo maeneo mbali na wanakoishi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Muyuni swali lake namba 42 kama hivi ifuatavyo:-

Shirika limeliona tatizo hilo na limeanza kazi ya kuwasogezea huduma hiyo na litaendelea kufanya hivi hatua kwa hatua kama ilivyokwisha kufanya katika maeneo yafuatayo:-

Maeneo ya ng'ambu ya Mji, Shirika limefungua kituo cha Mazizini na Mwanakwerekwe.

Maeneo ya vijijini shirika limefungua kituo cha Mauzo huko Mkokotoni.

Maeneo ambayo vijiji vyao havijafunguliwa kituo, Shirika huwatangazia wananchi na masheha wao kwa siku maalum ambazo wafanyakazi wahusika watakwenda kupokea na kuwauzia umeme huko huko.

Aidha, Shirika hivi sasa linaendeleza na mpango wake wa ktaka kutoa huduma hizo kupitia simu za mkononi, ambao ndio itakuwa rahisi zaidi. Mazungumzo baina ya ungozi wa Shirika na Kampuni za simu za mkono yanaendelea ili wananchi waweze kutumia huduma ya kulipia na kununua umeme kupitia simu zao za mkononi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri mzoefu, usumbufu wa wateja bado unaendelea na siku zote tunaambiwa watu watapata huduma kupitia simu zao za mikononi kwa muda mrefu, hebu ni lini hasa huduma hii itapatikana ukiangalia wenzetu Bara wanakwenda mbio sisi bado tunatambaa kwenye vituo.

Pili, kutokana na mji wetu wa Zanzibar kukua kituo cha Malindi ambacho wananchi wengi wa Mji mkongwe wanakitegemea kile ni kimoja tu.

Tatu, kituo cha Michenzani foleni yake imekuwa kubwa hata wananchi kufika barabarani kuhatarisha usalama wao, kuna mpango gani wa dharura kuongeza vituo na utakuta katika kituo hicho muuzaji ni mmoja tu.

Nne, ni sababu gani zinazosababisha mwezi wa Ramadhani huduma hiyo kufungwa kuanzia saa nane hadi saa mbili za usiku. Je, waumini wote hao wanaume wamekwenda kupika futari.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti ni kweli tumekuwa tukiambiwa tumekuwa tukisema kwamba tunataka tutumie utaratibu wa huduma za simu za mkononi. Lakini hili suala ni makubaliano baina yetu sisi na mashirika ya simu za mikononi, lolote kati ya mashirika ya simu yatakayokubali, basi tutatumia utaratibu huo. Kwa hivyo tunamuomba Mhe. avute subira maana mazungumzo ndio yanaendelea hivi sasa, na tukiwa tayari bila shaka taarifa itatolewa.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli hata hapa mjini hivi vituo ni vichache na kweli ipo haja ya kuongeza vituo zaidi hilo swali tutalifanyia kazi na tutaongeza vituo zaidi hata hapa mjini vile vile ili wananchi wasipate usumbufu.

Mhe. Mwenyekiti swali la mwezi wa Ramadhani, mwezi wa Ramadhani huduma zetu huwa tunakusudia kuzisogeza mbele baada ya kufunga saa nne tunataka tufunge saa sita usiku.Tunafikiria bila shaka jioni watakuwa wameshughulika, kwa hivyo vitu inabidi tuvifunge watu waendelee na mapishi yao lakini tukimaliza kufutari tunafungua tena tunaendelea mpaka usiku kama kawaida.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, malalamiko haya ambayo Mhe. Jaku Hashim ameyaleta katika suala lake ni masuala ya msingi kabisa, hata mimi katika jimbo langu tuna matatizo na wananchi wangu wameshanifika mara nyingi kwa matatizo hayo ya vituo vya kutoa huduma. Konde ni kituo kikubwa sana na kuna wateja wengi sana ambao wanatumia shughuli za umeme na wanapata tabu mpaka watafute nauli kwanza ya kutoka pale kwenda Chake Chake au Wete ndiko kiliko kituo, watafute nauli ya kwenda huko halafu watafute na pesa za kulipia hizo shughuli zao.

Sasa mimi ningemuomba Mhe. Waziri masuala haya ya malipo ya muda mrefu lini hasa yataondoka? Kama ulivyozungumza kuwa simu za mkononi ambazo zitasaidia, angalia wananchi ambao wako vijijini katika suala hili kwao wao litakuwa gumu sana. Kwa hivyo, kuangalia angalau kwa hatua ya mwanzo hasa kama Chake Chake na Konde ni mbali sana basi ningekuomba Mhe. Waziri ni lini hasa watawekewa vituo vya uhakika katika Jimbo la Konde au kwa Wilaya nzima ya Micheweni kwa jumla.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, njia rahisi ya kutatua tatizo la kuuza umeme katika maeneo ya vijijini au katika maeneo yote ya Unguja na Pemba ni suala la kutumia simu za mikononi. Napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kwamba, hivi sasa wanaomiliki simu za mikononi wengi mno hata huko vijijini unaweza ukadhania kwamba hakuna watu wanaomiliki simu za mkoni lakini wengi kweli kweli. Kwa hivyo, najua suala hili kutatuka kwake ni kuweza kuingia katika utaratibu wa kuuza umeme kwa kutumia simu za mikononi, sasa akiniuliza ni lini ni kwamba mpaka mazungumzo haya yamalizike tuelewane na Shirika la Simu itakuwa tayari kutoa huduma hii Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Makao Makuu ya Umeme *ZECO* ina ulinzi masaa 24, kwa nini isiweke kuuza umeme wa Tukuza kwa masaa 24 kama tunavyopata huduma za benki kwa njia ya *ATM*. Kwa vile *ZECO* haijapata uwezo wa kuwa na *ATM* kwa nini isiweke mtu wa kuuza umeme kwa masaa 24 tukapata huduma hiyo Zanzibar sote tukajua tunakwenda wapi kama tunavyopata huduma za umeme au huduma za simu na mafuta kwa masaa 24 hapa Zanzibar. Kwa nini shirika hili bado linajirejesha nyuma na uwezo wanao wa kufanya hivyo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, hiyo ni rai na ni rai nzuri na naipokea kwenda kuifanyia kazi.

Nam. 44

Upigaji Rangi Majengo ya Mji Mkongwe

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Kwa vile Mji Mkongwe ni moja kati ya maeneo ya urithi wa dunia, na wakati huo huo ni eneo la kihistoria linalofanya watalii wengi kuja kutembelea na kuona mji wetu ulivyo.

Je, wizara husika na hifadhi ya Mji Mkongwe hawaoni kwamba alau mwaka mara moja kupigwa rangi majengo yote japo kwa chokaa ili kuupa mji huo haiba inayostahiki.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 44 kama ifuatavyo:-

Kwa kweli Mamlaka ya Mji Mkongwe ina nia ya kuona majengo yote yaliyomo katika eneo hilo yanapakwa rangi kila mwaka ili kubakisha haiba yake ya kuvutia kwa majengo hayo ya asili, lakini kutokana na uhaba wa fedha kwa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, na Mamlaka kwa ujumla haiwezi kubeba jukumu hilo kwa hivi sasa. Kwa hivyo, Mamlaka kwa kushirikiana na wizara inaahidi kuendelea kuwashajiisha wamiliki wa majengo kuyapaka rangi majengo yao ili kuendeleza urithi wa Dunia (*World Heritage Site).*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, Mji Mkongwe hivi sasa umekabiliwa na uchakavu mkubwa wa majengo na kuhatarisha usalama wa wananchi, na ukiangalia uwezo wa wananchi wetu ni mdogo hasa eneo la Mji Mkongwe majumba yamechoka sana. Serikali ina mpango gani wa dharura kuyafanyia marekebisho hayo wananchi hao.

Pili, karibu miaka minane au tisa kuna suala mimi mwenyewe binafsi yangu nilikuwa nikilipigia kelele Mji Mkongwe kuna nyumba imetiwa mabati ilikuwa Shirika la Umeme la Kuuza Umeme pale Mwanzo nyumba ya kwanza ya pili, imetiwa bati miaka minane au tisa nyumba hiyo haijengwi imezingizwa mabati na hakuna sababu yoyote inayoendelea pale baada ya kuwaudhi wananchi tu wapita njia. Je, Mji Mkongwe huu umekuwa sheria kwa wengine na kwa wengine hawatumii sheria hizo? Huu si ndio ubaguzi wenyewe Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, majumba ya Mji Mkongwe ni mengi kweli, mji wenyewe ni mkubwa umeanza tangu Forodhani umekwenda zake mpaka Hospitali ya Mnazi Mmoja wote ni Mji Mkongwe, na huku umekwenda mpaka barabara ya kati kati ya Michenzani sehemu ya huku nyuma yote ni Mji Mkongwe, na ni kweli kuna majengo mule ndani ambayo yanahitaji kufanyiwa matengenezo. Lakini kwa kuepusha madhara kwa wananchi majengo yale wananchi waliwahi kuhamishwa katika majengo ambayo yameelekea kuwa mabovu watoke wahame, wakahama lakini baadae kinyemela wanarudi mule tena na mpango wa kusema tunayajenga yote majumba yale hivi sasa hatuyawezi kusema kweli.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, tunasema kwamba hatuna mpango wa dharura kwa majengo yale kwa hivi sasa, lakini kadiri tutakavyoweza kuyafanyia matengenezo na ndio maana tunaanzisha hii Mamlaka ya Mji Mkongwe kwa pale ambapo wanaweza kufanya matengenezo wafanye matengenezo. Lakini nawasihi wananchi wanaoingia katika majumba ambayo yaliwahi kuhamishwa na wakajirudi kinyemela hakuna marehemu mvua, ikija mvua kwenye majengo yale ajue hatari yoyote itatokea.

Halafu kuna hili suala la hapa Forodhani ambapo kuna jengo limezungushwa mabati haliendele na ujenzi. Hili ni suala la kufuata masharti, masharti ya Mji Mkongwe yanapotolewa kwa ajili ya mjenzi lazima yafuatwe na kama huyafuati bila shaka utazuiwa kuendelea na ujenzi. Tunatilia mkazo sana kwamba majengo ya Mji Mkongwe yanayojengwa upya yabakishe sura ile ya Mji Mkongwe kama yalivyokuwa zamani sio majengo ya Mji Mkongwe yakae sawasawa na nyumba iliyojengwa hivi sasa Makadara au wapi ya kisasa kabisa. Majengo yale Mhe. Mwenyekiti, ndani unaweza ukalitengeneza vizuri sana, lakini nje ile sura ya Mji Mkonwe ionekane kwamba imebakia katika umbo la yai sio umbo la mikato mikato kama ya sasa hivi.

Mhe. Omar Ali Shehe: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ili nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye sehemu (a), (b) na (c).

(a) Mhe. Mwenyekiti, Mji Mkongwe ni majumba ya zamani ambayo yamechoka na kama alivyosema Mhe. Waziri mara nyingi husababisha maafa na hofu kwa wananchi wetu katika maisha yao. Nchi yetu imekuwa ikijisifia sana kuwa na Mji Mkongwe. Ni kitu gani hasa Mhe. Mwenyekiti, kinachowafanya wageni watembelee Mji Mkongwe

(b) Ukiacha mbali mapato yanayotokana na ununuzi wa vinyago na mahoteli machache yalioko kule ni faida gani au ni mapato gani mengine ambayo serikali hupata kwa kuwa na Mji Mkongwe.

(c) Mhe. Waziri haoni kuwa laitani kama serikali ingeliyavunja majumba yale mabovu na kujenga majumba mapya na ya kisasa kutokana na eneo lilipo Mji Mkongwe na mazingira mazuri na manzari nzuri ya Bahari huoni kwamba nchi yetu ingelipata mapato mengi zaidi,

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, Mji Mkongwe ni rasilimali ya nchi ya kukumbusha mji wa asili Unguja zaidi ya huu uliopo sasa ulikuwa vipi. Hiyo ni historia inapatikana katika Mji Mkongwe. Na *architecture* iliyotumika katika baadhi ya majengo Mji Mkongwe ni *architecture* ya kuvutia ambayo katika baadhi ya nchi hivi sasa duniani haipo tena. Kwa hivyo, wageni wanapokuja Zanzíbar wakitembelea Mji Mkongwe wanajikumbusha *architecture* za kizamani sana ambazo hivi sasa katika baadhi ya nchi hazipo tena wameziharibu. Sasa Zanzíbar hatutaki kuwa miongoni mwa watu wanaoharibu *architecture* ya zamani ambayo bado ipo katika mji wetu.

Sasa faida gani zinapatikana baada ya vinyago. Ukianza kuwavutia wageni hata kama hukuuza kinyago hao wageni wanakuja na pesa za kigeni kwa hivyo tayari unapata faida kwa sababu wewe umepata wageni katika nchi yako. Sasa unaposema kwamba majumba yale tuyavunje kwa kweli tutakuwa tumeharibu kitu adhimu sana katika mji wetu.

Mimi nadhani hivi sasa maafisa wangu wa mipango miji wanafikiria namna ya kujenga majumba ya kisasa katika maeneo kama Gulioni, Makadara, Kwaalamsha, Mikunguni, kule ndio kuwe kuna majumba ya kisasa kama yale yanayopatikana New York unaweza ukaona ni ndoto lakini litatokea katika nchi hii suala hili. Yatajengwa majengo ya kisasa kabisa ya kuonesha kwamba sasa hivi mji utaonekana vizuri katika hali hiyo, hatukuwahi sisi lakini najua mitandiko ya mambo hayo ipo na tutajenga, lakini Mji Mkongwe ubakie kama Mji Mkongwe kama mnavyokwenda katika nchi nyengine ukenda unaoneshwa hii hapa ni sehemu mpya na hii huku ni sehemu ya zamani.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kuweza kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kuwa ule ni mji wa historia. Je, Mhe. Waziri haoni iko haja ya hivi sasa bajeti yake ya mwakani akaiwekeza pale ili kupata historia yetu ikawa nzuri na majumba yakawa mazuri na watalii wakaja kwa wingi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, rai ya Mheshimiwa ni nzuri lakini uwezo, fedha kama hazipo basi huwezi kufanya kitu chochote. Lakini tunajaribu kushirikiana na Washirika wa Maendeleo mbali mbali kwa kuzidi kuboresha masuala hayo tunasaidiana katika hapa na pale sehemu mbali mbali. Kama sasa hivi tunataka tutengeneze ukuta wa Forodhani ambao sasa unaanza kuvunjika ule, tunataka tuujenge upya ili ubakie na uonekane kama ulivyokuwa zamani. Jitihada hiyo tunaifanya ni sawa sawa kama tulivyofanya kujenga ukuta wa Maruhubi, ukipita sasa hivi utaona kama ni ukuta wa zamani sana na umejengwa juzi kwa mara ya pili umetengenezwa tena. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Nam. 13

Walimu wa Sayansi Kutoka Nigeria

Mhe. Rufai Said Rufai (Kny. Mhe. Saleh Nassor Juma) – Aliuliza:-

Kuna taarifa kuwa katika kuziba pengo la walimu wa sayansi serikali ina azma ya kuchukuwa walimu kutoka Nigeria.

(a) Je, serikali imefanya uchunguzi wa kina na upembuzi yakinifu juu ya kuleta jopo la Wa-nigeria katika visiwa vidogo kama hivi.

(b) Mhe. Waziri anaweza kulieleza Baraza hili wasifu/hadhi ya Wa-nigeria katika medani ya kimataifa.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nambari 13 lenye sehemu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Kabla ya kumjibu naomba kutoa maelezo mafupi ya kwamba ni kweli kuwa serikali imeomba walimu wa masomo ya Sayansi katika nchi mbali mbali ikiwemo Nigeria. Makubaliano ya kuleta walimu wa kujitolea yametiwa saini kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Nigeria tarehe 5 Julai, 2012 ya kutuletea walimu wa kujitolea 15 hapa Zanzíbar. Kati ya Walimu hao 15 walimu sita wameshafika na wameshapangiwa skuli zao nao wanaendelea na kazi vizuri. Walimu wengine saba watafika Jumatatu watapokelewa na watapangiwa skuli zao, walimu wawili watakaobakia watakuja mwezi ujao. Baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali la (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Wizara imefanya uchunguzi yakinifu kuhakikisha kwamba walimu wanaokuja au waliyoombwa na kuchaguliwa wana uwezo mkubwa sana wa kusomesha au wa kufundisha na ni walimu waliotimia hawana matatizo yoyote ya kiafya au kiutamaduni. Walimu hao baada ya kupokelewa hao walimu sita mimi mwenyewe na wasaidizi wangu tulikutana nao tukaendelea kuwadadisi na tukathibitisha kwamba ni wazuri na ndipo tulipowagawa katika skuli zilizohusika. Skuli tulizowapeleka ni Matemwe, Donge na Pwanimchangani. Walimu watakaobakia watagawiwa katika skuli za Wawi, Pandani na Tumbe kutimiza walimu 13 watakaokuja wataobakia ni walimu wawili watapangiwa badea.

b) Serikali ya Nigeria inapeleka walimu wengi sana wa kujitolea katika nchi mbali mbali za Afrika na nchi za Visiwa vya Caribbean. Kwa mfano, hivi karibuni wamepelekwa walimu Namibia, Kenya, Visiwa vya Karibean na walimu 1000 wamepelekwa hivi karibuni Afrika ya Kusini. Kwa hivyo, kufuatilia usambazaji wa wasaidizi walimu kwa mpango huu wizara imegundua kwamba hakuna matatizo ya kuwaleta walimu hao kutoka Nigeria kuja kutusaidia. Ahsante sana.

Mhe. Nassor Ali Salim: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa majibu mazuri na yenye ufasaha. Walimu hao wa Nigeria ambao wamekuja hapa Zanzíbar kwa ajili ya kusomesha vijana wetu. Je, wamekuja hapa kwa mkataba wa miaka mingapi.

Pili, maposho yao na huduma nyengine zinatolewa na serikali gani ya Zanzíbar au Serikali ya Nigeria.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, walimu hawa kama nilivyosema ni wa kujitolea, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzíbar haiwalipi mishahara bali itawalipa gharama za kwenda hospitali au kutibiwa wanapokuwa wagonjwa, watapatiwa nyumba za kuishi na watafidiwa gharama za matibabu wakati wote wakiwa nchini.

Suala la pili kuwa ni muda gani. Walimu hawa tumewaomba na tumewaajiri kwa muda wa miaka miwili na baada ya hapo tutajishauri kama tunataka kuwaongezea miaka miwili mingine, au tunabadilisha kuwaleta walimu wengine au kuacha kabisa kwa ajili ya walimu hao.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa fursa na mimi nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu ya Zanzíbar skuli zetu karibu zote zina matatizo ya walimu wa sayansi na walimu hawa walioombwa kwa njia ya kujitolea ni walimu 15 na bahati nzuri Mhe. Waziri amezitaja zile skuli ambazo watapelekwa hawa walimu. Sasa napenda nimuulize kwa sababu skuli zetu karibu nyingi hazina walimu wa sayansi. Je, walitumia vigezo gani katika kuwagawa hao walimu katika hizo skuli.

Vile vile je, zile skuli nyengine ambazo zina matatizo wizara yake itachukua juhudi gani ili kuondoa matatizo hayo ya walimu wale wa sayansi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kabisa alivyosema Mhe. Mjumbe kuwa tuna tatizo la walimu wa sayansi. Tatizo hili ni la kitaifa tena ni la muda mrefu sana, tunajitahidi kuliondosha kwa kadiri tutakavyoweza kwa kutumia njia mbili. Njia ya kwanza kuwasomesha au kuwahimiza kwanza wanafunzi wetu wapende kuchukua masomo ya sayansi ili wakimaliza tuwapeleke Vyuo Vikuu wakasome sayansi na wachukue *course* za ualimu. Njia hiyo ndio njia endelevu na ndio tunayoifuata kwa uhakika lakini bila shaka ni njia ya muda mrefu, kumsomesha mwalimu au mwanafunzi mpaka amalize darasa au amalize *Form VI* achukue miaka

mitatu au minne Vyuo Vikuu halafu ndio awe mwalimu bila shaka ni muda mrefu, lakini bila shaka pia muda endelevu na huu pia tunaufuata.

Lakini kutafuta walimu wa kutusaidia waliokuwa wameshasomeshwa masomo ya sayansi ni njia nyengine tunayoitumia ambayo ni njia ya muda mfupi. Tutaendelea na hivi karibuni tumemaliza mazungumzo na nchi ya Misri, Pakistan tutaomba walimu wa aina hiyo kutoka Misri na Pakistan na kwengineko waendelee kuja kutusaidia kama hivyo nyuma tulivyozowea kwa ajili walimu wa aina hiyo na wafanyakazi wa aina hiyo kutusaidia kuondosha mapungufu tuliyonayo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa majibu yake ya uhakika ambayo ameyajibu katika Baraza hili. Lakini kwa ruhusa yako naomba nitoe jibu la nyongeza juu ya serikali ina mpango gani kuhusu suala la kuondosha tatizo la walimu kwa jumla hasa wa masomo ya sayansi hapa Zanzíbar.

Mhe. Mwenyekiti, serikali hivi karibuni kupitia Tume ya Utumishi Serikalini imetangaza nafasi za kuajiri walimu na katika mkakati wetu katika kipindi cha mwaka huu tulipanga kuajiri walimu 1,018, lakini kwa awamu hii kwa mujibu wa uwezo uliopo serikali imeamua kuajiri walimu 140 wa *degree* ya sayansi, walimu 100 wa *degree art*, walimu 50 wa diploma ya sayansi, walimu 150 wa diploma ya *art* na walimu 60 *Form VI* sayansi na walimu 100 wa cheti. Jumla ya walimu tunaotarajia katika kuwaajiri kipindi hiki ni walimu 600 na utaratibu wetu wa kuwaajiri walimu hawa, Tume ya Utumishi Serikalini itaitaka Wizara ya Elimu waoneshe mapungufu yaliyopo katika skuli zote za Unguja na Pemba, walimu hawa wataajiriwa kwa mujibu wa mahitaji yaliyoko katika skuli. Huo ndio mkakati ambao serikali unatarajia uufanye kuondosha tatizo la walimu wa sayansi katika Visiwa vya Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, na mikataba ya walimu hao itazingatia pia ni eneo gani analoajiriwa mwalimu huyu ili kwenda kuondosha tatizo badala ya kuwaajiri walimu hawa na kurundikana katika Mkoa wa Mjini Magharibi au katika mijo mikuu ya visiwa vya Unguja na Pemba. Ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii nikamuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni ni juzi tu, tuliangalia katika vyombo vya habari katika ziara ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoifanya nchini Oman. Kwa bahati nzuri katika ziara ile alifuatana na Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Mhe. Mwenyekiti, katika ziara ile tulimuona Mhe. Waziri wa Kazi akatia saini kwa niaba ya Zanzíbar msaada kwa ajili ya kusaidia elimu ya juu hapa Zanzíbar. Je, Mhe. Waziri katika msaada ule hatuoni kwa kuwa kuna tatizo kubwa la walimu wa sayansi tukatumia nguvu ile ya msaada wa elimu ya juu kutoka Serikali ya Oman kwa ajili ya kusaidia na kusomesha kwa wingi wanafunzi ambao wanasoma masomo ya sayansi pamoja na walimu ambao wanasomea masomo ya sayansi ambao hivi sasa wanakwama katika fedha za kujiendeleza na elimu hiyo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Hamza Hassan Juma swali lake kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kulikuwa kuna ziara hiyo na ni kweli kulitiwa saini mkataba au makubaliano ya kusaidiana. Na ni kweli kwamba nguvu zaidi ziliekwa katika mafunzo.

Mhe. Mwenyekiti, taaban sisi tulipeleka mahitaji yetu, yaani Wizara ya Elimu na mahitaji yetu yalikuwa yame-*base* zaidi katika masomo ya sayansi. Makubaliano yaliyofikiwa ni kusomesha shahada ya kwanza na shahada ya pili ya *BSc* na *MSc*. Shahada zote mbili ni za sayansi.

Hapo baadae tunaweza tukatia tena saini mkataba au makubaliano katika masomo ya *Arts*, lakini kwa bahati nzuri sisi kwa sasa mahitaji yetu zaidi yapo katika sayansi kuliko katika *Arts*. Kwa hivyo mawazo ya Mhe. Mwakilishi yanalingana kabisa na mkataba tuliotia saini na lengo letu na namshukuru Mhe. Hamza kwa kuliona hilo na kulifikiria suala hilo na bila shaka tutalitekeleza kwa utaratibu huo na tumeshajiandaa.

Nam. 14

Wananchi wa Vitongoji Kutokulipwa Fidia Zao

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza**:-**

Katika Mkutano wa Baraza uliopita Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali alieleza kwamba tayari tathmini imeshafanywa kwa wananchi ambao mazao yao pamoja na mashamba yaliyoingia Chuo cha Mafunzo ya Amali – Vitongoji na kwamba malipo ya wananchi hao yatafanywa kwa awamu.

Ni sababu gani za msingi zilizosababisha kuwa hadi leo hii hawajalipwa fedha zao hizo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu**:-**

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe, Mwakilishi swali lake Namba 14 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti**,** ni kweli kabisa tulitoa ahadi hiyo ya kulipa fidia kwa wale ambao vipando vyao viliharibika au viliharibiwa. Na ni kweli kabisa tulitoa ahadi hiyo kwamba tutalipa kwa awamu. Ninataka nikiri kwamba ni kweli kabisa tumechelewa na muda mrefu umepita kabla hatukulipa. Kwa nini tukafanya hivyo.

Katika eneo tunalolizungumza la Vitongoji ni eneo tulilolitembelea, tumeliona vipando tumeviona na kilimo tumekiona. Kwa bahati mbaya sana tulipolitembelea eneo hili tumepokea madai ya wakulima 18 waliolima vipando mbali mbali ikiwemo mivinje.

Tulikubaliana kwamba mivinje tutaacha hatulipi fidia lakini na tutawaachia wenyewe kwa sababu haitukeri hapo ilipo katika ujenzi wa hayo majengo tunayotaka kuyajenga. Lakini kwa bahati mbaya sana madai tuliyopokea badala ya wakulima 18, tumepata madai ya wakulima 46. Kwa eneo dogo kama hilo haliwezi kuweka wakulima 46.

Halikadhalika madai ya vipando vilivyoburugwa kwa mfano migomba, mihogo tulikubali hivyo tutavilipa fidia, lakini idadi ya vipando imeongezeka marudufu. Kwa mfano mtu mmoja alidai alipwe migomba yake 100. Migomba 100 haiwezi kupandwa katika eneo hilo.

Kwa hivyo basi sasa tumekubaliana, maana waliofanya makisio haya ni watu wa Wizara ya Kilimo na watu wa Wizara ya Kilimo nao wakasisitiza kwamba madai yao au makisio yao ni sahihi wakati sio sahihi.

Tumekubaliana sasa na wakulima wenyewe kwa mujibu wa idadi yao na kwa mujibu wa vipando vyao walivyotaka walipwe fidia. Fidia ya Wizara ya Kilimo ilikuja shilingi mia tatu na tatu milioni. Jambo ambalo halikuwa sahihi hata kidogo, ni pesa nyingi mno.

Lakini baada ya kukutana na wenye vipando tumekubaliana milioni 30 ndio fidia sahihi kwa awamu ya kwanza na awamu hii tutailipa mara tu tutakapotiliwa fedha na Wizara ya Fedha na tumeshaziomba fedha hizo.

Tutalipa shilingi milioni 30 haraka sana tukishatiliwa hizo fedha na fedha tumeshaziomba. Kwa hivyo namuomba radhi sana Mhe. Mwakilishi pamoja na wananchi wa Jimbo la Wawi. Kwanza nawapongeza na kuwashukuru kwa ustahamilivu wao lakini sasa nawaahidi tena kwa mara ya mwisho kwamba hivi karibuni tutawalipa shilingi milioni 30 kwa awamu ya kwanza na awamu ya pili na ya tatu itafuata baadae.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa busara zake na majibu yake aliyotumia lugha nzuri sana nampongeza kwa hili.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri aliyonijibu mzee wangu hapo mkereketwa mwenzangu kuhusiana na suala zima la kulipa fidia, nataka akumbuke tu kwamba ni miaka karibu nane tangu fidia hii idaiwe bado hawajalipwa wananchi, na kwa mujibu wa taaluma ya sheria wanasema kwamba haki ikichelewa kutolewa ni sawa sawa kuwa haikutolewa kabisa.

Ameahidi kwamba shilingi milioni 30 atazilipa hivi karibuni, jee Mhe. Waziri anaweza akaniambia ni lini kwa sababu ni miaka nane imepita tunaahidiwa tu, jee leo hii anaweza akatoa kauli ni lini Wizara ya Fedha watawalipa hao.
Nilitaka nijue hili ili tuweze kuwaeleza wale wananchi kwa sababu siku zimekuwa ni nyingi. Hilo ni swali langu la mwanzo ni lini hizi shilingi milioni 30 za awamu ya kwanza atawalipa kwanza.

La pili kwa kuwa juzi tu wakulima wengine pale sehemu anayojenga taasisi hata za binafsi, kwa mfano *Istiqama* pamoja na wale Chuo Kikuu Huria, hata mwaka mmoja haikupita wakulima wamelipwa gharama na taasisi binafsi zaidi ya milioni 100 pale. Haoni kwa kufanya hivi ni kuitia aibu serikali yetu hii ya Mapinduzi ya Zanzibar na hususan kwa vile Wizara hii unaiongoza wewe Mhe. Waziri mwanasiasa nguli kabisa katika nchi hii na muasisi, huoni ni kuitia aibu serikali.

La tatu, wanataka kulipwa shilingi milioni 30 Mhe. Waziri anaweza kusema jee ni *the total cost estimate* ambayo wamekusudia kulipa pale ni bilioni ngapi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye kifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo.

Nitamuomba kifungu cha (b) akirejee baadae lakini naomba nijibu kifungu cha (a) na (c).

Lini tutawalipa. Ahadi ni deni. Nikitoa ahadi hapa lini tutawalipa nitaishi na deni na fedha hizo sina mimi mkononi mwangu, zipo Wizara ya Fedha, nimeshazidai na zimetiwa katika bajeti. Sina wasi wasi hata kidogo kwamba pesa hizi nitapewa.

Jibu langu ni kwamba nikipewa tu nitalipa.

Namuomba alirejee swali la (b) na (c).

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe Mwenyekiti, nilisema kwamba juzi tu *Istiqama* ambayo ni taaisisi ya watu binafsi pale walilipa zaidi ya shilingi milioni mia moja pale kwa wakulima wa aina hiyo hiyo pamoja na wale wanaotaka kujenga Chuo Kikuu Huria pale Vitongoji, walilipa haraka haraka haikufika miaka minane kama ilivyofika nyinyi watu wa Wizara ya Elimu.

Jee, kwa kufanya hivyo kushindwa hata na *Istiqama* Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzíbar ambao wamelipa zaidi ya milioni mia moja juzi tu wakulima hao hao. Si kuitia aibu Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzíbar na hasa kabisa kwa vile wizara hii kwa wakati huu unaongoza wewe mwanasiasa nguli ninayekuamini sana mahiri kabisa, huoni ni jambo la aibu hili. Hilo ni la (b).

Na (c) ulisema kwamba utalipa milioni 30 kama *first payment, what the total estimate for whole cost*. Ni kiasi gani cha makisio yote, wewe utalipa milioni 30 awamu ya mwanzo. Jee, zote ni ngapi watakazolipwa fidia wananchi hao.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe Mhe. Waziri tungelikuomba ujibu swali moja kati ya haya mawili kwa mujibu wa Kanuni ya 40 (3) kinaeleza kwamba “Mjumbe anaruhusiwa kuuliza swali moja tu la nyongeza kwa kila swali la msingi lakini anaweza kulieka swali hilo kwenye sehemu zisizozidi mbili. Naona Waheshimiwa Wajumbe tumekuwa na utaratibu wa kuuliza maswali ya nyongeza matatu matatu.

Kanuni inatuongoza tuulize maswali mawili ya nyongeza.

UTARATIBU

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, swali moja linaweza kuwa na vipengele (a), (b) na (c).

Sasa mimi nimeuliza (a), (b) na (c) hilo hilo moja lakini kama Kanuni zimenifunga hapo basi naomba anijibu hilo la pili.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali (b) na (c) kwa pamoja.

Nasema Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikitoa ufafanuzi wa ziada wa suala hili, mimi nilisema sitaki niuite udanganyifu lakini nataka niseme makoseo ya kuweka bajeti kubwa ya shilingi mia tatu na tatu milioni kwa eneo dogo kama lile ulilolizungumza la Vitongoji ambalo eneo lote lile haliwezi hata kufika thamani hiyo.

Lakini zaidi ya hivyo vipando vilivyoongezwa, idadi kubwa ya wakulima kutoka 18 mpaka 46. Wameongezeka wakulima maradufu wala hawajakuwepo.

Sasa kuchelewa kwa hilo hakutii aibu serikali bali serikali ililazimika kulifuatilia kwa umakini zaidi kuhakikisha idadi ya vipando vinavyodaiwa na wadai, yaani wakulima vinalingana. Ikaonekana havilingani.

Sasa badala ya kulipwa shilingi milioni mia tatu na tatu, ndio sasa tumeshaafikiana na wakulima wenyewe na vipando vyao tutalipa pesa hizo kwa awamu tatu.

Awamu ya kwanza ni hiyo ya kulipa shilingi 30 milioni haraka iwezekanavyo tutakapotiliwa fedha hizo ambazo tumeshaziomba. Kwa hivyo si aibu ya serikali wala si aibu ya mtu yeyote lakini kwa bahati mbaya makisio ilikosewa na kwa hivyo tumepata kadhia hiyo.

Ahsante sana.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa serikali inaondoa matatizo na haitaki iweke matatizo kwa wananchi wake na inataka kuwalipa wananchi wa Vitongoji kwa nia nzuri kabisa. Lakini alipokuwa akijibu swali mama Mhe. Waziri amesema kama wao wamefanya utaratibu wa mwanzo waliochunguza wameona kama ni watu 18, baadae sasa wamefika watu 46.

Sasa jee, namuuliza Mhe. Waziri kutokana na hilo kwa watu 18 na hivi sasa ni 46 na sasa wanataka kuwalipa watu. Jee, utaratibu gani utatumika ili kuona kama wale waliopewa ndio wale wahusika kamili na hawa wengine wasije wakazua matatizo baadae ili serikali iondoe matatizo isije ikaweka matatizo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza hiyo figure uliyoitoa mimi sikuitoa hiyo. Mimi nilisema kwanza wakulima waliokuwepo ni 18 na sio 800, lakini baadae wakaongezeka wakawa 46. Wakulima 46 sio sahihi wakulima 18 ndio sahihi.

Ndio tuliowakuta na tukawasajili, maana hawa tumewasajili. Tumewahesabu tumezungumza nao tumewakuta tukawasajili. Ni hao 18 ndio tutakaowalipa kwa mujibu wa mazao yaliyoharibika.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza.

Pamoja na majibu yake mazuri sana Mhe. Waziri lakini na mimi naomba kumuuliza swali lenye (a) na (b).
Mhe. Waziri tulipokuwa tukitembea sisi kwenye kamati yetu ya Mawasiliano na Ujenzi tuliwaita wahusika na tukakutana nao uso na macho, na wakatueleza kuwa ni kweli kuwa fedha hizo zilifanywa bajeti kubwa lakini watakapokuwa tayari kuweza kurekebisha hiyo bei iliyoletwa kubwa basi kwa hivyo wanaweza wakalipwa wale watu mara moja.

Lakini leo unatwambia kuwa ndio kwanza umeanza kupeleka jibu la kuomba fedha hizo. Jee, Mhe. Waziri ili lugha sahihi kati ya hawa wahusika na wewe.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa heshina taadhima naomba kumjibu Mhe. Makame Mshimba swali lake kama hivi ifuatavyo.

Mimi ndio sahihi. Hao watu walikosea.

HOJA ZA KAMATI

Ripoti ya Kamati Teule ya Kuchunguza Utendaji wa Baraza la Manispaa Zanzíbar

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati Teule): Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniruhusi niendelee na kuwasilisha ripoti yetu; Ripoti ya Kamati Teule kuhusu kuchunguza utendaji wa Baraza la Manispaa la Zanzibar.

Lakini kabla ya kuwasilisha Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo yafuatayo.

Jana daktari wangu Mhe. Abuu baada ya kuona hali yangu si nzuri katika kuendelea kusoma aliomba nisitishe ili niendelee leo na akaomba hotuba yangu nifanye *summary* ili isije ikawa kama ya jana. Namshukuru sana *doctor* kwa kuona hali ya mgonjwa wake kuwa hawezi kuendelea na shughuli.

Lakini bado hali yangu haijawa nzuri wiki nzima hii, lakini kutokana na umuhimu wa jambo hili nimejilazimisha kufanya hivyo. Nilikusudia kufanya *summary* lakini sikuweza kufanya *summary* kwa sababu ya jambo moja Mhe. Mwenyekiti.

Nimekuwa nikipokea simu kutoka kwa wananchi mbali mbali juu ya ripoti hii jinsi ilivyowagusa, lakini pia wengine walikuja nyumbani asubuhi ambapo kamati ilishindwa kuwasiliana nao. Hii ni kutokana na faida kwamba nimeisoma ripoti yote na wananchi walikuwa wanaisikiliza.
Sasa ninataka kuliambia Baraza lako tukufu ripoti hii ya uchunguzi inagusa maeneo mengi, inagusa watu wengi, taasisi nyingi. Sasa unapoifanya *summary*, maana yake unawanyima haki wale wananchi wengine ambao wameguswa na jambo hili.

Kwa sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunakuwa hatuna tatizo kwa sababu tatizo ripoti ile tayari tunakuwa tunayo. Lakini kwa wale wananchi waliokuwa nje, wanakuwa wao hawana chochote wanategemea kupata taarifa hii kutokana na chombo hiki. Kwa hivyo ningemuomba sana Mhe. Mwenyekiti, niendelee na ripoti hii kama ilivyo, naomba kama muda wa saa moja hivi nitaimaliza na Waheshimiwa Wajumbe muendelee kunistahamilia.

Nitakapofika pahala nikikwama daktari wangu akiniona siwezi kuendelea ninaye msaidizi wangu hapa Mhe. Abdalla Juma atashika nafasi ili tuimalizie ripoti hii. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Baada ya muhtsari wa ripoti ya maelezo hayo, sasa naomba niendelee Mhe. Mwenyekiti, na nitaendelea nitaunganisha na muhtasari wa mambo yaliyobainika na kamati kufuatia uchunguzi wa suala lile lililopita.

Miongoni mwa mambo yaliyobainika ni pamoja na kwanza shughuli ya ujenzi imetolewa bila ya kufuata utaratibu za zabuni jambo ambalo ni kinyume cha kanuni ya 55 (b) ya Kanuni za Baraza la Manispaa na Sheria ya manunuzi na uuzaji wa mali ya umma.

Lakini pili kuna utata kuhusu tarehe ya kuanza kwa mkataba ambapo risiti zinaonesha kwamba wameanza kulipa tokea tarehe 1 Aprili, 2010, wakati mkataba umeanza tarehe 1 Novemba, 2010.

Tatu kitendo cha Mkurugenzi kutamka kuwa mali ya serikali hazikodishwi zaidi ya miaka kumi ni kinyume ya kifungu cha 47 cha sheria ya ardhi Nam. 12 ya 1992 kama ilivyorekebishwa na kifungu cha 6 cha sheria Nam. 11 ya mwaka 2010. Hii ni kutokana na kifungu hicho kinaruhusu mali ya serikali kukodishwa sio zaidi ya miaka 99.

Nne kamati imebaini kuwa mkataba huo hauna tija kwa Baraza la Manispaa.

Maoni ya Kamati kutokana na Matokeo ya Uchunguzi Huo:

Kamati inapendekeza yafuatayo.

1. Watendaji wa Baraza la Manispaa wakiongozwa na Mkurugenzi wafuate sheria na kanuni mbali mbali za nchi.
2. Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa awe muangalifu na kauli zake anazozitoa
3. Kwa kuwa mkodishwaji alishindwa kutoa maelezo ya kina mbele ya kamati kuhusiana na malipo yaliyofanywa tarehe 1 Aprili, 2010, kamati inashauri kuwa mkataba huo uanze mwezi huo, yaani mwezi wa Aprili badala ya Novemba.
4. Kamati inapendekeza Baraza la Manispaa kuwa makini wakati linapoingia na kufunga mikataba ili mikataba hiyo iweze tija

Mhe. Mwenyekiti, Bustani ya Makontena Darajani:

Eneo la makontena Darajani limedhamiriwa kujengwa bustani ya maegesho ya magari. Baraza la Manispaa limefunga mkataba na kampuni ya Golden Group chini ya Ndugu Ali Abdalla Ali yaani Ali Kibasi.

Katika kufuatilia hili kamati ilikutana na ndugu Ali na ilitaka kujua chanzo cha Ndugu Ali kupewa kazi ile, naye alieleza kwamba baada ya kazi nzuri aliyoifanya kutengeneza bustani ya Jamhuri kwa kushirikiana na Ndugu Asia pamoja na kuweka bollard na pipe stone katika eneo la Skuli ya Haile Selassie ndio sababu iliyompelekea Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa kumuomba amsaidie katika kazi zake mbali mbali ikiwemo hiii ya ujenzi wa bustani ya Darajani.

Kazi ya uwekaji wa bollard na pipe stone ilifanywa na kwa kushirikian na mafunzi wa Baraza la Manispaa. Pia alieleza kwamba gharama za ujenzi zililipwa na Baraza na Ndugu Ali alitoa vifaa vya ujenzi tu ambapo bollard moja aliiuzia Manispaa shilingi hamsini elfu. Walikubaliana hivyo na Manispaa na kwa kuwa Ndugu Ali hana utaalamu wa ujenzi isipokuwa ni mtaalamu wa utengenezaji wa bustani.

Baada ya maelezo hayo, kamati ilitaka kujua namna mkataba ulivyofungwa baina hizi mbili. Kwa kulitolea ufafanuzi hili Ndugu Ali alieleza kwamba alipokea barua kutoka Baraza la Manispaa ya kumtaka kutengeneza bustani ya Darajani ambapo alitakiwa pia kuwasilisha gharama za ujenzi.

Ujenzi wa bustani ya Darajani iligharimu shilingi milioni sita laki saba na thalathini na tano elfu na mia moja ambapo fedha za kazi hiyo zililipwa kwa awamu kama ifuatavyo:-

1. Tarehe 2 Mei, 2011 alilipwa Shs.2, 356,585/- baada ya kazi kufikia asilimia 30.
2. Tarehe 11 Mei, 2011 alilipwa Tanzania shilingi 2,356,585/- baada ya kazi kufikia asilimia 70.
3. Tarehe 23 Mei, 2011 alilipwa shs.2, 356,586/- baada ya kazi kufikia asilimia 100.

Alizidi kuieleza kamati kwamba wamekubaliana na Manispaa kuishughulikia bustani ile kwa mwaka mmoja.

Muhtasari wa Mambo yaliyobainika na Kamati kufuatia Uchunguzi wa Suala hili:

Mhe. Mwenyekiti, mambo yafuatayo yalibainika:-

1. Shughuli ya ujenzi ilitolewa bila ya kufuata taratibu za zabuni jambo ambalo ni kinyume cha Kanuni ya 55 (b) ya Kanuni ya Baraza la Manispaa ya Sheria ya manunuzi na mali za umma.
2. Ingawa zipo barua tatu tofauti zinazoonesha Ndugu Ali kulipwa gharama alizotumia kwa awamu. Hata hivyo kamati imebaini kuwa kwa mujibu wa barua hizo malipo yalifanywa ndani ya mwezi mmoja kutokana na tarehe za barua hizo jambo ambalo lilitia mashaka kamati. Sambamba na hilo hundi Nam. 990305 inaonesha kuwa malipo hayo yalifanywa kwa pamoja. Kutokana na mashaka hayo kamati ilimtaka aeleze ukweli wa jambo hilo ambapo Ndugu Ali alikiri kwamba alilipwa fedha zile kwa pamoja kimakosa na katika kutatua hili alitakiwa na Baraza kuandika barua zile.
3. Hakuna mkataba baina ya Baraza la Manispaa na mtengenezaji wa bustani.

Maoni ya Kamati kutokana na Uchunguzi huo:

Kamati inapendekeza ifuatavyo.

Kwa kuwa Baraza lina wataalamu wa fani mbali mbali, kamati inalishauri Baraza kukabidhi kazi ya wataalamu wake hao ili kuepuka kutumika vibaya fedha za walipa kodi na wananchi.

Maeneo mengine aliyojenga Ndugu Ali Abdalla Ali (Kibasi), kwa kuwa Ndugu Ali ni mteja mkubwa wa Baraza la Manispaa, kamati ilitaka kujua maeneo mengine aliyofanyakazi ya Baraza.

Katika kufafanua hili alieleza kwamba katika bustani ya Donge aliwahi kupewa kazi katika awamu mbili. Awamu ya kwanza alitakiwa kutengeneza maegesho ya gari (parking) kwa kutengeneza njia, kupanda miti, kutia mbolea pamoja na kuweka piping stone.

Kazi hizi alilipwa kwa hundi mbili tofauti ambapo hundi ya mwanzo ni nambari 9902097 ya tarehe 3 Juni, 2011 ambayo ililipwa kwa mchanganuo ufuatao.
Kwanza alilipwa ;

i. Tsh. 3, 038,500/- kwa ajili ya ununuzi wa mbolea na miti ya bustani.
ii. Tsh. 2, 704,560/- kwa ajili ya ununuzi wa vifaa.
iii. Tsh. 2, 506,320/- kwa ajili ya ununuzi wa vifaa.

Na Hundi ya pili ni Namba 074409 ya tarehe 23 Machi, 2012 ambayo alilipwa kwa ajili ya uuzaji wa *paving stone* kwa gharama ya Tsh. 4, 403,760/-.

Awamu ya pili alitakiwa kutengeneza njia ya watembeaji kwa miguu (njia ya Mkunazini) kwa kuweka *carbstone* na *bollard*, kazi ambayo hajapeleka makisio yake.

Pia, alieleza kwamba baada ya mafundi wa Baraza kushindwa kumalizia ujenzi wa eneo la Bodi ya Mapato Zanzibar – *Zanzibar Revenue Board (ZRB)* aliombwa kupeleka makisio ya kutengeneza eneo lile isipokuwa aliwauzia Baraza *cable stone* pekee na vifaa vilivyosalia kama vile udogo, saruji, mchanga vilipelekwa na Baraza la Manispaa. Ingawa kazi hii ilipewa Kampuni ya *Golden Group*, mafundi wa Baraza walitumika kwa kushirikiana na Kampuni hii. Kazi hii iligharimu Tsh. 5, 389,000/-.

Ndugu Ali aliendelea kwa kueleza kuwa mfumo kama huu hutumika zaidi endapo kutakuwa kuna kazi inayotakiwa haraka; kwa mfano alitengeneza bustani ya Ikulu ya Mnazi mmoja ambapo waliwauzia Baraza *cable stone* ambazo hadi anatoa taarifa hii fedha zake hajalipwa, isipokuwa alilipwa fedha za kununulia miti ambazo ni Tsh. 940,000/-. Vile vile, mafundi wake walishirikiana na mafundi wa Baraza.

Sambamba na hayo alieleza kwamba alipewa pia kazi ya kutengeneza Bustani eneo la mbele la Skuli ya Vikokotoni. Kazi hiyo imegharimu Tsh. 3, 140,000/-.

Kazi zote hizi hupewa na Mkurugenzi wa Baraza na huzitekeleza chini ya Mfanyakazi wa Baraza Ndugu Khamis Mwalim Khamis.

Mambo yaliyobainika na Kamati kufuatia Uchunguzi wa suala hili:-

Kamati imebaini kuwa;-

1. Ingawa kazi ya ujenzi hupewa Kampuni bado mafundi wa Baraza hutumika kusaidia kazi ile, jambo ambalo ni kinyume na utaratibu.

2. Shughuli za ujenzi zimetolewa bila ya kufuatwa utaratibu wa zabuni kwa zile kazi zenye gharama zinazohitaji hivyo.

3. Mjenzi alipewa fedha za kununulia miti kinyume na taratibu za manunuzi.

4. Baraza linanunua vifaa kama vile *bollard*, *paving stone* kwa mtu binafsi wakati lina uwezo wa kutengeneza vifaa hivyo. Pia, vifaa vinavyonunuliwa havina ubora ukilinganisha na vile vilivyokuwa vinatengenezwa na Baraza siku za nyuma.

Maoni ya Kamati.

Baada ya matokeo ya uchunguzi huo Kamati hii inapendekeza yafuatayo;-

1. Baraza liache tabia ya kukwepa masharti ya Sheria na Kanuni zilizopo na lifuate matakwa ya Sheria na Kanuni hizo.

2. Wafanyakazi wa Baraza la Manispaa wasishirikishwe au wasitumike kwenye kazi zilizopewa Kampuni, hata kama kazi hiyo inatakiwa haraka (yaani Kampuni iachiwe itafute mbinu za kumaliza kazi zake kwa wakati).

3. Kwa kuwa Baraza lina wataalamu wa fani mbali mbali, Kamati inalishauri Baraza kukabidhi kazi kwa wataalumu wake hao ili kuepuka kutumika vibaya fedha za walipa kodi wa nchi hii.

DIPLOMATIC SUPERMARKET YA MAZIZINI

Kamati ilitaka kujua utaratibu unaotumika wa kukodisha duka hilo. Katika kufuatilia hili Kamati ilikutana na Mkodishwaji wa duka hilo Ndugu Nassor Ali Hamad tarehe 29/08/2012 ambaye alieleza kwamba, yeye ni Mkodishwaji wa duka hilo kwa takriban miaka 19 sasa. Hadi mwaka 2004 alikuwa analipa kodi ya Tsh. 120,000/- kwa mwaka, lakini mnamo mwaka 2005 iliongezwa hadi Tsh. 400,000/-, aliomba kiwango hicho kipunguzwe na kilishushwa hadi Tsh. 250,000/- kwa mwaka. Mfumo wa mkataba wake ni wa mwaka moja mmoja na kila ukimalizika hutakiwa kufunga tena.

Ndugu Nassor aliendelea kueleza kuwa alipokuwa anataka kufunga mkataba mwengine '*renew contract'* Mkurugenzi wa Baraza alikataa kufunga mkataba na Mkodishwaji huyo. Kwa kuwa Mkodishwaji bado ana nia ya kuendelea kutumia eneo lile alipeleka malalamiko yake kwa Mhe. Waziri, Wizara ya Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ. Kutokana na malamiko yake hayo alitakiwa na Wizara kulipa kodi ya duka hilo Tsh. 2, 400,000/- katika akaunti ya Baraza la Manispaa iliyopo Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ).

Mnamo tarehe 15 Julai, 2011 alipokea barua ya kuhama kutoka kwa Mkurugenzi wa Baraza kwa hoja ya kuwa alifunga mkataba wa kukodi eneo lile kupitia Wizara iliyo chini yake, hivyo, Baraza halina mkataba na Mkodishwaji na kutakiwa kukabidhi jengo hilo sio zaidi ya tarehe 5 Januari, 2012.

Vile vile, alieleza kuwa tarehe 7 Septemba, 2011 alipokea barua nyengine kutoka Baraza la Manispaa inayokatisha matumizi ya jengo lile na alitakiwa kukabidhi jengo sio zaidi ya tarehe 16 Septemba, 2011 kwa kisingizio kwamba Manispaa imekamilisha taratibu zake za kuliimarisha eneo hilo, na endapo hatofanya hivyo atapelekwa Mahkamani.

Kutokana na hatua hiyo Mkodishwaji alipeleka malalamiko yake tena kwa Mhe. Waziri wa Wizara hii. Katika kufuatilia hili Wizara husika ilimtaka Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa kutochukua uamuzi wowote hadi hapo Uongozi wa Wizara utakapotoa maamuzi yake.

Vile vile, tarehe 5 Disemba, 2011 alipokea barua ya ukumbusho wa kuhama katika jengo hilo kutoka kwa Mkurugenzi na kutakiwa akabidhi jengo hilo sio zaidi ya tarehe 5 Januari, 2012 kwa kuwa Manispaa inataka kutumia sehemu ile kama Afisi pamoja na kuendeleza mali zake tangu mwaka 2010/2011.

Kwa hivi sasa Ndugu Nassor amekodishwa duka hilo na Wizara ya Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na muda wa kutumia eneo hilo unaishia mwezi wa Disemba, 2012.

Mkodishwaji wa *Diplomatic Supermarket* alizidi kueleza kwamba baadhi ya Madiwani na Mkurugenzi wa Baraza waliwahi kufika dukani hapo na kumtaka ahame na arejeshe funguo ndani ya wiki mbili. Ingawa Baraza linadai kuwa linahitaji kuimarisha eneo hilo kwa kutaka kujenga Afisi ya kisasa itakayojumuisha kumbi za kukodisha, Mkodishwaji hajapewa nafasi ya kufanya shughuli hiyo ijapokuwa uwezo wa kufanya hivyo anao.

Kamati ilibahatika pia kuonana na Mkurugenzi wa Manispaa katika kufuatilia suala hili ambaye alieleza kwamba Mkodishwaji alianza kufunga mikataba na Baraza tangu mwaka 2000, ingawa hapo kabla alikuwa anatumia eneo lile. Mnamo mwaka 2009 Baraza liligundua kwamba Mkodishwaji amewakodisha Shirika la Umeme miongoni mwa eneo la pale. Katika kufuatilia hili Mkodishwaji alikanusha jambo hilo, hata hivyo, Baraza lilipata ukweli baada ya Mkodishwaji kwenda kinyume na makubaliano yake na Shirika la Umeme baada ya kukiziba choo ambacho alikuwa akikitumia kama ni ghala ya kuwekea bidhaa zake. Kwa kuwa Mkodishwaji mkataba wake ulikuwa upo ukingoni, na kwa kuwa Baraza la Manispaa lilipitisha azimio la kutaka eneo lile lijengwe jengo la kisasa na tayari wameshaamua jinsi ya kujenga jengo hilo baada ya kutakiwa kuhama katika jengo wanalolitumia hivi sasa (Afisi Kuu) pamoja na kuchukuliwa kwa jengo lao la Mnazi Mmoja (Bustani ya Viktoria) kwa kupewa Chuo Kikuu cha Zanzibar - SUZA.

Mkodishwaji baada ya kuelezwa hivyo na Baraza, alipeleka barua katika Wizara inayohusika na Manispaa (Wizara ya Nchi, (AR), Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ) mnamo mwaka 2010 ya kutaka kuruhusiwa kuendelea kutumia jengo lile na kuanzia hapo Mkurugenzi alitakiwa asitishe hatua alizokuwa anataka kuchukua dhidi ya Mkodishwaji huyo, na Mkodishwaji alitakiwa kulipa fedha ya kodi moja kwa moja kwenye akaunti ya Baraza.

Sambamba na hilo alieleza kuwa Mkodishwaji aliwahi kumuandikia barua Makamo wa Pili wa Rais ya kuomba kuuziwa eneo lile.

Mkurugenzi aliendelea kueleza kwamba kwa kuwa hawana mtu maalum wa kujenga eneo lile, waliwahi kutoa tangazo la ujenzi katika vyombo vya habari lakini hakujitokeza mtu yeyote mwenye nia ya kutaka kujenga akiwemo Ndugu Nassor ambaye anatumia eneo hilo kwa hivi sasa. Kamati ilimtaka Mkurugenzi kuwasilisha nakala ya tangazo hilo, hata hivyo, hadi tunatoa taarifa hii Mkurugenzi huyo alishindwa kufanya hivyo kwa kisingizio kwamba baadhi ya nyaraka huibiwa na Watendaji wa Baraza.

Wakati wa mahojiano hayo, Kamati ilimtaka Mkurugenzi wa Baraza kuthibitisha kauli iliyoipata ya kuwa anataka kumuondoa Mkodishwaji katika eneo lile baada ya kupewa fedha na watu wawili tofauti ili wapatiwe eneo lile. Watu wenyewe ni Ndugu Kimti na Ndugu Muzammil. Mkurugenzi hakukubaliana na kauli hiyo na alizidi kusisitiza kuwa alimtaka Mkodishwaji kuhama kutokana na sababu alizozieleza hapo kabla.

Kamati haikutosheka na maelezo hayo na ilikutana na Mstahiki Meya ambaye alieleza kuwa alilishauri Baraza kuimarisha eneo lile kwa lengo la kujenga Afisi ya kisasa ili kuimarisha mapato. Suala hili tayari limeshapitishwa na Kamati ya Fedha na Uchumi na Baraza Zima. Alizidi kueleza kwamba alitoa rai hiyo baada ya kubaini kuwa miaka miwili imepita na Mkodishwaji anatumia eneo lile bila ya mkataba wowote na Baraza la Manispaa.

Baada ya Baraza kuchukua hatua za kumtaka Mkodishwaji arejeshe jengo lile kwa Mkodishaji, Mkodishwaji alimtumia Waziri wa Wizara husika Dkt. Mwinyihaji Makame ambaye alililazimisha Baraza kumuacha Mkodishwaji kuendelea kutumia jengo lile, ingawa hana mamlaka ya kufanya hivyo. Aidha, Mkodishwaji aliwahi kumuandikia barua Makamo wa Pili wa Rais kuhusu kuuziwa eneo lile.

Kwa kuwa Baraza la Manispaa ndilo lenye mamlaka ya kuamua mambo ya Baraza kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha Sheria Namba 3 ya 1995, Katibu Mkuu wa Wizara husika Ndugu Salum Maulid alimshauri kwa mdomo Mstahiki Meya kuwasilisha mpango wao huo kwa Mheshimiwa Rais, lakini hadi Mstahiki Meya anatoa taarifa hizi tarehe 04 Septemba, 2012 hakuna michoro wala ramani ambayo wamependekeza kujengwa eneo lile.

Kamati ilimtaka pia Mstahiki Meya kuthibitisha kauli ilizozipata ya kuwa Mkurugenzi anataka kumuondoa Mkodishwaji katika eneo lile baada ya kupewa fedha na watu wawili tofauti ili wapatiwe eneo lile, na kwa upande mwengine Mheshimiwa Waziri wa Wizara husika amepewa fedha na Mkodishwaji ili aendelee kukodishwa eneo hilo, na ndio maana Mkodishwaji hivi sasa anatumia eneo husika kwa nguvu za Wizara. Katika kulitolea maelezo suala hili, Mstahiki Meya alieleza kuwa alizipata taarifa hizi kupitia kikao kilichoitishwa na Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii kilichowajumuisha Mkuu wa Mkoa wa Mjini Maghribi, Mkuu wa Wilaya ya Mjini, Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa na Watendaji wengine wa Wizara husika.

Kamati haikuishia hapo alifanya mahojiano pia na Waziri wa Wizara hii (Mheshimiwa Dkt. Mwinyihaji Makame) ambaye alieleza kwamba ni kweli kuwa Wizara yake imetoa barua ya kumtaka Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa kusitisha zoezi la kumhamisha Mkodishwaji wa eneo lile baada ya kupokea malalamiko hayo kutoka kwa

Mkodishwaji wa duka hilo, Watendaji wa Wizara yake pamoja na baadhi ya Madiwani kumfuata na kumtaka awasaidie kutatua suala hili.

Alieleza kwamba pamoja na yote hayo mvutano baina ya Mkurugenzi wa Baraza na Mkodishwaji wa duka hilo ulianza tokea Baraza lipo chini ya Wizara ya Nchi, (AR), Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ na Mheshimiwa Waziri wa Wizara hiyo (Mheshimiwa Othman Nyanga) kuingilia kati baada ya Mkurugenzi wa Baraza kutompatia mkataba wa nyongeza Mkodishwaji wa eneo hilo pamoja na kumueleza kuwa hana fedha za kuendesha biashara katika eneo lile.

Kwa kuwa Serikali ina mpango wa kuimarisha eneo la Mazizini Mheshimiwa Dkt. Mwinyihaji aliliomba Baraza la Manispaa kuwasilisha mpango wao kwake ili auwasilishe mbele ya Baraza la Mapinduzi. Sambamba na hayo alieleza kwamba makosa yote hayo hujitokeza kwa kuwa Baraza la Manispaa halifuati taratibu za kisheria zilizopo.

Katika mahojiano hayo, Kamati ilimtaka Mheshimiwa Waziri kuthibitisha kauli iliyoipata ya kuwa anataka Mkodishwaji aendelee kuwepo dukani hapo kwa kuwa amempatia fedha. Kwa upande wa tuhuma hizo alieleza kuwa hiyo ni fitna tu na hakuna ukweli ndani yake.

Mambo yaliyobainika na Kamati kufuatia Uchunguzi wa suala hili:-

Kamati imebaini mambo yafuatayo;-

1. Maamuzi ya Waziri ya kuliandikia barua Baraza la Manispaa ya kusitisha zoezi la kumhamisha Mkodishwaji wa duka hilo ni kinyume na masharti ya kifungu cha 62 cha Sheria Namba 3 ya 1995. Hii ni kutokana na kuwa kifungu hiki kinamtaka kwanza Waziri afanye uchunguzi wa jambo husika na endapo atagundua kuwa Baraza la Manispaa linatekeleza majukumu yake kinyume na utaratibu basi atoe taarifa kupitia Gazeti Rasmi la Serikali na hatua nyengine ziendelee. Kwa msingi huo kitendo cha Waziri cha kumuongezea muda Mkodishwaji hakina uhalali.

2. Baraza na Kamati ya Fedha na Uchumi zilipitisha Azimio la kujengwa au kuimarishwa eneo la Mazizini liliopo duka la Diplomatic.

3. Kamati ina wasiwasi juu ya baadhi ya Viongozi akiwemo Mheshimiwa Waziri na Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa kupokea fedha kwa ajili ya kutoa maamuzi ya upendeleo.

4. Hakuna tangazo lolote lililotolewa kuhusiana na uimarishaji wa eneo la *Diplomatic Super Market*.

5. Kumbukumbu za Vikao ya Baraza Kuu zinaonesha kuwa kumbukumbu zimeandikwa mwanzo na vikao ndio vikafuata. Kwa mfano; Kikao Namba 1/2012 kilifanyika tarehe 6 Machi, 2012 wakati kumbukumbu zimeandikwa tarehe 12 Machi, 2011. Aidha, Kikao Namba 2/2012 kilifanyika tarehe 6 Juni, 2012 wakati kumbukumbu zimeandikwa tarehe 11 Juni, 2011.

Hatua za Kuchukuliwa na maoni ya Kamati kutokana na matokeo ya uchunguzi huo

Kamati inapendekeza yafuatayo;-

1. Waziri kabla ya kuchukua hatua azingatie zaidi matakwa ya Sheria mbali mbali kuliko utashi ili kuepuka mvutano usio wa lazima.

2. Serikali kwa kupitia Makamo wa Pili wa Rais ichunguze tuhuma zilizotolewa dhidi ya viongozi hawa, na endapo itathibitika hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya wote waliohusika.

3. Kamati inalishauri Baraza la Manispaa kuitisha zabuni kwa ajili ya ujenzi wa eneo hilo.

4. Kwa kuwa kuna mgongano wa tarehe katika kumbukumbu za vikao, Kamati inawashauri Watendaji wa Baraza wawe makini wakati wa kuandaa kumbukumbu mbali mbali za vikao.

UNUNUZI WA BASI LA AFISI

Kamati ilifuatilia taratibu zilizotumika wakati wa ununuaji wa basi la kuhudumia wafanyakazi wa Baraza. Katika kupata ufafanuzi wa suala hili Kamati iliwahoji baadhi ya Watendaji wa Baraza, Muuzaji wa basi hilo (Ndugu Abdalla Moh'd Nassor) pamoja na Mkurugenzi wa Baraza.

Kwa upande wa Watendaji, Afisa Utawala (Ndugu Mwanakhamis) aliieleza Kamati kwamba kutokana na kilio cha siku nyingi cha Wafanyakazi wa Baraza kuhusu kupatiwa usafiri alimuandikia barua ya maombi Mkurugenzi wa Baraza ambaye aliruhusu kununuliwa kwa basi. Hata hivyo, hajui Mnunuzi alipatikana vipi na wala haelewi kama manunuzi yamepitishwa na Baraza Zima, isipokuwa, anajua kuwa Kamati ya Fedha na Uchumi imeridhia ununuzi ule.

Alizidi kueleza kwamba basi hilo lilinunuliwa kwa Tsh. 40, 000,000/- bila ya kutolewa zabuni, na katika kujiridhisha kama basi hilo halina matatizo lilikaguliwa na Fundi Mkuu wa Baraza.

Kamati ilimhoji pia muuza basi Ndugu Abdalla Moh'd Nassor ambaye alieleza kwamba aliwahi kuliuzia basi aina ya *Coaster* Baraza la Manispaa baada ya kupokea barua ya maombi kutoka kwa Mkurugenzi wa Baraza hilo ambalo liligharimu Tsh. 40, 000,000/-, ingawa baadhi ya watu hususan mafundi walimtaka aongeze fedha ili wachukue wao lakini hakufanya hivyo. Basi lililonunuliwa lilikuwa tayari lipo kwenye *show room* yake hapo Mbweni. Kutokana na barua hiyo aliwasilisha '*invoice'* na alilipwa fedha zake katika awamu tatu. Mkurugenzi pamoja na Fundi Mkuu wa Baraza walifika kulikagua basi hilo na kuridhika nalo.

Alizidi kueleza kuwa mbali ya basi hilo aliwahi pia kuwauzia Baraza gari aina ya *Canter* kwa njia hiyo hiyo ya barua mnamo mwezi wa Juni, 2010 kwa gharama ya Tsh.18, 000,000/- na baada ya mwezi mmoja ndio aliuza basi hilo kwa Baraza.

Katika kulitolea ufafanuzi suala hili Mkurugenzi wa Baraza alieleza kuwa ni kweli kwamba Baraza lilinunua basi kwa Muuzaji huyo na kwa gharama hizo. Pia, alieleza kuwa alinunua basi hilo kwa kufuata kifungu cha 38(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uuzaji wa Mali za Serikali Namba 9 ya 2005.

Mambo yaliyobainika na Kamati kufuatia Uchunguzi wa suala hili:-

Baada ya kuchukunguza hili Kamati imebaini mambo yafuatayo;-

1. Ingawa Mkurugenzi katumia kifungu cha 38(1) cha Sheria Namba 5 ya 2005 Kamati haikubaliani na maamuzi yake hayo. Hii ni kutokana na kuwa kifungu hicho hutakiwa kutumika endapo kutakuwa na uharaka wa kile kinachotaka kununuliwa. Kwa msingi huo, ununuzi wa basi lile haukuhitaji kufanywa kwa haraka na hasa tukizingatia kuwa wauzaji wa gari wapo wengi. Hivyo, palikuwa na muda mzuri wa kutafuta kwa wauzaji wengine ili kulinganisha bei.

2. Baraza kwa makusudi limekiuka Kanuni ya 55 ya Kanuni za Baraza, ambayo inamtaka Mkurugenzi kutoa tangazo la kuitisha zabuni.

3. Kauli ya Ndugu Abdalla (Muuzaji wa basi) aliyoitoa mbele ya Kamati ya kuwa aliliuzia gari mbili Baraza kwa maombi tofauti (katika miezi tofauti) inapingana na barua ya tarehe 12 Mei, 2010 iliyotumwa kwake na Baraza la Manispaa.

Maoni ya Kamati

Kamati inapendekeza mambo yafuatayo:-

1. Watendaji wa Baraza la Manispaa wakiongozwa na Mkurugenzi kufuata matakwa ya Sheria kiukamilifu na sio kuyafumbia macho baadhi ya masharti kwa maslahi yao binafsi.

2. Maamuzi yote ya Kamati za Kudumu za Baraza la Manispaa yawasilishwe mbele ya Baraza kwa kuidhinishwa, jambo hili litasaidia kila Diwani kujua kinachoendelea ndani ya Baraza la Manispaa.

HADIDU REJEA YA TATU

KUCHUNGUZA TARATIBU ZA UAJIRI NA UPANDISHAJI VYEO KATIKA BARAZA LA MANISPAA, NA KAMA TARATIBU HIZO ZINAZINGATIA SIFA ZINAZOHITAJIKA KWA NAFASI HUSIKA.

Utangulizi

Kamati ilitakiwa pia kuchunguza taratibu za uajiri na upandishaji vyeo katika Baraza la Manispaa na kama taratibu hizo zinazingatia sifa zinazohitajika kwa nafasi husika. Katika kutekeleza jukumu hili, Kamati ilitaka kujua utaratibu unaotumika wakati wa uajiri pamoja na utaratibu wa kuwapandisha vyeo Maafisa wake na kujiridhisha iwapo upandishaji vyeo huo unazingatia sifa kwa nafasi husika.

Kamati katika kufuatilia hadidu rejea hii ilikutana na kufanya mahojiano na Madiwani tarehe 4 Juni, 2012, Afisa Utawala ambaye pia ni Mkuu wa Idara ya Sheria na Utawala tarehe 27 Agosti, 2012 katika Afisi ya Baraza la Wawakilishi – Zanzibar.

Pia, Kamati ilifanya mahojiano na Madiwani ambao ndio wenye mamlaka ya kuteua Watumishi kwa mujibu wa kifungu cha 25 cha Sheria Namba 3 ya 1995. Aidha, tulihojiana na Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa kwa kuwa ndie Mtendaji Mkuu wa Taasisi hiyo.

Katika kuona kwamba hadidu rejea hii inapata majibu yaliyo muafaka, vile vile Kamati haikusita kuzungumza na wahusika ambao kwa namna moja au nyengine wamepata nafasi ya kupandishwa vyeo katika taasisi hii ambapo Kamati ilimuhoji Mkuu wa Idara ya Mipango Miji tarehe 5/6/2012 katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi sambamba na Kaimu Mhasibu Mkuu wa Baraza la Manispaa, pamoja na Mkuu wa Idara ya Sheria na Utawala.

Baada ya utangulizi huo sasa ni vyema tukapata uchambuzi wa hadidu rejea hii.

Uchambuzi wa hadidu rejea husika

Baraza la Manispaa kama zilivyo taasisi nyengine za Serikali zinawajibika kufuata utaratibu maalum katika kuajiri wafanyakazi wake kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma. Uajiri huo lazima utambuliwe na Tume ya Utumishi Serikalini na baada ya kupata kibali hicho ndipo taasisi inaporuhusiwa kuendelea na taratibu nyengine. Hivyo, kwa upande wa Baraza la Manispaa baada ya kupata ruhusa hiyo, Baraza kwa kupata ridhaa ya Waziri mwenye dhamana na Baraza la Manispaa linaweza likateua na kupanga stahiki za baadhi ya Maafisa kwa mujibu wa kifungu cha 25 cha Sheria ya Baraza la Manispaa, Namba 3 ya 1995.

Kuchunguza uajiri wa Wafanyakazi 83

Katika kufuatilia suala hili la uajiri, Kamati ilitaka kufahamu juu ya taratibu zilizotumika kuwaajiri Wafanyakazi 83 ambao walikuwa ni wafanyakazi wa kutwa kwa muda wa takriban miaka 30 na baadae kuajiriwa kuwa ni wafanyakazi wa kudumu.

Afisa Utawala wa Baraza la Manispaa aliieleza Kamati kwamba uajiri wa watu hao baada ya kupata ruhusa kutoka Wizara yenye dhamana na mambo ya Utumishi hayakupita katika mkutano wowote wa Baraza la Manispaa kwa ajili ya kupata ridhaa, na badala yake Mkurugenzi wa Baraza aliwaajiri vijana hao moja kwa moja kwa kuwa alisharuhusiwa na Baraza lililopita (2005 – 2010), ingawa katika mwaka 2010 Serikali haikuwa tayari kuajiriwa watu wa namna hiyo.

Kwa kuwa Serikali iliamua kutokuwa na waajiriwa wa kutwa, mnamo mwezi wa Julai, 2011 Baraza liliruhusiwa kuwafanyia uajiri vijana hao. Baada ya uajiri kufanyika na Madiwa wapya kubaini hilo walianza kulalamika na ndipo Mkurugenzi wa Baraza alipolazimika kutoa maelezo kwa uamuzi wake huo aliouchukua, na baadae aliomba radhi kwa maandishi.

Katika kufuatilia hili Kamati ilifanya majadiliano na Mstahiki Meya ambaye alieleza kwamba ni kweli ajira ya vijana hao haikuridhiwa na Baraza jipya la Manispaa kwa kisingizio kwamba tayari azimio la ajira hiyo

limeshapitishwa na Baraza lililopita. Katika kupata ushahidi wa jambo hilo Mstahiki Meya aliomba kupatiwa kumbukumbu ya kikao hicho, hata hivyo, Watendaji wa Baraza walishindwa kumpatia kumbukumbu hizo.

Alizidi kueleza kwamba, sio kweli kwamba vijana wote 83 walioajiriwa ni wa kutwa, isipokuwa wameingizwa na vijana wengine ambao hawahusiki.

Kuchunguza Taratibu za Upandishaji vyeo Kwa Watendaji.

Katika kipengele hichi Kamati imechunguza na kufuatilia taratibu za upandishaji vyeo kwa Watendaji wa Baraza la Manispaa na kama taratibu hizo zinazingatia sifa za nafasi husika.

Kwa mujibu wa kifungu cha 51 cha Sheria Namba 3 ya 1995 Baraza la Manispaa lina jumla ya Idara Tano kama zifuatazo;-

i. Idara ya Fedha na Maendeleo ya Uchumi;
ii. Idara ya Mipango Miji;
iii. Idara ya Utawala na Sheria;
iv. Idara ya Kazi, Ujenzi na Mazingira; na
v. Idara ya Huduma za Jamii.

Katika kuchunguza hili Kamati ilitaka kujua elimu pamoja na uzoefu wa Wakuu wa Idara hizi. Kamati ilitumia njia ya '*sampling'* katika kupata taarifa za kipengele hiki. Kwa msingi huo, kati ya Idara Tano za Baraza la Manispaa, Kamati ilihoji sifa za Wakuu wa Idara Tatu za mwanzo kama ifuatavyo;-

i. Ndugu Eshe Juma Abdalla; Ni Kaimu Mhasibu Mkuu wa Baraza la Manispaa ambaye alipandishwa katika nafasi hiyo tokea mwaka 2009. Cheo hicho alipandishwa kupitia barua yenye kumbukumbu namba MFEA/M.30/4/09/VOL.V/174 ya tarehe 5/11/2009 kutoka Wizara ya Fedha na Uchumi Zanzibar na Dokezo la tarehe 11 Novemba, 2009 lenye kumbukumbu Namba TM/1/C/VOL.11 lililotoka kwa Afisa Utawala wa Baraza la Manispaa. Mtendaji huyu ana elimu ya Shahada ya Kwanza ya Uongozi wa Biashara - *Degree* in Business *Administration*.

ii. Ndugu Khamis Mwalimu Khamis; Ni Mkuu wa Idara ya Mipango Miji ya Baraza la Manispaa, amekuwa akishikilia nafasi hiyo tokea mwaka 2009. Alipewa dhamana hiyo kupitia Dokezo la tarehe 30 Septemba, 2009. Mtendaji huyu ana elimu ya '*Full Technician Certificate - F.T.C in Civil Engineering* na uzoefu wa kazi wa miaka 7.

   Kamati katika kufuatilia hili, ilitaka kujua Ndugu Khamis aliteuliwa na nani kushika wadhifa huo, ambapo ilipomhoji Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa alieleza kwamba wakati anateuliwa kuwa Mkurugenzi tayari Ndugu Khamis alikuwa ameshateuliwa kuwa Mkuu wa Idara hiyo.

iii. Ndugu Mwanakhamis Salum Omar; Ni Mkuu wa Idara ya Utawala na Sheria, amepewa nafasi hiyo tokea mwaka 2009 kupitia Dokeza la tarehe 30 Septemba, 2009 lenye kumbukumbu namba TAA/THA/M.01052/C/86. Alipewa nafasi hiyo baada ya kupendekezwa na aliyekuwa anashikilia cheo hicho Ndugu Maryam Marshed. Ili Ndugu Maryam aruhusiwe kwenda masomoni alitakiwa na Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa kumpendekeza Afisa atakayeshika nafasi yake hiyo kwa muda wa miezi mitatu na baadae Baraza litaajiri mtu mwengine.

   Ndugu Mwanakhamis kabla ya kushika cheo hiki alikuwa ni Mhasibu wa Mradi wa Maji Machafu, Michirizi na Taka. Mtendaji huyu ana elimu ya Stashahada ya Uongozi wa Biashara katika mambo ya Fedha - *Diploma in Bussiness Administration in Accounting*.

Majukumu ya Mkuu wa Idara ya Utawala na Sheria ni kusimamia watumishi kwa kuandaa mishahara yao, '*nominal roll'* na mengineyo. Hata hivyo, kwa upande wake alieleza kuwa hakuwahi kupewa '*job description'* hadi anawasilisha taarifa hii tarehe 27 Agosti, 2012.

Muhtasari wa mambo yaliyobainika katika hadidu rejea hii.

Baada ya kufuatilia suala hili Kamati imebaini mambo yafuatayo;-

1. Sheria na Kanuni za uajiri na upandishwaji wa vyeo katika Baraza la Manispaa hazifuatwi kwa baadhi ya watendaji.

2. Ingawa uajiri wa wafanyakazi 83 ulifanywa kinyume na utaratibu lakini uajiri huo ulikuwa sahihi.

3. Kwa kuzingatia Dokezo la tarehe 30 Septemba, 2009 inadhihirisha wazi kwamba Ndugu Khamis ameteuliwa na Mkurugenzi Rashid kushika wadhifa huo kwa kuwa yeye ndiye aliyeweka saini Dokezo hilo.

4. Utaratibu wa upandishaji vyeo katika Baraza la Manispaa hauzingatii sifa kwa nafasi husika, bali hufanywa kwa upendeleo. Kwa mfano, kwa kuzingatia Sheria ya Fedha za Umma, Namba 12 ya 2005, Afisa Uhasibu ametafsiriwa kuwa ni afisa mwenye angalau Cheti cha Uhasibu kutoka Chuo kinachotambulika na anayefanya kazi katika Kitengo cha Uhasibu cha Wizara au Idara. Kutokana na kifungu hicho Ndugu Eshe Juma Abdalla hakupaswa kushika nafasi hiyo hata kama anakaimu, kwa kuwa hana taaluma ya mambo ya Uhasibu, ingawa aliwahi kufanya shughuli hizo. Hii ni kutokana na kuwa kifungu hicho kinamtaka Afisa Uhasibu awe na mambo yote mawili.

   Vile vile, Ndugu Khamis Mwalimu Khamis ameteuliwa kuwa Mkuu wa Idara Mipango Miji wakati kuna mfanyakazi anayeitwa Azzan Salum Khatib mwenye elimu ya *Advanced Diploma in Mechanical Engineering* na uzoefu wa miaka 30 hakupewa nafasi hiyo.

   Aidha, Ndugu Mwanakhamis Salum Omar hakustahiki kupewa nafasi hiyo hasa tukizingatia kuwa elimu aliyokuwa nayo inahusiana na Uongozi katika mambo ya Fedha tu.

5. Mkurugenzi anatumia madaraka aliyokuwa nayo kwa maslahi yake binafsi.

6. Watumishi wa Baraza la Manispaa hawapewi '*job description'* kitu ambacho ni kinyume na taratibu za kazi.

7. Mkuu wa Idara ya Utawala na Sheria anafanya shughuli zaidi za Afisa Utumishi.

Hatua za kuchukuliwa kutokana na hadidu rejea hii.

Kamati inapendekeza hatua zifuatazo zichukuliwe;

1. Mkurugenzi awajibishwe kwa mujibu wa Sheria kwa kutofuata Sheria mbali mbali za nchi.

2. Mkurugenzi achukuliwe hatua za kisheria kwa mujibu wa kifungu cha 22 cha Sheria Namba 4 ya 2007 kwa kutoa taarifa za uongo mbele ya Kamati kuhusiana na uteuzi wa Ndugu Khamis.

3. Serikali kwa kupitia Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora iupitie muundo wa utumishi wa Baraza la Manispaa, kwa lengo la kuweka utaratibu maalum wa upandishaji vyeo, pamoja na kuandaliwa sifa za watumishi kwa mujibu wa Idara na nafasi husika.

4. Watendaji waliopandishwa vyeo bila ya kuwa na sifa katika nafasi husika waondolewe mara moja na kuwekwa wale wanaostahiki.

5. Watendaji wa Baraza la Manispaa watekeleze majukumu yao kwa mujibu wa taaluma zao na maadili yao ya kazi, na waachane na tabia ya kufuata amri za Mkurugenzi.

HADIDU REJEA YA NNE

KUCHUNGUZA UTENDAJI WA MKURUGENZI WA BARAZA LA MANISPAA JUU YA TUHUMA ZA KUTOFUATA SHERIA NA KANUNI KWA MAKUSUDI, UBADHIRIFU WA FEDHA NA KUHUSIKA KWAKE KATIKA MIGOGORO INAYOLIKUMBA BARAZA LA MANISPAA.

Utangulizi

Kamati ilitakiwa pia kuchunguza utendaji wa Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa Zanzibar juu ya tuhuma za kutofuata Sheria na Kanuni kwa makusudi, ubadhirifu wa fedha na kuhusika kwake katika migogoro inayolikumba Baraza la Manispaa Zanzibar.

Katika kufuatilia hadidu rejea hii, Kamati ilifanya mahojiano na watu mbali mbali akiwemo Mheshimiwa Waziri wa Wizara husika, Mstahiki Meya, Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa, baadhi ya Watendaji wa Baraza la Manispaa, Wateja wa Baraza na baadhi ya Wafanyabiashara mbali mbali pamoja na kuzingatia uzoefu wa kazi wa Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa.

Uchambuzi wa hadidu rejea husika.

Kwa mujibu wa kifungu cha 11(1) cha Sheria ya Baraza la Manispaa Namba 3 ya 1995, Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa ndio Mtendaji Mkuu wa Taasisi hiyo ya umma. Mtendaji huyu anatakiwa kuwa ni kioo na mfano kwa watendaji wengine anaowaongoza. Kwa mnasaba huo, anatakiwa kufuata misingi yote ambayo kiongozi anatakiwa kuwa nayo katika utendaji wake wa kazi za kila siku, ili kufikia malengo yaliyokusudiwa ya uanzishwaji wa Taasisi hii.

Kuchunguza juu ya tuhuma za kutofuata kwa Sheria na Kanuni kwa makusudi:

Mhe. Mwenyekiti, utendaji wa Baraza la Manispaa unatakiwa ufuate Sheria na Kanuni mbali mbali za nchi kama zilivyo taasisi nyengine. Hivyo, kwa kuzingatia kifungu cha 11(2) cha Sheria Namba 3 ya 1995, Mkurugenzi wa Baraza anapaswa kutekeleza majukumu yake kwa kufuata Sheria hii na Sheria nyengine yoyote.

Mambo yaliyobainika katika tuhuma hii:

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuzingatia taarifa mbali mbali zilizotolewa na watu tuliowataja hapo kabla pamoja na uzoefu wa kazi wa Mkurugenzi, Kamati hii inadiriki kutamka kwamba Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa hafuati Sheria na Kanuni za nchi kwa makusudi kwa lengo la kujinufaisha.

Baadhi ya vifungu alivyovikiuka wakati wa utendaji wake ni kama ifuatavyo:-

1. Kifungu cha 20(2) cha Sheria Namba 3 ya 1995, kinachoelekeza kwamba mikataba yote itakayoingiwa na Baraza itatiwa muhuri wa Baraza mbele ya Meya au Naibu Meya, na Mkurugenzi au Afisa mwengine wa Baraza atakayeidhinishwa kwa niaba ya Mkurugenzi kwa kibali au Azimio la Baraza.

   Vile vile, kanuni ya 55(b) ya Kanuni za Baraza la Manispaa inaelekeza kwamba mikataba yote itakayofungwa na Baraza ambayo thamani yake itazidi shilingi 5, 000,000/= ni lazima kipate kibali cha Baraza Zima.

   Kwa mujibu wa maelezo yetu tuliyoyatoa katika vipengele mbali mbali hukusiana na mikataba tumebaini kuwa hakuna mkataba hata mmoja uliofungwa na Baraza ukafuata maelekezo hayo.

2. Taratibu za upandishaji vyeo kwa Watendaji wa Baraza huwa hazifuatwi bali hufanywa kienyeji tu. Hii ni kutokana na kuwa kwa mujibu wa kanuni ya 28(a) ya Kanuni za Utumishi Serikalini za mwaka 1997 ambazo zilikuwa zinatumika, wakati ule zilieleza kwamba ili mfanyakazi apandishwe cheo lazima kuwe na nafasi mbali ya uwezo na elimu kwa anayependekezwa.

Vile vile, katika aya ya (d) ya kanuni hii imelezwa kwamba lazima kuwe na nafasi tupu ambayo lazima itangazwe lakini katika kujaza nafasi hiyo kipaumbele apewe mfanyakazi anayeongoza kwa ukubwa na mwenye sifa zinazohitajika. Endapo itathibitika kwamba yule aliyeongoza katika orodha ya ukubwa hatazimudu kazi au dhamana za madaraka atayopewa, nafasi hiyo itajazwa na mfanyakazi mwengine atayeonekana ana sifa zinazohitajika**.**

Kwa mnasaba huo mambo yote hayo hayakuzingatiwa na Baraza la Manispaa wakati wa kupandishwa vyeo watendaji hao.

3. Baada ya Mkurugenzi wa Baraza kuruhusiwa na serikali kuajiri wafanyakazi 83 wa kutwa, alipaswa kutoa taarifa mbele ya Baraza liliopo. Hata hivyo, alichukua hatua bila ya kuliarifu Baraza hilo.

4. Katika suala la uidhinishaji wa matumizi hakuna mtiririko maalum unaofahamika katika Baraza la Manispaa, kwa kuthibitisha hili tafadhali angalia kipengele cha 3.3.0 cha ripoti hii. Hii ni kutokana na kuwa Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa humtumia zaidi Afisa Utawala ambaye ana hadhi sawa na Wakuu wengine wa Idara kwa mujibu wa vifungu vya 51 na 53 vya Sheria ya Baraza la Manispaa Zanzibar Namba 3 ya 1995. Aidha, Kanuni za Baraza Sehemu ya Nne na ya Sita hazimtambui Afisa huyu katika masuala ya matumizi.

5. Kwa upande wa manunuzi, utaratibu uliowekwa na Kanuni za Baraza la Manispaa na Sheria ya Manunuzi na Uuzaji wa Mali za Serikali haufuatwi. Kwa mfano, Baraza lilinunua basi kwa ajili ya usafiri kwa watendaji wake. Tafadhali angalia ukurasa wa 52 na 53 wa ripoti hii kwa maelezo zaidi.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, wale ambao wako nje tunaomba waingie ndani kwa sababu Mhe. Mwenyekiti anaendelea kumalizia, ili tuweze kupitisha hii hoja na wahudumu tusaidieni katika hilo. Mhe. Mwenyekiti, endelea.

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Kuchunguza Utendaji wa Baraza la Manispaa):

Kuchunguza juu ya tuhuma za ubadhirifu wa fedha:
Mhe. Mwenyekiti, Kamati haikugundua ubadhirifu wa moja kwa moja wa fedha katika Baraza la Manispaa, lakini kuna ukiukwaji mkubwa wa sheria ambao unaashiria ubadhirifu wa fedha za umma.

Kuchunguza juu ya tuhuma ya kuhusika kwake katika migogoro inayolikumba Baraza la Manispaa:

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuzingatia maelezo mbali mbali tuliyoyatoa, Kamati hii inathubutu kusema kwamba Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa anahusika kufanyika kwa migogoro katika Baraza.

Baadhi ya mambo ambayo yametokea na kusababisha migogoro ni pamoja na;

1. Kitendo cha kuwaondosha Wafanyabiashara waliokuwa wanauza ndizi katika Soko la Darajani kwa ajili ya ujenzi wa maduka kumi na tatu bila ya kuwapatia eneo jengine. Kwa maelezo zaidi tafadhali angalia ukurasa wa 36 na 37 wa ripoti hii.

   Halikadhalika, aliwaondosha wafanyabiashara katika eneo la mboga mboga katika Soko la Darajani, kwa ajili ya ujenzi wa maduka kumi na sita bila ya kuwapatia eneo jengine. Kwa maelezo zaidi tafadhali angalia ukurasa wa 40 na 41 wa ripoti hii.

2. Mkurugenzi wa Baraza alishindwa kutoa taarifa kwa zile kampuni zilizovunja mkataba. Ingawa kipengele cha 1.1 cha mikataba hiyo hakimlazimishi kufanya hivyo, ila kwa kanuni za kawaida za utawala (*Routine Administrative Procedure*) alitakiwa kutoa taarifa hiyo, ili kuepusha migongano. Kitendo cha kufuta mikataba bila ya kuwajulisha wahusika kilileta vurugu baina ya kampuni hizo. Kwa maelezo zaidi tafadhali angalia ukurasa wa 6 hadi 15 wa ripoti ya Kamati hii.

3. Amehusika na mgogoro baina ya Baraza la Manispaa na Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi, kutokana na kitendo chake cha kukusanya ada ya leseni kwa wafanyabiashara wa ndani katika Soko la Mwanakwerekwe. Jambo hilo lilipelekea Mhe. Waziri wa Wizara husika kutoa agizo la kumtaka Mkurugenzi huyo kurejesha fedha hizo ambazo ni shilingi 10, 000,000/=. Pamoja na wizara kumuandikia barua mbali mbali Mkurugenzi kuhusiana na malipo hayo, hadi tunaandaa taarifa hii fedha hizo hazijalipwa.

Hatua za kuchukua kutokana na uchunguzi huo:

Mhe. Mwenyekiti, Kamati hii inapendekeza hatua zifuatazo zichukuliwe dhidi ya Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa:-

1. Awajibishwe kwa mujibu wa sheria za nchi.

2. Kuwalipa fidia wale wote walioathirika kwa namna moja au nyengine kutokana na matendo yake.

HITIMISHO:

Mhe. Mwenyekiti, Kamati Teule imekamilisha uchunguzi kuhusu utendaji wa Baraza la Manispaa. Kamati hii imekamilisha jukumu hilo kwa kufanya mahojiano na watu mbali mbali, kupitia Sheria, Kanuni, nyaraka mbali mbali na kufanya ziara katika maeneo mbali mbali kutokana na hadidu rejea husika kama ilivyooneshwa katika utangulizi wa ripoti hii.

Matokeo ya uchunguzi huu yamebainisha kwamba asilimia kubwa ya utendaji ndani ya Baraza la Manispaa unakiuka Sheria na Kanuni mbali mbali zilizopo. Jambo hili huchangia kwa kiasi kikubwa kuleta migongano au migogoro baina ya watendaji, wateja wa Baraza, Madiwani na jamii kwa ujumla.

Kamati Teule imebaini kuwa makosa yote hayo hufanywa ili kuwanufaisha baadhi ya Watendaji ndani ya Baraza la Manispaa. Hii ni kutokana na kuwa watendaji wa Baraza la Manispaa hutekeleza majukumu yao kinyume na taaluma zao na maadili yao ya kazi kwa kutekeleza au kufuata amri au maelekezo ya Mkurugenzi.

Vile vile, baadhi ya wateja wa Baraza la Manispaa wamediriki kuidanganya Kamati hii kwa lengo la kuficha ukweli unaotendeka katika Baraza hili.

Baraza la Manispaa halimshirikishi Mhe. Waziri husika kwa yale mambo anayohusika nayo kwa mujibu wa Sheria Namba 3 ya 1995.

Kwa kuwa asilimia kubwa ya mikataba inayofungwa na Baraza haimshirikishi Mwanasheria wake, Kamati imebaini kuwa takriban mikataba yote ina mapungufu ya kisheria.

Kwa kuwa serikali inalitumia Baraza la Manispaa kama ni chombo cha kuwapeleka watendaji waliofanya makosa (watendaji wahalifu) katika taasisi zao, Kamati imebaini kuwa kitendo hiki kinalifanya Baraza kukabiliwa na tatizo la wizi wa nyaraka, watendaji kughushi nyaraka na mambo mengi mengineyo ambayo ni kinyume na maadili ya kazi.

Jambo hili lilithibitishwa na Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa mbele ya Kamati hii, tarehe 3 Septemba, 2012, sambamba na barua yake ya tarehe 5 Septemba, 2012 yenye kumbukumbu Namba ZMC/BW/2 VOL.111/103 na tarehe 13 Septemba, 2012 ambayo haina kumbukumbu.

Mkurugenzi wa Baraza na watendaji wake hawazijui sheria za nchi na kanuni zake hususan zile wanazozifanyia kazi. Hata hivyo, ni msingi wa Sheria kwamba kutokujua sheria sio utetezi *'Ignorance of Law is not a defence'*.

MAPENDEKEZO YA KAMATI TEULE KWA UJUMLA:

Mhe. Mwenyekiti, kufuatia changamoto mbali mbali za kiutendaji zilizojitokeza ndani ya Baraza la Manispaa, Kamati hii inapendekeza yafuatayo:-

1. Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa na wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyengine kutofuata sheria na kanuni mbali mbali kuchukuliwa hatua za kisheria.

2. Wateja wa Baraza la Manispaa waliodhulumiwa haki zao warejeshewe wenyewe kwa kuzingatia thamani halisi ya fedha.

3. Baraza la Manispaa liyafanyie matengenezo masoko yake kwa kulinda dhana ya soko na sio kujenga maduka ya kudumu ambayo yataiondosha dhana hiyo.

4. Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa atekeleze majukumu yake kwa mujibu wa sheria na kanuni za nchi. Vile vile, awashirikishe Wakuu wa Idara zake kwa yale mambo yanayowahusu.

5. Serikali ijenge soko kubwa ambalo litakidhi haja kwa wafanyabishara wetu.

6. Kwa kuwa Baraza la Manispaa linafunga mikataba na watu mbali mbali ni vyema likaandaa mikataba yenye hadhi ya kisheria. Pia, tunalishauri Baraza kuheshimu mikataba inayofunga ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima.

7. Kwa kuwa Baraza lina eneo maalum la wafanyabiashara kufanyia shughuli zao, kwa kuwa wafanyabiashara hao wanatozwa ada mbali mbali kuhusiana na biashara zao hizo. Kamati inalishauri Baraza kuwatafutia eneo mbadala wafanyabiashara wote wanaouza biashara zao pembezoni mwa barabara katika Soko la Mwanakwerekwe kwa lengo la kulinda hadhi ya Mji sambamba na kuepusha ajali zisizo za lazima.

8. Baraza la Manispaa liachane na tabia ya kuwatumia watendaji wake kwa zile kazi zinazotoa kwa mtu binafsi.

9. Mkurugenzi wa Baraza na watendaji wake wazijue kwa kina Sheria za nchi hususan zile wanazozifanyia kazi.

10. Ripoti hii ibakie katika Maktaba ya Afisi ya Baraza la Wawakilishi, ili iwe rahisi kwa kila mtumiaji wa maktaba hiyo kuipata kwa wepesi.

11. Watendaji wa Mamlaka ya Hifadhi na Uendeshaji Mji Mkongwe wanapotoa barua za taasisi yao waandike majina yao, ili ajulikane nani aliyesaini barua ile ingawa wanafanya kazi kwa niaba ya Mkurugenzi.

12. Sheria ya Baraza la Manispaa na Kanuni za Kudumu za Baraza hilo zifanyiwe mapitio ili ziendane na mazingira halisi. Miongoni mwa vifungu ambayo Kamati inahisi ni vyema vikafanyiwa marekebisho ni pamoja na kifungu cha 3(1) kinachotamka kwamba kutakuwa na jaduweli ya kwanza katika sheria hii litakaloonesha mipaka ya Manispaa, lakini jaduweli hilo halipo. Hivyo ni vyema jaduweli hilo likawepo, ili kuondosha utata wa mipaka.

    Vile vile Kamati inapendekeza kifungu cha 519(c) kifanyiwe marekebisho kwa kufuta neno *administration* na kupendekeza kisomeke *Law and Order Department*, ili kifungu hichi kiendane na jina la Kamati hii kama ilivyooneshwa katika kifungu cha 49(1) na (c). Hii ni kutokana na kuwa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Manispaa zilizosalia zimepewa majina kulingana na idara zake.

13. Kamati inaliomba Baraza hili tukufu liitake serikali iyatekeleze mapendekezo ya ripoti hii kwa vitendo ndani ya miezi mitatu kutoka tarehe ya kuwasilishwa kwa ripoti hii, yaani leo na hatimaye serikali iwasilishe taarifa ya utekelezaji wake mbele ya Baraza hili Tukufu. Lengo ni kuijenga nchi yetu na kuifanya izidi kuwa ni sehemu ya furaha kwa kila mtu anayeishi katika nchi hii. *(Makofi)*

SHUKRANI:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla Kamati inashukuru kumaliza kazi hii nzito kwa salama na kwamba serikali na kila aliyehusika atapata fursa ya kufahamu na hatimaye kufanywa marekebisho makubwa na ya kimsingi katika utendaji.

Kamati inaamini kwamba ripoti hii itaisaidia sana serikali katika utekelezaji bora wa majukumu yake, huku ikiheshimu haki na wajibu wa Baraza la Wawakilishi katika kuisimamia, kwa maana ile ile ya kuishauri, kuielekeza na hata kuikosoa kila penye haja ya kufanya hivyo. Jambo la msingi zaidi ni kuipongeza kila inapotokezea haja ya kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii ni elimu tosha na ufahamu uliofika kilele cha mafanikio kwa wananchi wote wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla pamoja na wasomaji wote wanaotumia muda wao vizuri kwa kujisomea taarifa mbali mbali, ili kupata elimu ya ufahamu na kuongeza maarifa.

Kwa kupitia ripoti hii mambo mbali mbali ambayo kwa muda mrefu ilikuwa ni kilio kwa wananchi kwa kukosa ufasaha wake au wamekuwa wakiyalalamikia kwa kuyajua kwa kiasi, basi watapata upeo wa kufahamu na uelewa mzuri kwa kuisoma ripoti hii.

Mhe. Mwenyekiti, kubwa zaidi baada ya maelezo hayo ni kwamba Kamati imetoa mapendekezo kadhaa kwa kila hadidu rejea. Kwa kweli tumefanya hivyo kwa lengo la kurahisisha ufahamu wa ufasaha, lakini kwa kuweka wepesi wa kutekelezwa kwake kama inavyostahiki kufanywa hivyo pamoja na kwamba tayari tumeshaeleza maoni na mapendekezo yetu mwisho wa kila hadidu rejea husika, kwa kuwa tunatakiwa kwa maelezo ya Kanuni ya 122 kifungu kidogo cha Kanuni ya Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2002 kutoa ripoti yetu na sehemu ya tatu ya hitimisho tutoe mapendekezo kwa Baraza hilo.

Mhe. Mwenyekiti, nakiri kama Wajumbe wote wa Kamati hii kwamba Kamati yetu imetekeleza majukumu yake katika mazingira mazito na magumu, kwani baadhi ya walioguswa ni wenzetu wa karibu na vipenzi vyetu. Lakini Kamati haikuwa na budi kulitekeleza jukumu hili la wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuwahakikishia Wajumbe wa Baraza lako tukufu pamoja na wananchi kwa jumla kuwa Kamati yangu imejitahidi kadri Mwenyezi Mungu alivyotuwezesha kuifanya kazi hii kwa uadilifu na uaminifu wa hali ya juu bila ya kumuonea au kumpendelea mtu. Hata hivyo, inawezekana ikawa kuna aina fulani ya mapungufu katika ripoti hii, hilo itakuwa ni bahati mbaya na wala halikufanywa kwa kukusudia na hasa ukizingaita kuwa Kamati hii ni ya wanaadamu.

Mhe. Mwenyekti, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani kwa Baraza letu Tukufu la Wawakilishi la Zanzibar, kwa kuona umuhimu na kupitisha Azimio la kuundwa kwa Kamati hii Teule. Vile vile, kwa moyo wa dhati kabisa nachukua fursa hii kumshukuru Mhe. Spika wa Baraza hili Mhe. Pandu Ameir Kificho kwa kutuamini na kutupatia heshima kubwa kwa kututeua kuwa Wajumbe wa Kamati hii. *(Makofi)*

Aidha, napenda kutoa shukrani za dhati kwa wale wote waliofika mbele ya Kamati hii na kutupatia taarifa mbali mbali kuhusiana na uchunguzi huu, akiwemo Mhe. Waziri, Wizara ya Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mstahiki Meya wa Manispaa ya Zanzibar, Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa, watendaji mbali mbali wa Baraza la Manispaa, wafanyabiashara mbali mbali, wateja au watu mbali mbali wanaotoa huduma katika Baraza la Manispaa na wengineo kwa kutupatia ushirikiano katika mahojiano na mashauriano wakati wa kipindi chote cha uchunguzi uliofanywa na Kamati hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa naomba nimalizie kwa kukushukuru tena Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii pamoja na kuwashukuru sana Wajumbe wenzangu wote kwa kunisikiliza kwa utulivu na umakini tokea jana tena kwa hali ya juu kabisa. Kwa hivyo, najua utulivu na umakini wenu unatokana na hamu ya kutaka kufahamu kuichangia ripoti hii.

Mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Ndugu Yahya Khamis Hamad kwa kuiwezesha Kamati hii kufanya kazi yake bila ya matatizo na wala usumbufu wowote na hatimaye leo tumeweza kukamilisha na kuiwasilisha ripoti hii kwenu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imeafikiwa na nilipaswa kuwahoji Wajumbe, lakini kila nikiangalia Wajumbe wenyewe humu ndani naona hatukidhi haja. Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria tuongoze, ili tuweze kujua nini tufanye katika hili.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni zetu zinasema kama hakuna *quorum* hatuwezi kuendelea na Baraza. Sasa kama *quorum* ipo basi tuendelee na kama haipo basi tuakhirishe, ili upige kengele kama Wajumbe watakuja na ikiwa hawapo itabidi tuakhirishe.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, ahsante. Waheshimiwa Wajumbe, mimi nafikiri tuliakhirishe Baraza letu kwa muda wa dakika tano, ili Wanadhimu wa Vyama watoke nje kuwahimiza Wajumbe ambao hawapo karibu yetu hapa, ili waje humu ndani na tuweze kuendelea na taratibu. Kwa hivyo, naomba kuakhirisha kwa muda wa dakika tano.

(Saa 5.20 asubuhi Baraza liliakhirishwa kwa muda kutokana na kukosekana quorum)

(Saa 5:25 asubuhi Baraza lilirudia)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kwa mujibu wa Kanuni zetu kifungu cha 122(3) (ii) inatuelekeza kwamba endapo hoja itatolewa ya kujadili taarifa ya Kamati Teule na majadiliano yatafanyika.

Sasa taarifa ya Kamati Teule tayari imeshawasilishwa na Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Kuchunguza Utendaji wa Baraza la Manispaa Zanzibar). Kwa hivyo, sasa ni wajibu wa Wajumbe kutoa hoja, ili tuweze kuikubali na tuendelee kujadili hoja hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, kuhusu utaratibu.

UTARATIBU

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba nitumie ukurasa huo wa 94 kifungu cha 3(ii), endapo hoja itatolewa na kujadiliwa Taarifa ya Kamati Teule na majadiliano kufanyika, hoja itatolewa kuhusu Azimio la kukubaliana na taarifa hiyo pamoja na marekebisho na kuchukua hatua kama inavyoamuliwa na Baraza. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja wanyanyue mikono, wanaokubaliana na hoja sijaona vizuri mikono yao.

Mhe. Hamza Hassan Juma, kuhusu utaratibu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mhe. Mwenyekiti wa Kamati Teule tayari ameshawasilisha hoja kwa ajili ya kujadiliwa, na halafu baadaye ndio tuhojiwe tunaoikubali, lakini hivi sasa tukisema tunaikubali basi hatutapata tena kuijadili. Kwa hivyo, kwanza tuijadili na halafu baadaye tukishamaliza atafanya majumuisho na Mhe. Mwenyekiti utatuuliza.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri uturuhusu tuendelee kuijadili hii hoja na wala tusitake kutafuta kushindana kwa Kanuni hapa na kupoteza muda, ahsante. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ahsante sana. Kwa hivyo, naomba tuendelee kuijadili hoja hii. *(Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kuweza kunipa nafasi asubuhi ya leo kwa ajili ya kuchangia kuhusu Ripoti ya Kamati Teule, hasa leo nataka niingie kwenye Katiba.

Mhe. Mwenyekiti, sisi Wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi tunapotoa hoja kuielekeza serikali, basi ni wajibu kwa serikali kufanya utekelezaji haraka ipasavyo. Lakini kinyume chake Mhe. Mwenyekiti, kwamba huwa zinakuja hoja nyingi na kuonekana kama sisi Baraza hatuna haki ya kumuwajibisha mtu wala hatuna haki ya kuleta hoja kwa ajili ya kuielekeza serikali kwa lengo la kufanya marekebisho.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia Katiba ukusara wa 33 kifungu cha 43(5) Mhe. Mwenyekiti naomba kunukuu kidogo.

Kifungu cha 43 (5) cha Katiba ya Zanzibar kinaeleza hivi:-

> "Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya mamlaka ya Rais ndio itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya Sera za Serikali kwa jumla na mawaziri chini ya uongozi wa Makamo wa Pili wa Rais, watawajibika kwa pamoja katika Baraza la Wawakilishi kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi". *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hapo sasa. Kwa kweli sisi hatupendi sana kufungua Katiba, lakini inapofika pahala hoja zinapokuja za shutma kwetu sisi watu wa *backbenchers* wa Baraza la Wawakilishi inatubidi tufungue Katiba kwa ajili ya kuzieleza kwani tunazijua. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, siku moja nilimuuliza swali hapa Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, jamani tukibaini mapungufu kwenye wizara zenu je mtakuwa mko tayari kujiuzulu. Kwa hivyo, nikajibiwa ala! Wakati jambo ni la kweli. Sasa tunasema tutawajibisha watu kwenye Baraza. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii imechukua siku nyingi sana na imetumia fedha za wavuja jasho kwa lengo la makusudi ya uzuri na kuweka hali halisi ya sera zetu, ambazo tunazozisema kila siku kwamba Serikali ya Umoja wa Kitaifa kuwa tunao utawala bora pamoja na mambo mengine. Lakini Mhe. Mwenyekiti, huu ndio utawala bora wenyewe inavyoonesha kwenye Kamati hii, kwa kweli inasikitisha sana.

Kuna mambo mengine Kamati Teule hawajayaona, lakini sisi tutawaonesha. Mhe. Mwenyekiti, ninao mkataba huu wa shilingi milioni 473,000,000/= huu hapa. Nani amesaini, tuangalie aliyesaini kwa upande wa mkodishaji (Manispaa) ni Mkurugenzi ndiye aliyesaini, hivyo ndivyo zinavyosema sheria na kanuni. *(Makofi)*

Halafu leo tunakuja hapa tunapingwa na mimi wakati mwengine ah! Mhe. Mwanasheria Mkuu hukwambia usiingizwe tu kwenye dimbwi tupo sisi *bush lawyers*, hii tayari *typical* kabisa ni kosa kubwa kwa mujibu wa kanuni zao za madiwani, kwa sababu Mkurugenzi amehusika zimefika fedha nyingi ni shilingi milioni 3,000,000/= na pasipo na budi ndio shilingi milioni 5,000,000/= ndio anaweza kusaini mkataba. Sasa leo *above* 473,000,000/= *millions*, ukiuliza hizi ziko wapi na zitaonekana kweli. *(Makofi)*

Mhe. Mwanasheria Mkuu ni mwalimu wangu mzuri sana. Kwa hivyo, tunapokuja kutoa hoja basi tunaona zitizamwe kwa umakini, kwa sababu sisi hatupendi ku-*provoke* tu hapa kiholela tunavyotaka aa! Kwa kweli sisi hatumuonei mtu.

Waheshimiwa Wajumbe, tutakumbuka juzi Mhe. Spika alivyotuasa na kutoa kauli ambayo ni nzito sana kwamba tumuogope Mwenyezi Mungu. Kwa kweli alisema au alitoa kauli ambayo ni nzito tena ni kubwa sana, na nyinyi hamkufahamu na mimi nimefahamu, kwa sababu ni mwanazuoni. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hivyo, nimeifahamu kauli ile na alisema kwamba sisi ndio wa kubeba majukumu mbele ya Mwenyezi Mungu, kwa sababu gani, tunao wananchi wenye haki ngumu tena ni masikni na wala hatutoi haki, hivi tutasema nini mbele ya Mwenyezi Mungu.

Mhe. Mwenyekiti, tunashikishwa Msahafu pale na tunasema mambo yote huku tukinyoosha mkono, na mimi ninaposhika Msahafu huwa natia udhu na sijui wengine kama wanatia udhu, maana niseme ukweli kama wengine tunafanya *joking is ok* hakuna tatizo, ndio maana mambo yanayotokea hayajulikani, wakati unashika Msahafu basi uhakikishe kila unalolifanya litendewe haki.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu leo na nimshukuru sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati Teule huyu ni *expert* mzuri pamoja na jopo lake lote la Kamati, na wameleta vitu *cream* kabisa, kwa sababu mimi huko nyuma nilivieleza kabla ya Kamati Teule. Mhe. Mwenyekiti, kama tunakumbuka vizuri tukatafute *hansard,* na nilieleza hapa na nikaonekana huyu Mshimba hana lolote, sasa leo tizameni *PhD* yangu. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa kwenye Kamati yetu ya Mawasiliano na Ujenzi sisi tulilitoa tamko hili pamoja na matatizo mengi yanayohusiana na watu wa *ZANTEL* pamoja na Manispaa. Kwa hivyo, utaratibu kwa mujibu wa Kanuni umetupa sisi tuwaite watu kuwahoji na kuwasikiliza.

Kwa kweli tulifanya kazi hiyo na tukaileta hapa pamoja na kueleza, nilieleza vizuri kwa sababu nilikuwa na *full documents*, lakini kuna mtu alikuja kuniibia humu *documents* zangu kama vile zilivyoibiwa za Manispaa, basi na zangu zimeibiwa humu na baadhi ninazo mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, tulimuita mama mmoja ambaye ni muhusika Afisa wa Mabango akifuatana na mzee ambaye alikuwa akikaimu Mkurugenzi kwa siku hiyo. Mhe. Mwenyekiti, walikubali moja kwa moja kwamba ni kweli mikataba hii nimesaini, lakini yametokea mambo mengine na yule mama alisema kwamba mimi napewa amri na Mkurugenzi. Lakini alikwenda kwa Mhe. Waziri na kusema ametukanwa matusi ya nguoni, Mhe. Mwenyekiti ilitusikitisha sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri alisema pale na kutoa mfano na huyo mama mwenyewe hapo angekuwepo juu basi tungesema tumuulize. Mhe. Mwenyekiti, Kamati haina utaratibu wa kumtukana mtu. Lakini je leo sasa Kamati Teule imemtukana mtu. Kwa kweli Kamati Teule hii imekwenda vile vile *step by step* kama tulivyokwenda sisi au nilivyoeleza mimi *issue* hapa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hatimaye nasema Baraza hili kwa mujibu wa Katiba hii basi mtu ajiondoe mapema kabla Wawakilishi wa *backbenchers* hawajatoa amri. Mhe. Mwenyekiti, kila siku tunaletewa hapa na Kamati Teule matatizo tu, mishahara haipandishwi na fedha kumbe zinaliwa na watu wengine. *(Makofi)*

Kwa mfano, huu hapa leo 473,000,000/= *millions* watu wangapi tumeshawalipa mishahara, huko Manispaa kila leo hakuna *overtime*, mishahara midogo na wanafanya kazi *over limit* na mishahara yenyewe wanayopewa ni midogo sana, hakuna *risk allowance*, kwa sababu wana-*risk* wanafanya kazi za hatari wana *risk*. Lakini kumbe *as a time* watu wanakwenda kula pesa wao. Halafu leo tuambiwe chombo hiki hakina haki kumuwajibisha mtu, watajizulu, kabisa. Hakuna masihara kitu hichi, sasa hivi tumekuwa wakali kutokana na kuchunga fedha za umma. Tunaletewa matatizo, tuaambiwa mara leo hospitali tunaambiwa *CT-Scan* imeharibika fedha hamna. Ndio pesa zenyewe hizi zinakushanywa kwa mzunguko mpaka zinafika huko serikalini.

Mheshimiwa kusema ukweli hali halisi mimi nasikitika sana. Mawaziri tusishindane na sisi wa *backbenchers* sisi wenzenu tunavipata hivi vitu, tusimlinde mtu. Kwa sababu ukimlinda mtu wewe tayari unajitia matatizoni. Lakini ukiwa *fare* na sisi na kama utafanya utaratibu ulivyo basi wewe Waziri utakuwa ni mzuri sana, huwezi kupata matatizo na *backbencher*.

Mheshimiwa habari iliyotoka katika kutafuta watu Bustani ile pale, mataa line zile ambazo Zantel, sasa hivi ni Zanzibar ni mdau wetu mkubwa sana. Lakini zile laini ambazo yeye ameziomba mapema hakuweza kupewa kwa sababu mwekezaji pengine walikuwa ana dau lake dogo. Wametokea watu wenye dau kubwa wamepewa nafasi ile kinyume na utaratibu, mikataba ndani ya mikataba. Leo Manispaa imepelekwa Mahakamani, tunakwenda wapi. Kila siku itakuwa serikali zetu zinapelekwa mahakamani tu. Mhe. Mwenyekiti, hili suala linanisikitisha sana.

Lakini twende kwenye sheria. Manispali ina kamati zake zinazohusika zikiwa chini ya msimamizi Meya Mstahiki, lakini kila mikataba mimi sioni saini za Mhe. Meya haimo humu. Mhe. Meya anataka kuleta maendeleo katika nchi hii, lakini utizame atakwenda wapi, wakati mtendaji Mkuu wake yeye hawaelewani, kila mtu anakwenda njia anayotaka kwenda yeye. Yupo tu Mhe. Meya hana hata kimoja alichokifanya kuanzia sasa hivi, ataanzia wapi.

Tulisema si chini ya mara ya kwanza au mara mbili, jamani ee kwa maslahi ya wananchi tumuondoweni mapema kwa, lakini nimshukuru na yeye kafanya njia ya kisasa. Katika sheria ambayo itam-*keep out automatically* kabisa, sasa yuko nje ninavyosikia, sisi tufanye nini. Ama kweli watu wa sayansi, watu anasoma kwa sababu kuna kitu

ambacho ukikifanya *automatically* kinakutengua, lakini *time late* kinajiengua kipindi ambacho ngoma ipo mezani hapa kwa Mhe. Mwenyekiti.

Kamati Teule imesema pamoja na hayo yote tuliyokuwa tunayo aliyokuwa nayo, basi mimi naomba si vibaya Mhe. Waziri akasema jamani najiondoa kwa kuweka heshma yangu kama Waziri mwenzake mmoja hapa Mhe. Hamad Masoud alijiondoa kwa heshima na taadhima akasema mimi jamani kutokana na hali najiondoa. Jamani si vibaya tena ni *international* kabisa, halafu isitoshe unapata *privilege* kubwa. Mhe. Hamad Masoud amepanda daraja sasa hivi kajiondoa kwa heshima yake kawa Naibu Katibu Mkuu.

Naamini na wewe waziri ukijiondoa kwa heshima hii basi mimi naamini kabisa Mwenyezi Mungu hakutupi, atakuweka na wewe mahali pazuri tu. Mimi naamini kwamba hukufanya wewe lakini kwa heshima yako na hali halisi kila siku Baraza hili linasemwa tu kila siku. Basi ningeliomba sana Mheshimiwa wangu na wewe ungesema aaaaah. Usinipishe miye si lazima lakini ungesema tu kwa heshima na taadhima mimi najiondoa ili niwaachie nafasi, Mhe. Dokta Sheni atafute mwengine atakayeweza kuleta ufanisi zaidi. Mheshimiwa mtu kugonga akili imo, leo tumeona hapa Mtu jimbo la Rahaleo anapewa Kwahani, akili kuchoka imo, *over age* hiyo. Akili zinachoka lakini niangalie akili yangu miye na Dokta Mwinyi ndio sawa sawa, yeye bado *steel* naweza kufanya kazi. Kwa sababu muda ninao na bado naweza.

Kwa hiyo mimi naona hoja hizi zinazoletwa tuzithamini kutokana na fedha za mchango wa wavuja jasho zinatolewa ili kutafuta maovu yanayofanyika. Mhe. Spika, mimi sitokuwa na mengi sana kwa sababu wenzangu wananambia niwaachie. Mimi nimeanza kama ni burdoza ili kuweza kuwawekea wenzangu njia ili wapate zaidi kuchangia. Mheshimiwa huu hapa ninao mkataba, watu wakitaka kuuona mimi kwa fursa yako niko tayari kuutoa.

Mhe. Mwanasheria akitaka kuuona auone na kifungu hichi Mwanasheria anakijua kukisoma, lakini binaadamu kughafilika imo. Mimi sitaki kumsema mwalimu wangu, kwa sababu mwalimu wangu nampenda sana msikivu. Kwa hayo machache Mheshimiwa mimi nasema uwajibishwaji ni muhimu sana tunaomba wawajibishwe watu kwa haraka sana. Naiunga mkono hoja ya kamati hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, nami nitumie fursa hii kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii angalau na mimi nichangie kwa kusema angalau mawili matatu juu ya ripoti hii iliyowasilishwa punde na Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda niipongeze sana Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi inayoongozwa na Dokta Salmin Awadh Salmin. Kwa kweli Kamati hii imefanya kazi kubwa, imefanya kazi kwa umakini wa hali ya juu. Hatimae leo imeweza kutuletea ripoti ambayo tunasema kwamba imekamilika katika viwango. Kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu niipongeze kwa dhati kabisa Kamati hii na pongezi maalum ziende kwa Mwenyekiti aliyeiongoza Kamati hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa muda mwingi tumekuwa tukisikia hasa kwa watendaji wa serikali wakizungumza katika wakati tofauti, kwamba tatizo letu Zanzibar tuna kitu kinachoitwa muhali. Hatufanyi maamuzi, hatupitishi maamuzi kwa sababu ya muhali. Sababu hiyo imekuja kutokana na jiografia na hali ya Zanzibar takriban huzunguuki mara mbili unamkuta kwamba aliyefanya tokeo ni mtu wa karibu, ni jamaa, ni swahiba au vyenginevyo vyovyote. Sasa mara nyingi viongozi wa serikali hutwambia kwamba muhali, muhali, muhali. Sababu hiyo inatumika kama ni sababu ya kutokuchukua maamuzi. Maana serikali wakati mwengine hutumia sababu hiyo kama ndio sababu inayofanya watendaji wasichukuliwe maamuzi kutokana na muhali.

Mhe. Mwenyekiti, sisi wawakilishi ni sehemu ya Wazanzibari. Sisi hatukutolewa pahala pengine popote tumetoka miongoni mwa Wazanzibari, miongoni mwa wananchi. Lakini Mwenyekiti, wewe umekuwa ni shahidi namna ambavyo sisi Wawakilishi kupitia Tume zetu tumekuwa tukitekeleza majukumu yetu pasi na kuona muhali.

Sisi kama ni sehemu ya Wazanzibari kwa kweli tungelikuwa tuna kila sababu. Kazi unazotutuma Mhe. Spika, kuzifanyia muhali, kwa sababu ni hawa hawa ambao ndio ndugu zetu, ni hawa hawa ambao ndio jamaa zetu, ni hawa hawa ambao ndio rafiki zetu wanaoguswa na mambo kamka haya. Lakini hii ni ripoti ya pili inayokuja na inathibitisha na inadhihirisha kwamba tunapotumwa kufanya kazi tunatekeleza wajibu wetu inavyopaswa. Kwa hivyo kama ni suala la kupewa pongezi wawakilishi katika shughuli hizi tunapaswa tupewe pongezi za kina.

Kwa sababu hii nayo kwa upande mwengine ni changamoto hata kwa serikali. Inapaswa nayo isichukulie muhali kuwa ndio sababu ya kutokuwajibika kwao. Lazima wawajibike kwa sababu shughuli hizi ni za umma ni shughuli za wananchi na wananchi wanachohitaji ni utumishi uliotukuka. Serikali haipaswi kutumia kigezo hichi cha uswahiba au mambo haya ya muhali kuwa ndio sababu inayoifanya serikali isitekeleze wajibu wake.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii iliyowasilishwa na Mhe. Salmini Mwenyekiti, ni ripoti ya pili katika kipindi hichi nadhani cha miaka 10. Jana tulishuhudia Mhe. Waziri wa Nchi, akilieleza Baraza hili namna serikali ilivyochukua hatua kwa ripoti ya Kamati Teule iliyopita. Ukweli ni kwamba mimi binafsi pamoja na wenzangu tulifadhaishwa mno. Kwa kweli tuseme kwamba hatukufikia pahala ni sawa sawa na kucheza mpira timu pinzani ikatia mpira kwapani ikaondoka nao.

Maana jana ilionekana kwamba Wawakilishi hatukuikubali ripoti ile ya utekelezaji, hatujui kama ripoti ile serikali wameondoa au hawakuiondoa, hatujui. Ilituwacha kwa lugha ya mjini ilituacha kwenye mataa. Lakini tunachukulia ile kauli iliyotolewa na Waziri kwamba hoja ile inaondoshwa lakini serikali itazungumza na Kamati Teule kuangalia namna ya utekelezaji. Kama hivyo ndivyo si vibaya, serikali ikitaka msaada wa kutekeleza ripoti ile sisi kama Kamati tuko tayari. Chamsingi ni kwamba tunataka, kwa sababu mtendaji Mkuu wa shughuli za serikali yupo ambaye ni Makamo wa Pili wa Rais, tunataka serikali isituache tunaelea itwambie ni lini itakutana na wajumbe wale wa Kamati Teule kwa ajili ya kuifanyia mapitio ripoti ile.

Vile vile tulipendekeza kwa sababu tunaingia katika utekelezaji, tulipendekeza ikiwezekana pendekezo hili na wenye viti wa Kamati nyengine waingie kuongezea nguvu kamati ile teule ili tukae pamoja na serikali tuone namna gani tunatekeleza. Tunasema kwamba tutafanya yote haya kwa maslahi ya nchi yetu na kwa uwajibika uliotukuka wa serikali yetu.

Mhe. Mwenyekiti, hilo naliwacha kwako naliacha kwa serikali tuone namna gani tutashirikiana. La kama mambo yatakwenda hivi hivi hii itakuwa ni ngoma ya kichawi, siku zote tutakapokuja katika Baraza hili tutakumbusha utekelezaji wa ripoti ile, niondoke hapo.

Mhe. Mwenyeki, ripoti hii katika azimio lake au pendekezo lake la kumi na tatu na la mwisho imesema naomba Mheshimiwa uniruhusu ninukuu.

> “Kamati inaliomba Baraza hili tukufu liitake serikali iyatekeleze mapendekezo ya ripoti hii kwa vitendo ndani ya miezi mitatu, kutoka tarehe ya kuwasilishwa kwa ripoti hii ambayo ndiyo leo, hatimaye serikali iwasilishe taarifa ya utekelezaji wake mbele ya Baraza hili tukufu. Lengo ni kuijenga nchi yetu na kuifanya izidi kuwa ni sehemu ya furaha kwa kila mtu anayeishi katika nchi hii.”

Mhe. Mwenyekiti, pendekezo hili la kumi na tatu limeitaka serikali itekeleze na hapa kidogo kuna mgogoro kuitaka serikali itekeleze, nahisi nayo italeta mgogoro. Maana tuliambiwa serikali haina mamlaka ya kuitaka serikali wala ya kuilazimisha serikali. Lakini kwa sheria zote, kwa katiba zote kama alivyosema pale Dokta Mshimba na kama alivyosema jana Mhe. Salmin kwamba Katiba inaipa mamlaka chombo hichi kwamba serikali itawajibika mbele ya chombo hichi. Lakini vile vile chombo hichi ndio chenye mamlaka ya kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nikumbushe isije tena baadae ikaleta mgogoro mwengine kwamba tunapojadili mambo haya maana yake tunajadili Baraza zima ikiwa ni sehemu ambayo ina mawaziri. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi tuna fursa pana ya kujadili mambo haya, kwa yule anayeunga mkono aunge mkono, kwa yule anayetaka marekebisho atake marekebisho, kwa yule anayetaka ufafanuzi atake ufafanuzi ndani ya Baraza hili. Tutakwenda hadi mwisho tutakapomaliza suala hili maana yake sasa yatakuja maamuzi. Isijekuwa kipindi hichi ni kipindi kwetu *back bencher* tu tuchangie serikali wao wakanyamaza kimya. Kwamba wao wana nafasi nyengine kwamba serikali kwenda kujadili. Tunasema taratibu haziruhusu hivyo.

Chombo hichi pamoja na Mawaziri, pamoja na serikali ndio chenye mamlaka sasa hivi kufanya kazi hiyo. Tufanye kwa pamoja na hata yule ambaye ana mawazo mbadala ndio mahala pake hapa aseme. Kama kuna mtu ana marekebisho serikali iseme hapa. Kama kuna wasi wasi wowote hapa ndio mahala pake. Tutakapomaliza tukafika mwisho mweyekiti ukatoa *ruling* yako sasa kwamba tumeipokea na tukasema sote kwa pamoja, pamoja na serikali kwamba tumepokea na tukasema sote kwa pamoja kwamba twende tukafanye kazi maana yake kutakuwa hakuna *rule* tena kwa serikali kwamba inakwenda kujadili.

Naomba hilo lifahamike kwamba katika mjadala huu tuna nafasi sote, Wawakilishi *backbencher* pamoja na serikali sote kwa pamoja. Kama kuna mamna yoyote turekebishe na kama kuna chochote kile ili tukiamua maana yake itakuwa ni Baraza zima sasa tumeamua. Tutamtoa Raisi tu kwamba yeye ni sehemu ya Baraza lakini kwa upande wake. Yeye sehemu yake kubwa ni katika kusaini Miswada na mambo mengine. Kwa hivyo litakalotoka hapa ni maamuzi halali kwa mujibu wa katiba na sheria zetu.

Mhe. Mwenyekiti, yaliyoonekana katika uchunguzi katika Manispaa *naasaf* kusema kwamba sura hii iliyoonekana Manispaa inatoa sura halisi ya utendaji katika tasisi zetu za umma. Takriban Kamati ilifanya kazi Manispaa, kamati iliyopita ilifanya kazi katika taasisi nyengine. Nathubutu kusema kwamba utendaji katika sekta yoyote ya umma takriban katika taasisi nyingi za umma utendaji uko hivi. Utendaji wetu unatoa huduma mbovu kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, katika taasisi nyingi za umma kuna matumizi mabaya na yaliyokithiri kama ilivyoonekana katika ripoti. Mhe. Mwenyekiti, ni yumkin kwamba vitendo vyote hivyo chimbuko lake na msingi wake ni rushwa iliyokithiri katika taasisi nyingi. Maana leo ikiwa sheria inasema fanya hivi, kanuni zinasema fanya hivi. Wewe kama mtendaji ukaamua kufanya vyako, nani kakuagiza kufanya hivyo na ulifanya kwa maslahi gani. Kufuata sheria hakuna gharama yoyote. Lakini watendaji wanakiuka kwa makusudi sheria.

Mimi nikiwa kama Mwenyekiti wa Kuchunguza Mahesabu ya Serikali nayaona mambo haya. Watendaji wetu hukiuka kwa makusudi sheria kwa sababu ya mambo fulani fulani ambayo kwao wao ni faida. Leo tumezungumzia Baraza la Manispaa lakini takriban sehemu nyingi za umma ziko hivyo. Katika hili Mwenyekiti, kwa kweli katika hizi taasisi, hizi serikali za mitaa ndiko matatio yanakuwa ni makubwa zaidi katika serikali zote za mitaa. Kwa maana ya Manispaa, Halmashauri pamoja na Mabaraza ya Miji tuliyonayo. Sura ni hii hii na mambo ni haya haya. Jukumu hili tumeliona na serikali nayo imeliona.

Mhe. Mwenyekiti, serikali takriban zaidi ya miaka saba sasa kaji nchi chenyewe ndio hiki, miaka saba kunakuwa tu kuna utafiti, kuna kuwa watu kwenda mbili kwa ajili ya kufanya mageuzi katika Serikali ya Mitaa, mimi nadhani hata ingelikuwa ni kama Tanzania Baraza na sehemu nyengine utafiti huo ungekwisha maliza. Mimi nathubutu kusema kwamba mambo yanacheleweshwa hivi kwa makusudi ili wakubwa waendelee kuzitumia halmashauri kama ni sehemu ya kujipatia kwao mapato.

Mhe. Mwenyekiti, tumeshuhudia na baadhi ya mawaziri wanazitumia sehemu hizo katika kuchota mapato. Suala hili halifikii kila siku tukizungumza leteni sera, leteni sera inakuwa ni tatizo na ni shughuli ambayo haina mwisho. Matokeo yake sasa ndio haya ambayo yameonekana. Wananchi wetu wanategemea huduma takriban kila siku kunyonywa kutokana na makodi haya ya manispaa, wananchi wakitaraji kupata huduma zilizobora na miji iliyosafi, lakini kumbe vile ni kinyume chake. Matokeo yake huduma katika miji yetu zinakuwa ni mbovu na hazitamaniki.

Hili nalo ni tatizo ambalo takriban linachangiwa na serikali, kwamba hawataki kuleta mageuzi ya kuleta sera hizi, hawataki kuleta sheria hizi ili tufike pahala kuwa na vyombo. Mwenyekiti, lazima tukubali kwamba hatuwezi tukaendelea na nchi yetu na nchi yetu haiwezi kupita hatua kama ikiwa hatujazipa nguvu Serikali hizi za Mitaa. Takriban nchi nyingi duniani unapokwenda Serikali hizi za Mitaa ndio zenye mamlaka na ndio zinazosababisha maendeleo katika nchi yeyote ile.

Unapokwenda katika nchi za watu ukaambiwa mambo haya yote yaliyomo hii ni Manispaa ndio iliyothubutu kufanya mambo kama haya. Huwezi ukaamini utadhani kama ni Serikali Kuu yenyewe, kumbe ni Manispaa. Lakini Manispaa kwa kuwa na watu na watendaji ambao wana uwezo wa kutumia rasilimali zao ndio hupelekea baadhi ya nchi hizo kuwa na mambo kamka hayo.

Mhe. Mwenyekiti, tunasema kwamba kadiri serikali inavyochelewa ndivyo kadiri na miji yetu nayo na nchi yetu kwa ujumla inavyoingia katika matatizo na inavyodumaa katika maendeleo. Leo ukiuliza Mji wa Unguja hasa ni upi? Mji wa Unguja maana unaposema au unapouliza jamani leo nimekuja Unguja nataka kwenda *down town* ni wapi? Ukenda katika miji huko unaambiwa jamani twende *down town* na ukifika kweli unaona *down town*. Leo ukiambiwa *down town* ni wapi hapa kwetu ni pale katikati ya kitovu cha mji maana yake kuna masoko na harufu mbaya ya majaa, harufu mbaya tupu.
Mimi leo asubuhi niliulizwa swali hivi huu Mji Mkongwe ndio sehemu ambazo za watalii au ni kitu gani. Kumbe vile kinachowavutia watalii ni kuja kuangalia majumba mabovu, kwao hakuna majumba mabovu kwa hiyo wao

wanaona ni ajabu. Hicho ndicho tunachojivunia na ndio tunachoringia. Kwa hivyo Mwenyekiti, tunasema kwamba serikali kwa vyovyote katika hili wawe na mkono.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii imejaa kama tulivyoona kutokea habibu ya kwanza hadi hadidu ya mwisho imethibitishwa na katika kila hadidu utakayoipitia utaona kwamba imemgusa ukurugenzi kwamba Mkurugenzi hapa kakiuka hichi, Mkurugenzi hapa kafanya hichi, Mkurugenzi hapa kafanya hichi pamoja na watendaji wake, kila hadidu inaeleza hivyo.

Nadhani hili kwa kweli lazima sasa tufike pahala tuende mbele zaidi. Kama alivyosema Mhe. Mshimba kwamba Mkurugenzi amejiondoa mwenyewe, hajajiondoa bado yupo. Lakini ripoti imependekeza kwamba achukuliwe hatua za kisheria. Lakini Mhe. Mwanasheria Mkuu jana pale kazungumza kwamba unapomwambia mtu achukuliwe hatua za kisheria maana yake unaruhusu sasa mamlaka nyengine ziweze kumchunguza na zitakapofika mahala kumuona kwamba hana hatia basi anaachiliwa. Ndio alivyozungumza jana Mwanasheria Mkuu, kama vile ripoti jana tulivyoisoma hapa ya serikali.

Sasa mimi katika hili nadhani kwamba ripoti ya madiwani ilikuja hapa tukaijadili kidogo tukasema kwamba ile ripoti tuiweke kando, Baraza twende na ripoti yetu. Ripoti yetu nayo imebaini yale yale takriban yaliyokuwemo katika Baraza. Kwa hivyo kwa hili Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono kwamba Mkurugenzi achukuliwe hatua za kisheria lakini zisizoruhusu. Maana kama ni uchunguzi tayari uchunguzi wenzetu wameshaufanya, sasa ukisema waziruhusu tena mamlaka nyengine hivyo sisi mnatwambia kwamba tulikwenda tukapoteza muda tu. Yote haya yaliyokuwemo humu kwamba hawa hawana akili. Sasa ikiwa wao hawaamini na sisi pia hatuamini hayo yao wao vile vile. (*Makofi*)

Inakuja kuwa ni ajabu leo tumeshachunguza, tunaushahidi wa *documents*, tuna ushahidi wa kanda, tuna ushahidi wa kila kitu, unasema kwamba kuna taasisi nyengine. Ikiwa haiaminiki sisi pamoja na kwamba hatukusoma lakini tuna akili na tuna uwezo wa kufanya kazi. Ile kusema kwangu kwamba tuna upungufu wa kibinaadamu, mtu yeyote makini lazima atasema. Nani kwani aliyekamilika? Maana yake kusema kwangu kule sasa ichukuliwe ndio udhaifu kwamba ripoti ile ipitiwe tena upya, hatukuwa na maana hiyo. Hakuna mtu hata mmoja atakayekwenda kusimama kwenye kiriri akasema kwamba yeye *perfect* hakuna. Aliyekamilika katika ulimwengu huu ni mmoja tu. (*Makofi*)
Kwa hivyo isichukuliwe kuwa sasa ni hoja ya kuhalalisha na kukichakachua kile tulichokifanya. Nilisema vile kama ndio muungwana yeyote analazimika kusema hivyo. Kwa hivyo Mwenyekiti, tunasema kwamba hatua zichukuliwe kwa Mkurugenzi na kwa mwengine yeyote si Mkurugenzi peke yake na mwengine yeyote aliyehusika na haya. Tena hatua isionekane kwamba ni kumuhamisha hapo kumpeleka kwengine. Maana huo ndio unakuwa utaratibu, anaeondoshwa leo kwenye sehemu hii, kaa miezi miwili mitatu au mine utasikia tayari keshatafutiwa fupa jengine keshakwenda kung'ong'ona. Maana anaondolewa padogo anapelekwa pakubwa, hiyo ndio staili inayoonekana.

Tunataka mtu yeyote atakayechukuliwa hatua hii kama ni Wawakilishi tunasema haiwezekani kumuondosha mtu halafu aka–*relax* keshachukua mabilioni ya shilingi leo aende aka–*relax* na mimi si nitaiba tu. Nitaiba hapa bilioni mbili halafu si nitafukuzwa tu. Kwani nikifukuzwa mimi hasara yangu nini tena katika ulimwengu huu, hapana.

Ripoti hii mimi nasema ingelikwenda kufanya tathmini kwa kila eneo, kwa kile kitendo kilichofanywa kimeleta athari gani pale au ni kiasi gani cha fedha kimepotea. Ili tumtake aliyechukua arejeshe mali serikalini. Kama ni fedha azilipe kana hana kasha zila zichukuliwe rasilimali zake ziuzwe ili pesa zinazopatikana zirejeshwe serikalini. Nadhani tukifanya hivyo angalau tukifanya hivyo tunaweza tukafika pahala tunaweza tukasema kwamba hivi vitendo vinaweza vikamalizika.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti imeandikika, ripoti imeeleza mambo kwa kina, ripoti ina mapendekezo. Niseme tu kwamba naunga mkono ripoti yote hii na naunga mkono mapendekezo yote yaliyotolewa. Lakini kwa sababu katika maelezo yangu Mhe. Mwenyekiti nilieleza kwamba inaonekana nayo serikali inalazalaza huu mchakato wa kuelekea kwenye mageuzi kamili ya serikali zetu za mitaa kwa makusudi kabisa.

Kwa hiyo naomba ikiwezekana nipendekeze kwamba katika ripoti hii kuwe na pendekezo jengine la kuitaka serikali ihakikishe mwakani tukijaaliwa mwezi wa April tuwe na sheria kamili inayohusiana na suala zima la Serikali za Mitaa. Lazima tufike pahala tujiwekee kikomo, hatuwezi tukenda tu hivi hivi, haiwezekani. Lazima tuwe na malengo kwamba jambo hili tunalichukua hapa mpaka hapa ikifika inakuwa ni mwisho. Hatuwezi tu, tukawacha watendaji maanaake ikawa jambo hili halimalizi.

Kwa hivyo napendekeza Mhe. Mwenyekiti, ikiwezekana tutie katika pendekezo kwa sababu kadhia hii ya Manispaa kama nilivyosema inahusu takriban serikali zote za mitaa. Na kwa kuwa serikali katika masuala haya yanayotokea yanatokana na kwamba serikali haitaki kuharakisha mchakato huu wa kuzifanyia mageuzi serikali za mitaa.

Kwa sababu hiyo naomba nishauri kwamba na hili nalo liingizwe katika mapendekezo kwamba serikali ipewe muda maalum wa kuhakikisha kwamba inakamilisha sera, inakamilisha sheria ndani ya kipindi tutakachokubaliana. Mhe. Mwenyekiti narudia kuipongeza Kamati, na ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuunga mkono hoja, naunga mkono hoja, naunga mkono mapendekezo. Ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti na mimi nataka nikushukuru na mimi kuweza kunipa nafasi hii na mimi nikatia nyama ripoti hii ya Kamati Teule ya kusimamia au kuchunguza mwenendo wa Baraza la Manispaa iliyowasilishwa na Mheshimiwa makini kabisa Mwenyekiti wetu Salmin Awadh Salmin.

Mhe. Mwenyekiti na mimi kama walivyoanza wenzangu nataka nimpongeze sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati hii pamoja na Wajumbe wake, wamefanya kazi kwa umakini, kwa uadilifu mkubwa, na bila ya kuwa na hata ya chembe ya muhali. Mhe. Mwenyekiti tunashukuru Kamati zetu za Baraza la Wawakilishi zimeanza kuondokana kufanyakazi kwa mazoea. Sasa hivi tunafanya kazi kama matakwa ya Katiba na sheria za nchi pamoja na wananchi wanavyotaka.

Mhe. Mwenyekiti mimi nataka nianzie pale alipomalizia Mheshimiwa mwenzangu Omar Ali Shehe, lakini pia katika mchango wangu nitakazia na yale maeneo aliyoyagusia mwanazuoni wetu wa Baraza Mhe. Makame Mshimba ambaye yeye amejitangaza leo kuwa ni mwanazuoni, sasa wanazuoni wasije wakahamaki huko, kuna CV za hapa Barazani, kwa hapa Barazani Mhe. Makame Mshimba ni mwanazuoni wa Baraza.

Mhe. Mwenyekiti nikimalizia dibaji yangu hiyo, nataka nije moja kwa moja katika michangio. Mhe. Mwenyekiti kutokana na ripoti hii tumegundua kuna udhaifu mkubwa sana uliofanyika katika Baraza la Manispaa. Lakini Mhe. Mwenyekiti mimi nataka niseme kwamba tusilaumu tulipoangukia, tulaumu tulipojikwaa. Kwa nini nikasema hivyo, Mhe. Mwenyekiti, uhuru waliokuwa nao Wakurugenzi wetu katika halmashauri mbali mbali pamoja na baadhi ya makatibu wa halmashauri mbali mbali ndio uliofikia pahala kama hapa.

Mhe. Mwenyekiti ilikuwa si busara sana, hii ilikuwa kazi ya madiwani waifanye wenyewe kwa sababu madiwani wenyewe ni wanasiasa kama sisi, wana chombo kama chetu sisi ambacho walichochaguliwa na wananchi. Lakini kwa kuwa sisi tunakosoa tulipoangukia hatukosoi tulipojikwaa ndio maana ikawa yanafikia haya. Kwa nini nikasema hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni za Baraza la Manispaa ambazo Mhe. Mwenyekiti alivitaja vifungu mbali mbali. Mkurugenzi hawezi kufanya maamuzi yoyote makubwa bila ya kupata baraka ya Baraza la Manispaa. Ambalo Baraza la Manispaa lina mtu mkubwa sana katika nchi ingawa hapa kwetu bado ile hadhi yake hatuichukulii kama inavyotakiwa. Meya ni mtu mkubwa sana katika nchi, wanapokuja viongozi wote wa kitaifa ambao Mhe. Rais anakuwa ni wageni wake basi Mstahiki Meya anatakiwa lazima na yeye awepo, ni mtu mkubwa sana. Lakini leo kitu cha kushangaa tunaambiwa kuna mambo mengi yanafanyika hata wenyeviti, hata hao madiwani hawana taarifa. Huu ni udhalilishaji mkubwa wa wanasiasa wenzetu madiwani akiwemo Mhe. Meya.

Sasa hii inatokana na nini, sheria tulizokuwa nazo sasa mimi nadhani ndio maana nikasema nitaanza kukazia alipomalizia Mwenyekiti mwenzangu aliyemalizia hapa, Mhe. Omar Ali Shehe, ninafikiri sasa wakati umefika kutengeneza *local government reform*. Tufanye marekebisho ya Serikali za Mitaa ili madiwani waweze kufanya kazi zao na kuweza kuzisimamia halmashauri pamoja na manispaa ili kuweza kutekeleza majukumu yao kisheria. Lakini vile vile mabaraza ya manispaa pamoja na halmashauri waweze kuwa na fursa ya kuweza kutafuta njia nyingi au vianzio vingi vya uchumi au mikataba mbali mbali ili kuweza kufanikisha mambo yao. Lakini katika hali kama hii mimi ninafikiri tutakuwa tunampigia mbuzi gitaa.

Sasa mimi ninatoa wito kwa madiwani wote ambao madiwani wengine ndio wanachaguliwa, aidha wanakuwa Mameya au Wenyeviti wa halmashauri. Mimi nadhani wafanye kazi yao vizuri waweze kuwasimamia watendaji wa serikali waliokabidhiwa, yaani makatibu wa halmashauri pamoja na wakurugenzi wa mabaraza ya miji au manispaa ili kuweza wasirejee tena utumbo kama huu ambao uliofanyika.

Mhe. Mwenyekiti mimi nataka niseme kwamba naamini madiwani wetu ni watu makini wakiweza kujitambua hasa baada ya kupita ripoti hii basi hawatoweza tena kumuachia Mkurugenzi wa aina yoyote au Katibu wa Halmashauri ya aina yoyote kuweza kujifanyia mambo anavyotaka yeye. Mhe. Mwenyekiti kwa kweli kitu ambacho cha kusikitisha hasa kwa wafanyabiashara ambao waliokuwa wanashiriki katika biashara wameamua kujiajiri wenyewe bila kwenda kuing'ang'amua serikali kuomba ajira, matokezeo yake tukawa tunawaondoa bila ya kuwatafutia utaratibu mwengine wa kuweza kuishi.

Mimi nadhani hili lilikuwa sio haki sasa kwa kuwa wenyewe wanatusikia, mimi nadhani wale walioathirika katika mchakato huu wote katika kadhia yote hii, basi angalau wangelijaribu kuangaliwa aidha kupatiwa maeneo ya kupatiwa zile kazi zao aweze kufidiwa kwa njia nyengine yoyote.

Mhe. Mwenyekiti katika ripoti hii imejaribu kuelezwa maeneo mbali mbali, maeneo ya Darajani, maeneo ya kwenye masoko, maeneo ya *diplomatic super market*, kwa hivyo kuna maeneo mengi ambayo yamejaribu kuzungumziwa. Lakini kimsingi ukija ukiangalia *conclusion* ya maeneo yote hayo, yote yanakuwa watendaji waliohusika akiwemo Mkurugenzi waweze kuwajibika. Kwa hivyo mimi na hili sina pingamizi na ninaamini Wajumbe wenzangu watakubaliana na hili. Kwa sababu kama tukishindwa kusimamia uwajibikaji tutakuwa siku zote tunakuja kupiga kelele tu hapa itakuwa sawasawa na kumpigia mbuzi gitaa.

Kwa hivyo mimi nadhani kama walivyosema wenzangu hatua za kisheria kuchukuliwa, hata hizi tunazochukua sasa hivi hizi pia ni hatua za kisheria kwa sababu haya tunayoyafanya yote yamo ndani ya kanuni zetu na sheria zetu. Kwa hivyo haya maamuzi yanayofanyika hapa vile vile ni halali.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwamba jambo ambalo nililoliona katika ripoti hii inaonesha katika utendaji wa Baraza la Manispaa hakuna maelewano ya kutosha baina ya Mkurugenzi pamoja na Madiwani. Lakini vile vile pamoja na Mkurugenzi na Waziri. Sasa hili nitaligusia la Mkurugenzi na Waziri. Mhe. Mwenyekiti sio Mkurugenzi huyu tu Mheshimiwa Wakurugenzi wengi, Mawaziri hasemi tu lakini sisi tunajua hawawatii maelekezo yao.

Mhe. Mwenyekiti kuna baadhi ya Wakurugenzi wengine wanasema aa hao bwana nguvu yao iko Barazani sio nguvu yao iko huku kwa sababu wanajua hata wakifanya utumbo wa aina gani hakuna hatua yoyote ambayo wanachukuliwa. Mhe. Mwenyekiti na hili linatokana na nini, na ndio maana nikasema kwamba tusiangalie tunapoangukia tuangalie tunapojikwaa. Mimi nadhani sasa hivi tuko katika mchakato wa Katiba mpya na kama baadhi ya wenzangu wanavyosema kwamba Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ita-*effect* na Katiba ya Zanzibar. Nadhani wakati umefika kumpunguzia Mhe. Rais majukumu, maana yake wananchi wetu hasa wa Zanzibar ukisema kumpunguzia madaraka watasema oo hampendi Rais, kumpunguzia majukumu.

Mheshimiwa tatizo la watendaji wetu na huu mgongano unovutana na kuwa Wakurugenzi wanashindwa kuwaheshimu Mawaziri kwa sababu kila mmoja anajua kateuliwa na Rais, kila mtu kateuliwa na Rais kila mmoja anamtambia mwenzake maneno ya wanawake wanarushana roho, hatuwezi tukafika. Sasa mimi nadhani ifike pahala wenzetu Bara wameshaanza kuzungumza kupunguziwa Rais madaraka, mimi nadhani sasa hivi ifike pahala Rais kuna baadhi ya maeneo awe huru kuteua. Kuna baadhi ya maeneo Rais katika uteuzi wake lazima yapate baraka za taasisi nyengine hapo ndio uwajibikaji ndipo utakapokuwepo.

Mhe. Mwenyekiti, hili mfano kama kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano tunaposema kwamba Rais apunguziwe madaraka awe anateua Mawaziri, Manaibu Mawaziri na Makatibu Wakuu hawa wasiingiliwe na mtu, lakini katika hizi ngazi nyengine lazima kuwe kuna uthibitisho au ushauri kwa taasisi nyengine. Sasa hapa sio kama umemvunjia heshima Rais lakini unaimarisha uwajibikaji. Kwa sababu leo kama Mkurugenzi angekuwa hateuliwi na Rais, Waziri angekuwa na mamlaka ya kuweza kumpa maelekezo na akayatekeleza. Lakini leo inafika pahala mpaka Waziri anaitisha vikao anaingiza mpaka Wakuu wa Mikoa vikao vya kusuluhisha na Wakurugenzi katika ripoti hii inasema. Jamani leo Waziri inafika pahala anajiona kama kinyago, hana maamuzi. Sasa mimi nadhani ifike pahala hizi nguvu wakati mwengine ndio maana nikasema na sisi ndio watengenezaji wa Katiba na Sheria. Mimi nimeshampelekea Mhe. Spika, nimepeleka hoja yangu binafsi ya marekebisho ya Zanzibar. Aa maana yake ngoja subiri kuna Katiba mpya kwa sababu haya tunayaona tunapata tabu katika utendaji hapa tunawasulubu wenzetu kwa makosa ambayo hawakufanya wao.

Kwa mujibu wa taratibu watendaji wako wanapoboronga unatakiwa uwajibike wewe, lakini je tuna utamaduni huo. Juzi tuliona kuna nchi moja sijui sina uhakika vizuri kuna mtendaji mkuu ndani ya serikali amejiuzulu sio kama

kafanya kosa yeye, kuna kijana kwa kuwa ana uhusiano wa karibu na alifanya mambo yale kwa kuwa anataja jina la kiongozi yule akaweza kupata fursa mbalimbali. Baada ya kuvuja ile habari yeye mwenyewe akasema aa kutokana na tukio hili na mimi nilihusishwa kaamua kujiweka pembeni.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, haya kama hatujayarekebisha madaraka ya uteuzi tukayagawanya tukayapa mamlaka tofauti tofauti, Mhe. Mwenyekiti hapa tutakuwa hatufanyi kitu. Mfano mdogo tu kama jana, jana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa bahati mbaya kidogo ulikuwa katika majukumu mengine ya kitaifa, lakini ripoti ya serikali imekuja hatukuikubali. Kwa sababu kuna mambo ya msingi ambayo hata serikali yenyewe wamekiri hapa kweli huyu mtendaji wetu kakosea lakini wanasema tunamtaka aamue moja. Hee, mtu ameshakiuka mpaka maadili ya uongozi unasema aamue moja wakati serikali unatakiwa umwambie fanya hili baada ya muda fulani hujalifanya fanya hili tunaogopana, muhali mwingi.

Mhe. Mwenyekiti, jana serikali imetia mpira kwapani na ndio maana mwenzangu akasema hatukupata jawabu mpaka sasa hivi. Mimi naomba kwa sababu yale mapendekezo tuliyoyafanya tumeyafanya kwa nia njema kwa ajili ya kuiokoa serikali yetu, lakini vile vile katika utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi, kuondoa ubadhirifu ndani ya serikali, kutumia vibaya madaraka ndio tunayoyatekeleza hapa. Sasa ninakuomba sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ikiwa utataka ile Kamati Teule ukae nayo au Wenyeviti wote tutakuja kukupa baadhi ya maeneo ambayo serikali yenyewe imekiri ni makosa lakini bado inamwachia mtendaji aamue yeye. Sasa Mhe. Mwenyekiti kuna baadhi ya mambo kama haya kidogo inakuwa na yale maamuzi ya jana yametuvunja moyo, wengine leo tulisema bora hata tusiseme maana hatujui tunamwambia nani.

Lakini ninaamini kutokana na ufafanuzi alioutoa Mhe. Waziri jana na Mwanasheria Mkuu nilihisi kwamba wamekiri kweli kuna udhaifu lakini bado katika utekelezaji wa ule udhaifu utafanyika vipi hiyo jawabu hakuna.

Mhe. Mwenyekiti kuna kijana humu ametajwa, sisi tulimtaja katika ripoti ya Kamati Teule iliyopita na leo ametajwa tena, tena ametajwa katika sifa zile zile za ubadhirifu. Katika ripoti ya Kamati Teule iliyopita, katika kadhia ambayo ndugu yetu, dada yetu, si vizuri kumtaja lakini kwa kweli kadhia ilimkuta, na kwa kuwa ripoti ilimtaja si vibaya kumtaja alikumbana na tapeli huyu. Kuna kijana humu ameandikwa anaitwa Ramadhan Abdalla Songa, mimi huyu namwita tapeli kwa sababu alihusika mpaka ku-*forge document* ya Mzee Ali Kidawa aliyoizungumza Mhe. Mshimba ame-*forge* akaenda akamtisha mpaka Sheha akamwambia anatoka nyumba kubwa, *hansard* zipo eti anasema anatoka kwenye nyumba kubwa, sheha akatishika, akatetemeka katoa vielelezo imekwenda kutengenezwa *document, document* hati, tunamuita yule mzee anasema mimi saini si yangu lakini lile jengo alikabidhiwa na mzee wa kihindi ambaye alikuwa hana familia.

Yeye katika urithi wake anamwambia aa mimi wakati wowote ninaweza nikafariki utakuja ukosa, anamwambia chagua shamba la Shakani au chagua nyumba ya Mji Mkongwe, akamwambia mimi nitachukua nyumba ya Mji Mkongwe. Lakini mzee yule kutokana na taaluma ndogo hakuwahi kwenda kuomba kwenda kuandika *document.* Kaja huyu Ramadhan Songa tena katumia jina lake hilo hilo katengeneza kitambulisho ikaandikwa hati akaenda akamtapeli yule mama, kamchapa milioni ishirini kanunua, Amina kanunua hati ile kisheria kwa sababu yeye kanunua *document* kwa mtu kwa mawakala wake, lakini je nani anayehusika, halafu *document* ile ile akaenda akachukulia mkopo akapata fedha akajengea hoteli.

Sasa kama yule mzee ile *document* angeitengeneza yeye akaenda Benki angepatia yeye mkopo, na ndio maana tukatumia busara kama Waheshimiwa basi huyu mzee angalau afidiwe ile ni busara. Ndio maana Mhe. Mwenyekiti ndio maana nikasema bora tusiyarejee haya lakini Mhe. Makamo wa Pili wa Rais atafute muda atutafute ili tuzungumze nae hili kiubinaadamu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti leo ametajwa tena Mhe. Ramadhan Abdalla Songa, Mhe. Mwenyekiti humu inasema vipi kuna fedha hizi milioni kumi, tukaambiwa katika ripoti hii Kamati imeambiwa ziliingizwa kimakosa katika akaunti ya ndugu Ramadhan Abdalla Songa. Makosa yale yakaja yakajirejea tena akaingiziwa tena milioni ishirini katika akaunti yake zimeingizwa kimakosa, mimi nataka niulize maana yake haya itakuwa mambo ya Kikwajuni mlango wa mbele unaujua unataka kupitia mlango wa nyuma.

Mhe. Mwenyekiti mimi ninavyojua unapokwenda kumuingizia mtu pesa kwanza unatakiwa jina lake na akaunti namba yake unakosea mara mbili hapo tena unakuwa unafanya makusudi. Sasa huyu alitajwa katika ripoti ya mwanzo, ina maana huyu ka-*forge document* ya serikali akawadanganya watendaji wa serikali haki ya mtu akauziwa

mtu mwengine na yeye ndiye aliyehusika na kuuza wakati yule mtu yeye hakuhusika. Na huku katika Baraza la Manispaa amehusika tena. Kuna fedha huyu mtu keshajenga milango ya maduka huyu anadai fedha zake, fedha zile anaambiwa zimekosewa zimeingia kwenye akaunti ya Abdalla Songa halafu anaambiwa yuko Dubai kaenda kufanyia biashara.

Mhe. Mwenyekiti huu mchezo wa kuigiza. Sasa jana Mhe. Mwanasheria Mkuu alisema kulikua kuna mambo mengine yanataka kupelekwa mahkamani, sasa hapa hatumjui nani wa kumpeleka mahkamani maana sisi Kamati tushaona huyu mkosa. Sasa serikali sijui wao itamburuza mahkamani, sasa hapa mimi ninafikiri Mwanasheria Mkuu aje atwambie, huyu Songa nani atakayemburuza mahkamani, keshaidanganya serikali mara mbili. Na nina wasiwasi katika ripoti nyengine za Kamati Teule sijui kama hatokuja kutajwa tena. Kwa hivyo ina maana Mhe. Mwenyekiti kuna watu humu wanakuwa madalali wanacheza na watendaji wetu wa serikali wanachukua fedha wanakwenda kufanya biashara, huku wananchi wetu wanaambiwa wajiunge kwenye saccoss watapewa mikopo, huku kumbe kuna watu wanaingiziwa mapesa wanakwenda kufanya biashara.

Mhe. Mwenyekiti kwanza fedha hizi kwanza azirudishe, lakini huyu kutokana na kudanganya *document* tofauti za serikali na huyo aliyemtilia hizi pesa huyo hakukosea kafanya kusudi, na yeye huyu hatua za kinidhamu zichukuliwe. Huu ni wizi, mwizi anapandishwa mahkamani huwezi ukakosea kuingiza pesa mara mbili kwenye akaunti ya mtu. Sasa utaandika jina basi ata namba ya akaunti? Tena mimi naomba tena huyu ndugu Ramadhan Abdalla Songa akaunti yake ikaangaliwe, ichunguzwe fedha anazozipata anazipata wapi kwa njia gani na kwa shughuli gani, hawa ndio matapeli wenyewe. Tumepitisha sheria *money laundering* tumesema watu wahojiwe jinsi gani wanavyopata mali zao, ndio watu wanapata mali kama hivi kwa milango ya nyuma.

Mhe. Mwenyekiti mimi nataka niseme kwamba sasa hivi wakati wa kufumbiana macho jamani uwe basi. Mhe. Makamo wa Pili wa Rais tunakuonea huruma sana, maana tukisema serikali ndio tunakwambia wewe, hawa watendaji wako Mheshimiwa watakuangusha hawa, sisi tunakupenda sana lakini watendaji wako wanapofika kukuangusha itabidi sasa tutumie kile kifungu chetu maana hatuna njia nyengine. Sasa hatutaki tufike huko, ninaamini kutokana na maoni yetu haya utachukua hatua zitakazofaa.

Mhe. Mwenyekiti mimi nataka niseme kwamba katika masuala ya manunuzi hili tuna tatizo kubwa lazima tukiri, tatizo kubwa hasa sisi tulipokwenda katika Kamati ile ya mwanzo tumegundua kwamba malipo yamekuwa yanafanywa kinyume cha utaratibu. Lakini vile vile wale wanaofanya malipo wanakuwa sio kama wanakosea wanakuwa wanafanya kwa makusudi. Mfano kama haya malipo yaliyofanywa kwenye makontena ya Darajani. Inalipwa *amount* ile ile 2,356,585 kwa tarehe ile ile lakini katika *cheque* tofauti. Kwa hivyo ina maana hapa ndio fedha zile watu wanatia huku halafu wakitoka huko watu wanakwenda kugawana mbele ya safari. Kwa hivyo mimi nadhani tuhakikishe hizi taratibu zetu zinafuatwa.

Lakini nije katika malengo. Mhe. Mwenyekiti pamoja na ubadhirifu uliofanyika lakini yale malengo yaliyokuwa yanafanywa yalikuwa yana nia njema. Mwalim Nyerere aliwahi kusema siku moja njia ya motoni imejaa, nia njema Mwalim Nyerere amewahi kusema katika hotuba zake. Maana yake lile unalolifanya zuri lakini unatumia njia za haramu tupu ndio hiyo una nia nzuri kuboresha lakini je njia unayotumia kuboresha ni sahihi na huo ndio uliokuwa ndio msamiati wake.

Mhe. Mwenyekiti ukiangalia hii mikataba iliyofungwa ya wenye mabango yote ilikuwa ina nia njema kwa sababu gani ilifika pahala ikawa tunapiga kelele mji wa Zanzibar hauna tofauti na kijiji cha nchi yoyote. Mji kiza hakuna taa kutokana na maarifa wanaotumia wenzetu Baraza la Manispaa wakabuni, na huu mradi kama tulivyosema huu mradi Mkurugenzi kaukuta tokea enzi ya Mabrouk Jabu, walianza kufunga mikataba ya hawa wamiliki wa mabango ili waweke matangazo yao ya biashara lakini wawaruhusu kuweka taa. Tunawashukuru Baraza la Manispaa taa zinawaka tena kunapendeza, maji yaliruka pale kwenye bwawa la Michenzani, lakini taratibu zilifuatwa. Maji yameruka tukasherehekea tukasema *alhamdu lillahi rabbil alamina* angalau Mzee Karume anakumbukwa sasa hivi. Kajenga Michenzani pale kaweka *round about* yeye karusha maji tunaambiwa hakusoma karusha maji, sisi tulosoma maji yametushinda. Wenzetu wamekuja wamerusha maji lakini ndio ile kwa njia ile ile ya Kikwajuni, mlango huu watu wamepitia mlango mwengine.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ndio maana nikasema nia yao sio kama ilikuwa mbaya, Manispaa watu wengine wanaweza yale mabango wakaanza kwenda kuyang'oa unaona ubadhirifu, jamani yale mabango yamewekwa kwa nia njema kulisaidia Baraza la Manispaa kujiongezea mapato kwa ajili ya kutekeleza shughuli zao. Na mimi ninafikiri tokea

kuundwa Kamati Teule, utendaji wa Baraza la Manispaa umebadilika sana, sasa hivi wanafanya kazi vizuri bustani zinatengenezwa, sasa hivi utakuta usafi mzuri, kumbe hewe hewe inasaidia. Hata jana Mhe. Mwanasheria Mkuu anasema pamoja na kwamba mnasema serikali nini lakini ripoti zenu zinatusaidia kweli. Alau kidogo kuna baadhi ya utendaji kuna sehemu nyengine unarekebishika. Lakini tuchukue hatua zaidi ili utendaji uzidi kuwa mkubwa zaidi.

Mheshimiwa kuna jambo moja nimeliona limejirejea sana Baraza la Manispaa, na ninaomba kufanyike mabadiliko makubwa sana katika Baraza la Manispaa sio kusema Mkurugenzi tu awajibike imetosha kwa sababu pale kuna *chain* Mheshimiwa, kitengo cha Masjala kibovu. Leo Mwenyekiti wa Kamati huku anazungumzwa hivi na Mkurugenzi akienda huku lete kumbukumbu unaambiwa kumbukumbu imepotea humu kwenye ripoti ya Mwenyekiti kuna kumbukumbu karibu nne mpaka tano, unaambiwa zimepotea au zimeibiwa na watendaji wa Manispaa. Hapana walinzi pale, ina maana hapa panafanyika mchezo mchafu halafu watu wanaiba *document*. Kwa hivyo ina maana huu mchezo unaonesha mchezo huu ushazoeleka katika Baraza la Manispaa, kwa pale lazima reki iende kubwa pale, liende fagio la chuma likasafishe, hata hiki kitengo cha Masjala hakifai kwa nini *document* za serikali zinapotea.

Mhe. Mwenyekiti ndio ile inayotokezea unaambiwa siri za serikali zinavuja ripoti hii ndio imeshatwambia maana yake kama *document* imepotea imekwenda wapi? Aidha kaichukua mtu kenda ichoma au kenda kufungia maandazi au kaificha, kuficha nini, ushahidi. Mhe. Mwenyekiti hili pia nimeliona upotevu wa kumbukumbu katika eneo la Baraza la Manispaa linahitajika. Suala la upandishaji wa vyeo mimi nafikiri pakishawekwa *re-shuffle* kubwa pale mimi ninafikiri watakaofuata nadhani wataweza kuwajibika vizuri.

Mhe. Mwenyekiti *super market* hapa ndio watu walipokuwa wanaoneshana misuli, kila mtu anaonesha msuli wake, Mkurugenzi anaonesha msuli wake, huku Waziri anaonesha msuli wake. Lakini sasa matokezeo yake kulikuwa hakuna maamuzi ya pamoja, kwa sababu maamuzi yote mpaka yanakwenda yalikuwa yanavutana. Sasa hili tumsaidieni Waziri tukishaweka sheria za serikali za mitaa zile hakutotokea tena mvutano baina ya Waziri na Mkurugenzi, au Mkurugenzi na Wenyeviti wa halmashauri.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tumeshapata malalamiko mengi ya Wenyeviti wa Halmashauri kuhusu makatibu wao. Kwa sababu huu mgongano tusiuone leo alivyosema Mwanasheria Mkuu leo limeangukia Manispaa, haya mambo yapo kila pahala hata huko katika Halmashauri kuna matatizo. Sasa tukiweza kurekebisha hizi sheria mimi nafikiri matatizo kama haya hayataweza kujirejea tena.

Hili la mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumzie bustani ya *Jamhuri Garden.* Mhe. Mwenyekiti, yule mwekezaji kwa kweli amefanya kazi kubwa ya kuweza kuliboresha lile eneo, lakini tatizo lililojitokeza kwamba kulikuwa hakuna umakini Baraza la Manispaa katika ufungaji wa mikataba. Kwa sababu ukiangalia yeye yule amelalamika lakini hata na wale wengine waliokuwa wanajenga maduka katika maeneo mbali mbali wamelalamika. Anapeleka hesabu yake nimejenga hapa nimefanya ukarabati au nimejenga kwa shilingi 18 milioni halafu huku Manispaa wanamwambia hizo nyingi, yani imekuwa kama biashara ya mapera, mtu keshajenga kwa gharama ya shilingi 18 milioni halafu unamwambia hizo nyingi nitakulipa shilingi 12 milioni halafu anakubali kwa hivyo inaonesha hapo pia kuna mchezo mchafu.

Kwa sababu mtu aliyetumia gharama yake mfano shilingi milioni kumi ukenda ukamwambia hizo nyingi bwana nitakupa shilingi milioni nane akakubali ina maana hata na yeye alikuwa anakudanganya. Sasa hii inatokana na nini? Hakuna utaratibu wa kuitisha *tender*, kwa sababu kama kungekuwa kuna utaratibu wa kuitisha *tender* basi ingeliitishwa vikatolewa vile vigezo, zikawekwa zile zikaja zikafunguliwa kwa hivyo ina maana ile bei iliyokubaliwa ina maana tayari imeshakubaliwa, lakini hata hawa waliofunga mikataba kwa kuwa na wao waliifunga kinyemela basi hata anapokuja kusema aa bwana wee mimi nimejenga kwa shilimi 20 milioni akiambiwa hizo nyingi shilingi 16 milioni atakubali kwa sababu anajua na yeye kapitia mlango siwo. Sasa mikataba hii yote inatokana na harufu ya rushwa.

Hapa kwetu sisi hatupendi sana kutumia neno ufisadi kwa sababu ufisadi ni neno kubwa sana, baya sana. Sisi hapa kwetu tunasema harufu ya rushwa na rushwa inakuwa *hmm*, inanuka. Sasa tuikemee rushwa hapa kwetu hakuna mafisadi lakini tuikemee rushwa na rushwa inatokana na pale tunapokiuka hizi taratibu.
Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubaliana na mapendekezo ya ripoti ya kamati lakini kama alivyosema Mhe. Omar Ali Shehe mimi nafikiri utaratibu tulioutumia safari hii kidogo tuliuhisi utakuwa mzuri

lakini tumeona si mzuri sana, kwamba wenzetu wakenda wakajifungia halafu wakasema hili silo kama silo bora tulizungumze hapa hapa, aah, hili silo tukiondoka hapa tunakubaliana ripoti ya pamoja. Hii Mhe. Mwenyekiti itakuwa haina lawama, hata kama waziri pengie Mkurugenzi wako unamuonea haya haya utakuwa hukuyafanya wewe tumeyafanya sote kwa pamoja. Waswahili wanasema "kifo cha wengi harusi".

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu mambo haya tukisema tukuachieni tu huko serikalini wengine wakati mwengine mkikaa kwenye *cabinet* huko sasa hapa ina maana waziri awajibike kusema mbele yake hamuwezi kumwambia awajibike, lakini tukisema hapa je, itakuwa hamkusema nyinyi tumesema pamoja. Sasa mimi nafikiri Mhe. Mwenyekiti, tujengeni utamaduni wa uwazi, tukijenga utamaduni wa uwazi watendaji wetu huku watajirekebisha naamini serikali yetu ina nia njema ya kuweza kuwatumia wananchi lakini bado kuna baadhi ya watendaji hawaheshimu katiba, hawaheshimu kanuni, hawaheshimu sheria na maadili yao ya uongozi.

Keshokutwa tunakwenda kupitisha hii Sheria ya Maadili ya Uongozi tunajiuliza itatekelezeka? Lakini Mhe. Mwenyekiti, naamini hii itatekelezeka na baada ya hayo machache kama nilivyosema naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hamza Hassan Juma kwa mchango wako, lakini ningependa kukufahamisha tu kuwa Kikwajuni uliyokwenda kabla ya Mapinduzi sasa imebadilika kuna nyumba za maendeleo zina mlango mmoja tu, hakuna tena nyumba ya milango miwili.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na kwa kweli muda ulionipa ni muwafaka kwa kumalizia hoja yangu na naomba nichangie kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, inawezekana na wananchi wa kawaida hawawajui Wajumbe wa Kamati hii, sasa nataka nichukue nafasi hii niwakumbushe wananchi wa kawaida hasa wale wa Jimbo la Kiwani nani walikuwa Wajumbe wa kamati hii, ili waone kwamba kamati hii iliundwa na wajumbe makini, wanaokubalika na kwa kweli ambao wanaitakia mema nchi hii ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mjumbe wa mwanzo aliyekuwa Mwenyekiti ni Salmin Awadh Salmin, huyu Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni lakini ana sifa tatu kubwa. Sifa ya kwanza ni Mnadhimu wa Wawakilishi wa CCM Barazani na ni Mnadhimu wa CCM kwa sababu CCM ndio Chama Tawala. Kwa hivyo, kwangu mimi na wananchi wa Jimbo la Kiwani ni mtu muhimu sana, anaongoza Wawakilishi wote wa CCM wasiopungua 45.

Sifa ya pili ya Mhe. Salmin Awadh ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM, huwezi kuchaguliwa urais kama hujapata Baraka za Mhe. Salmin Awadh kwa sababu ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM na sifa ya tatu ni Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi Zanzibar ambaye fedha zote za nchi hii yeye ndiye mwenyekiti lazima adhibiti. Kwa hivyo, wananchi wa Kiwani wajue kwamba Mhe. Salmin Awadh ni huyu wasione tu kwamba ni mtu aliyesoma ripoti kama ni mtu wa kawaida ni mtu mkubwa sana ambaye mimi namheshimu sana.

Mtu wa pili Mhe. Mwenyekiti, ni Mhe. Asha Bakari Makame ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Habari na Uvuvi, nchi hii ni wakulima na wavuvi. Kwa hivyo, Mwenyekiti wao pia alikuwa mjumbe wa kamati hii lakini pia ni Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake Tanzania kupitia CCM.

Mtu wa tatu Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ismail Jussa Ladhu ambaye kabla ya leo alikuwa ni Naibu Katibu Mkuu wa *CUF* Taifa na pia ndiye Mwakilishi wa Jimbo la Mji Mkongwe kwenye ofisi hiyo ya Manispaa.

Mtu wa nne ni Mhe. Mwanaidi ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto kamati ambayo inawajali sana wanawake na watoto wa nchi hii. Lakini makatibu wake Mhe. Mwenyekiti, ni wanasheria wawili wote ni wanawake. Wanawake wana sifa ya kuwa hawasemi uongo na pia wanawake wanakuwa waaminifu.

Mjumbe ambaye nimembakisha Mhe. Abdalla Juma Abdalla huyu ana sifa kubwa, kwenye kamati hii ni peke yake ndiye *alhaj*, amedirikiwa na Mwenyezi Mungu kwenda Makka. Kwa hivyo, hana tabia ya kusema uongo na hivyo ni mtu muaminifu na mimi namkubali. Lakini pia ni mnadhimu wa Wawakilishi wa *CUF* Baraza la Wawakilishi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika amewachagua watu watano hawa wenye kila sifa na mimi Mhe. Mwenyekiti nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Spika na kuwapongeza Wawakilishi hawa kwa sababu ya uwajibikaji wao na wajibu wao wa taifa hili la Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo sasa niende kwenye Ripoti. Ripoti hii imegusia mambo mengi, moja katika mambo ambayo imegusia ni suala zima la uidhinishaji wa fedha. Ripoti hii imesema kwamba kila penye kuidhinisha fedha palikuwa hapafuati sheria za nchi, hapafuati sheria za fedha. Na unaposema hivyo Mhe. Mwenyekiti, maana yake hilo ni kosa kwa mujibu wa sheria ya fedha ya Zanzibar ya mwaka 2005 na kanuni zake. Kwa hivyo, kila ambapo ripoti hii imegusa palikuwa na mapungufu hayo ya uidhinishaji wa fedha na kwa msingi huo ni kosa la kisheria. Sasa mimi sioni sababu sasa ya Wawakilishi kuulizwa tuchukue hatua gani wakati sheria imesema wazi kwamba mwenye kufanya kosa hili sheria inasema afanywe nini. Sasa serikali kuuliza Wawakilishi tufanye nini mimi kwa kweli bado nasema kwamba ni ule msingi wa kuwalinda watu ambao wamevuka sheria.

Lakini la pili ambalo limezungumzwa na ripoti hii ni suala zima la taratibu za manunuzi kwamba zimekiukwa. Vile vile sheria ya manunuzi imeeleza wazi utaratibu wa kufuata sheria na nini adhabu yake iwapo sheria haikufuatwa. Wala Mhe. Mwenyekiti, si jambo kabisa la kuulizwa wawakilishi sasa tufanye nini ikiwa sheria imevunjwa tayari sheria imesema hatua ya kuchukuliwa. Sasa serikali ina wajibu wake wa kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, njia ya muongo ni ndogo sana, Mhe. Hamza Hassan amesema hapa kwamba ripoti iliyopita ilimgusa mtaalamu mmoja wa ujanja anaitwa Abdalla Songa, na ripoti hii imemgusa vile vile Dr. Songa kwamba pia amejipatia shilingi 30 milioni kwa ajili ya ujanja na nina hakika na ripoti nyengine ya mbele itamgusa Dr. Songa. Sasa serikali inasubiri nini kuchukua hatua, hata hili pia bado anasubiriwa Mwakilishi mwenye kamati tuchukue hatua gani? Mtu aliyeandaa *document* kinyume na utaratibu maana yake huo ni uhaini na sheria iko wazi bado serikali inasubiri Wawakilishi kamati husika iseme tufanye nini.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani kwa msingi huu serikali itakubaliana nami kwamba serikali inawavumilia wale wote ambao wanaonekana ni matapeli na inaingia sasa ndani ya taasisi za serikali kufanya ujanja na watu waliokuwa si waaminifu ili kuhujumu taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba nyuma hapo Mhe. Makame Mshimba alipowasilisha ripoti yake nakumbuka siku ile na *hansard* ipo Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alikuwa mkali sana na kuonesha kama kwamba Mhe. Mshimba alikuwa ni mzushi hatimaye leo ukweli umeonekana. Hii ni dhahiri kwamba mawaziri wetu baadhi yao wana tabia ya kujenga utaratibu wa kuwalinda watu wasiokuwa waaminifu na kuona kama Wawakilishi ni waongo na labda wana chuki binafsi.

Nichukue nafasi hii Mhe. Mwenyekiti, kuwaomba wananchi wa Kitope kumuamini Mhe. Makame Mshimba kwamba ni jemedari na kwa kweli ni makini sana, yale yote ambayo aliyasema akiwa Mhe. Mshimba, Mwakilishi wa Kitope ndio ambayo kamati hii watu watano muhimu imeyasema yale yale. Sasa niombe tu kistaarabu kwa sababu Mhe. Waziri siku ile alikuwa mkali sana mimi ningeomba ingekuwa mimi ningesema basi leo naachia ngazi ili kujenga heshima yangu.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Waziri hili alione kwamba nidhamu pia ni uwajibikaji kwa hivyo angeona busara basi ya kupumzika katika nafasi hii ili akawaridhisha Wazanzibari kwamba kweli Wawakilishi wake hawafanyi uongo, Wawakilishi wake wana nia thabiti ya kujenga nchi na kamwe sisi Wawakilishi hatuna chuki na mtu kwa malengo binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine tabia ya Mkurugenzi imezungumzwa humu na hivi ndivyo walivyo Wakurugenzi wengi. Na hii ni ile hoja ya Mhe. Hamza aliyoisema kwamba, inawezekana kwa sababu Mawaziri Rais anawateua, Wakurugenzi Rais anawateua, wanadhani kwamba wana hadhi na nguvu sawa sawa sawa na Mawaziri, wamekuwa ni wasugu hawafuati sheria na wao wamekuwa ni wakaidi. Kwa hivyo, ni kweli kwamba kuna haja ya kupunguza mamlaka ya Rais katika uteuzi ili mamlaka tofauti ziwe zinateuwa watu kwa ajili ya uwajibikaji. Kwa msingi huu Mhe. Mwenyekiti, kila hatua ambayo ripoti hii imependekezwa kwa Mkurugenzi na watendaji wote ningeomba serikali ikachukua hatua wazi wazi. Hatua ya kuamua kujiengua, kuchukua likizo au kuwa Mjumbe wa Kamati ya CCM ya Taifa ili ukwepe majukumu yako ya uwajibikaji sio *solution*.

Kwa hivyo, serikali ichukue hatua Mhe. Mwenyekiti ili iweze kuwawajibisha wale wote ambao wamehusika kisheria kwa maana kwamba wengine waache nafasi zao na ikibidi wengie wapelekwe Mahkamani kwa kuhujumu taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, hii ni dhahiri kwamba hata ile hoja ambayo niliitoa ya ujenzi wa *Shopping Mall* pale Darajani ambapo Mhe. Waziri pia alipinga sana lakini mimi nilikuwa na barua siku zile, nilikuwa na barua ambayo Mkurugenzi ameisaini, amewanyima wazalendo Wazanzibari ambao walipeleka nia yao ya kujenga *Shopping Mall* Darajani akawanyima na akampa Mtaliana. Ni mtindo huu huu kwamba kila mwenye rushwa ndiye anayemkumbatia unawanyimaje Wazanzibari wazalendo wenye uwezo wa kujenga na ukaamua kumpa mtu mmoja mgeni ushahidi leo ni huu, kwamba Mkurugenzi huyu alikuwa na tabia ya kung'ang'ania wale watu ambao wanapenda rushwa na wanapenda kutoa fedha kwa ajili ya maslahi yake.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia kamati hii naomba Mhe. Waziri azingatie sasa umuhimu wa kuwapatia wazalendo fursa za kujenga *Shopping Mall* badala ya kumpa Mtaliana kwa sababu kumedhihirika dhahiri kwamba Mkurugenzi alikuwa na maslahi yake kwa ajili ya kujinufaisha yeye binafsi.
Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa naikumbusha serikali kwamba Katiba ya Zanzibar kifungu cha 45(5) imesema wazi na Mhe. Mwenyekiti, naomba ninukuu.

Kifungu 43(5) kinasema kwamba:

> "Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya mamlaka ya Rais ndio itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya sera za Serikali kwa ujumla, na Mawaziri chini ya uongozi wa Makamo wa Pili wa Rais watawajibika kwa pamoja katika Baraza la Wawakilishi kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar".

Mhe. Mwenyekiti, serikali ikubali kwamba muhimili huu wa kutunga sheria ndio muhimuli ambao unasimamia na kuwajibisha serikali. Si halali, si sahihi muhimili huu kuonekana kwamba uko chini ya mamlaka ya utendaji na hivyo ni kuvunja Katiba ya Zanzibar na kukiuka masharti ya sheria zote.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie tu kwa kusema kwamba, ripoti iliyopita ya Kamati Teule na ripoti hii ya leo na ripoti mbili zijazo mbele yake Wazanzibari wanahitaji kupata majibu yake na wala kamwe hawahitaji ubabaifu na kufanyiwa hadaa, kila aliyehusika na ubadhirifu wa mali za umma awajibike ikibidi arejeshe, ikibidi apelekwe Mahkamani kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono ripoti hii nawatakia heri Wajumbe wa Kamati hii na kwa kweli Mwenyezi Mungu awajaalie heri na baraka kubwa sana. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe. Waheshimiwa Wajumbe kwa vile muda uliobakia ni mchache mno hata tukitoa nafasi kwa Mhe. Ali Salum hatoweza kutumia, tuombe basi kwamba nichukue fursa hii kuweza kumuomba Mhe. Ali Salum ili jioni atakapokuja atakuja kuchangia pamoja na Waheshimiwa wengine ambao watapenda kufanya hivyo.

Baada ya maelezo hayo basi nichukue fursa hii tuakhirishe Baraza hili hadi jioni saa 11:00 barabara. Ahsanteni.

(Saa 6:55 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kupata fursa hii adhimu kuweza kuchangia taarifa ya Kamati Teule ya Baraza la Manispaa.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza ningependa kutoa pole sana kwa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais. Pole yangu Mhe. Mwenyekiti, ninapenda kumpa Mhe. Waziri kutokana na kubeba mzigo mkubwa ambao hauna mfano kwani ni katika wizara ambayo ina taasisi nyingi sana, basi ni Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais.

Wizara hii Mhe. Mwenyekiti, imebebwa na vikovi vya SMZ, Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Manispaa na Halmashauri ukiachia mbali hiyo Ofisi ya Rais yenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pole hizo nichukue fursa hii adhimu kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati Teule chini ya mwenyekiti wako jemadari Mhe. Salmin Awadh Salmin. Sisi wengine hatukupata kigugumizi baada ya Mhe. Spika kumtangaza Mhe. Salmin kuwa miongoni mwa wajumbe wa Kamati Teule, kwa sababu tunamfahamu fika kwamba Mhe. Salmin ana uzoefu wa kutosha katika taasisi ile.

Kwa hivyo tulikuwa tunajenga imani kwamba mapendekezo yatakayoletwa, taarifa zitakazopatikana basi zitakuwa ni sahihi na zitazisaidia serikali katika kuondosha ile hali halisi ya ukiritimba wa Baraza la Manispaa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya dibaji hiyo ndogo na mimi nianze kuchangia ripoti hii. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, ripoti nimejaribu kuifuatilia kifungu baada ya kifungu, ukurasa baada ya ukurasa sikuacha kitu. Hii ilinipa wepesi kabisa Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu na mimi miaka miwili mitatu iliyopita nilikuwa mdau mkubwa wa Baraza la Manispaa.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Manispaa nimelitumikia kwa muda miaka 10, nikiwa kama Diwani kwa vipindi vitano kwa awamu mbili; nikiwa kama Diwani wa Mikunguni lakini awamu ya pili nikiwa Diwani wa Wadi ya Kwahani. Kama kuna mtu analifahamu Baraza la Manispaa basi ninadhani ndani ya Baraza hili tutakuwa ni watu; mimi na Mhe. Salmin Awadh Salmin.

Mhe. Mwenyekiti, chombo cha Baraza la Manispaa kwa kweli ni chombo ambacho kinafanyakazi katika mazingira magumu katika pande mbili, pande ya Waheshimiwa Madiwani na pande ya watendaji. Kwa nini niseme hivyo Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu uhalisia wa Baraza la Manispaa huko nyuma linakotokea mwanzo wake ile taasisi ilikuwa ni kama taasisi ya kupelekwa wafanyakazi manunda, wafanyakazi ambao wameziuwa taasisi zao basi kuziuwa zile taasisi na taasisi kuvunjwa wanachukuliwa lile Baraza linakuwa ndio jaa la kutupia wale watendaji.

Mhe. Mwenyekiti, pale waliletwa wafanyakazi kutoka katika Serikali za Mitaa ambao walikuwa wanafanya kazi kupitia kwenye Serikali za Majimbo. Lakini baada ya watu kulifilisi Shirika la Bizanje basi karibuni maafisa wa Bizanje wote walioifilisi serikali hii, ndio waliochukuliwa wakatupwa katika jaa lile. Sasa kitengo kama hicho kuweza kufanya kazi, kazi ambayo tutegemee tujenge imani wananchi ni pahala ambapo pazito sana.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka 2000-2005 Baraza la Manispaa lilikumbwa na misukosuko mbali mbali, ilifikia pahala migongano ninayoizungumza hapa ilifikia pahala mpaka Madiwani wakajenga azimio la kutaka kumuondosha Meya baada ya mfarakano wa watendaji na Madiwani, na serikali kuu ikaunda kamati ya kuchunguza kadhia hiyo. Wakati huo Mstahiki Meya alikuwa Mhe. Ahmed Kessy.

Mhe. Mwenyekiti, yote ninazungumza hayo kwa kusema kwamba kama serikali haikuwa makini na madhubuti basi taasisi ile itakuwa kila siku tukenda ni kashfa tu. Namuomba sana Mhe. Waziri ajenge umahiri katika kulisimamia Baraza la Manispaa. Vyenginevyo kama wanavyozungumza wenzangu tutafikia pahala watu watakuja kumuhukumu pasipo na hatia, kwa sababu taasisi inapofanya uzembe, msimamizi wa taasisi basi inabidi majanga yote yakufuate wewe.

Mhe. Mwenyekiti, maamuzi magumu ambayo ninataka nimwambie Mhe. Waziri hapa, kwa bahati mimi nimekuja na gazeti la Nipashe la leo, niliangalia kwa haraka haraka na ninaomba ninukuu kwenye ukurasa wa 12. Inasema kwamba, “Halmashauri yatimuwa na kuwavua madaraka maafisa wa Halmashauri hiyo”. Hao wenzetu wa Tanzania Bara.

Lakini pia nilikuwa na *reference* za baadhi ya mawaziri Mhe. Mwenyekiti. Hapa niliweka *reference* ya Mhe. Mwakiyembe alipofika bandari na kuona utendaji si mzuri akatimua baadhi ya maafisa lakini pia nina *reference* ya Mhe. Waziri wa Afya Dk. Hussein Mwinyi baada ya maafisa wa bohari kununua madawa yaliyokuwa hayana ubora na kuwatimua wote ambao walihusika.

Mhe. Mwenyekiti, imefika haja na wakati utamaduni wa Mawaziri wetu wa Tanzania Bara basi kuigwa na Mawaziri wa Tanzania Visiwani. Kwa sababu pasipo na kuchukua hatua Mhe. Mwenyekiti, kwa watendaji wabovu na

wakorofi, inabakia ndio ile ile kufanya kazi kwa mazoea, watendaji wanakuwa nidhamu hakuna kwa sababu inakuwa hawaoni kwamba kuna jambo ambalo hatua itachukuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba hilo sana kwa upande wetu katika suala la kutafuta mabadiliko kwa Waheshimiwa Mawaziri katika taasisi zao wanazozisimamia, lakini pia nimuombe Mhe. Waziri kama alivyomuomba mwenzangu Mhe. Waziri hebu tuharakishie sera ya *local government* utuletee ili iweze kufanya kazi kuweza kupunguza hii migongano iliyokuwepo.

Mhe. Mwenyekiti, nasema pasipo na kutengeneza sera basi bado taasisi yetu ya Manispaa tutabakia kuilaumu, tutabakia kuibebesha lawama kwa sababu pana tatizo ambalo haliwezi likaepukika. Hakuna afisa ambaye hafahamu taratibu za Baraza la Manispaa au aliyekuwa haielewi Sheria Nam. 3 ya mwaka 1995 ya Baraza la Manispaa au hafahamu Kanuni za Baraza la Manispaa.

Madiwani wanazielewa, watendaji wanazielewa. Tatizo lililokuwepo pale ni mvutano baina ya maafisa kupitia nafasi ya utendaji na Waheshimiwa Madiwani. Kwa sababu kiutaratibu suala lolote ambalo linatakiwa lipitishwe katika Baraza la Manispaa liwe la matumizi au la utendaji wa kawaida, ni lazima lianzie kwenye kamati baadae liende kwenye *full council*, likitoka katika *full council* ndio watendaji wanatakiwa walifuate. Lakini mvutano huu na mgongano huu unapelekea watendaji kufanya yale ambayo wanayoyataka wao kwa maslahi yao.

Mhe. Mwenyekiti, na hili linafanyika kwamba baada ya kukaa vikao vya Waheshimiwa Madiwani, Mkurugenzi huamua kufanya vikao vyake yeye mwenyewe na maafisa wake na ndio zinapokuja zile kauli za kebehi, kwa sababu anachokiona yeye hakuna mtu anayemshughulisha. Anakwambia hasa mimi nimeteuliwa na Rais bwana, nyinyi mutasema katika Baraza lenu mpaka mutamaliza lakini hamna jambo ambalo munaweza mukalifanya kwangu mimi au hatua ambayo munayoweza kuchukua kwangu mimi.

Sasa hili ni tatizo Mhe. Mwenyekiti. Sasa sijajua hiyo sera inayokuja imeandaa utaratibu gani katika suala la kumpata Mkurugenzi. Imani yetu kwamba ingelikuwa Mkurugenzi anachaguliwa na Baraza la Manispaa basi mimi nina imani kwamba angefuata utaratibu wa Waheshimiwa Madiwani katika suala zima la utendaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na yote mara nyingi huwa siachi kuzungumzia pande zote mbili, pamoja na ubaya wa Baraza la Manispaa lakini pia wana wema wao ambao wameufanya. Lakini ndio ule wema ambao tunaouzungumza hivi sasa umekuwa wema wa mchwa.
Mhe. Mwenyekiti, wema wa mchwa huamua kutafuta mazingira ya kujenga nyumba yake lakini mazingira ya kujenga nyumba yake anakuwa anabomoa nyumba ya mwenzake. Sasa hili ndio tatizo la Baraza la Manispaa.

Wanajaribu kutengeneza mazingira mazuri lakini matokeo yake wanakuwa ni watu wakubwa wa kufilisi mali za serikali kwa kufunga mikataba ambayo iliyokuwa haieleweki, kwa kutumia matumzi ambayo hayafuati utaratibu, hiyo ndio hali halisi.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba lile chaka linahitaji kazi ya ziada na nimuombe Mhe. Waziri akafyeke chaka kwa maslahi ya Serikali ya Zanzibar na wananchi wa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, chaka lile sisi tuliwahi kulifyeka mwaka 2002 baada ya kufika pale kuona ile hali halisi ya Baraza kuendeshwa katika *system* ya kidugu na kifamilia.

Mhe. Mwenyekiti, tulijaribu kufyeka tukaondosha maafisa wote na tuliweka maafisa kwa mujibu wa CV zao na sifa zao. Lakini hali imerudi kama ilivyokuwa huko nyuma. Hali hii Mhe. Mwenyekiti, inapelekea kuharibu mazingira ya kila aina. Kazi hiyo ilitufikisha pahala tukaweza kugundua marisiti feki, mikataba feki, watu walikuwa na mihuri majumbani lakini tuliamua kudhibiti.

Mhe. Mwenyekiti, udhibiti huo ulifikia kuongeza mapato kwa asilimia 200 zaidi kutoka milioni 400 mpaka bilioni 1. Sasa hii ni hatari Mhe. Mwenyekiti, tusiposimamia vizuri basi hali ya wananchi itakuwa imo mashakani kwa sababu wananchi wanyonge wa nchi hii ndio wanaokamwa maziwa katika kila hali. Kwa sababu wao ndio wanaofanya biashara, kodi zinatoka kwao, ziwe za usafi, ziwe za leseni za kila mwaka. Sasa kunatokezea wajanja baadae inakuwa ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina maeneo mawili matatu ambayo nimejaribu kuyaangalia katika ripoti hii ya Kamati Teule. Kwenye ukurasa wa 12 kuhusu kutowasilishwa nyaraka kwa kusingizio cha kuibiwa. Niwapongeze sana kamati kwa kazi nzuri waliyofanya na kugundua hili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninataka nikuthibitishie kuwa hapa kamati imepigwa changa la macho, hakuna nyaraka iliyoibiwa wala iliyopotea. Mhe. Mwenyekiti, baada ya kelele za Baraza la Wawakilishi katika kuzungumzia kadhia ya Baraza la Manispaa, hapa ndipo baadhi ya watendaji walipoanza kuzitafuta nyaraka wao wenyewe na kuzitorosha kwa makusudi kwa kisingizio kutaka kuficha hii hali halisi ya upotevu wa mali na fedha za serikali katika Baraza la Manispaa.

Mhe. Mwenyekiti, nikuombe sana na nimuombe Mhe. Waziri alifumue Baraza la Manispaa lote, *otherwise* itakuwa kila siku kazi yetu kupiga kelele lakini hakuna liwalo. Mhe. Mwenyekiti, pia nilikuwa naomba nizungumzie katika suala la kutokutumia wataalamu husika ilikuwa ni njia moja ya upotevu wa mapato.

Mhe. Mwenyekiti, haya masuala yanafanywa makusudi. Mkurugenzi anafanya mambo haya ya kuwakataa maafisa kwa njia mbili. Aidha za kutokuwapa kazi au za kutumia watu ambao hawana sifa makusudi kwa maslahi yake katika kujipatia hizo watu wanasema pesa haramu.

Mhe. Mwenyekiti, sababu ya kusema hivi, mimi ninazungumza kwa evidence kabisa kwa sababu ninasema ninalijua Baraza la Manispaa *in and out*. Pale palikuwa pana *sister* alikuwa anaitwa Maryam alikuwa ndiye mkuu wa utawala, lakini cha kushangaza ameondoka mkuu wa utawala, amekwenda kuchukua *master*, amerudi baada ya kukaa ile nafasi yake ameondoshwa kenda kuekwa ofisi msaidizi wa uhusiano.

Mhe. Mwenyekiti, yule sister kutokana na kadhia ile ameamua kuomba kazi sehemu nyengine ya kazi kutafuta uhamisho, kwa maana amehama. Pale palikuwa na ndugu yetu anaitwa Abdalla Ali Kombo, alikuwa ni afisa mipango. Amekwenda kuchukua *master*, karudi pale ofisi hakupewa, anaambiwa hana kazi ya kupangiwa.

Mhe. Mwenyekiti, mzee wetu yule amehangaika mpaka ninashukuru serikali imemuona Afisa Tawala Mkoa wa Kusini kwenye Wilaya. Sasa hayo ndio matatizo ya Baraza la Manispaa kwamba wataalamu ambao wana sifa huwa hawatakiwi na hawatakiwi kwa sababu za msingi kabisa, wawekwe watu ambao mmoja wapo akae juu awatawale. Ndio kazi zote zinabakia zinafanywa na mkurugenzi, yeye ndiye atakuwa afisa muajiri, yeye ndiye mhasibu, afisa mnunuzi kwa sababu ndio tatizo, hakuna watu ambao wenye uwezo ambao yeye anahisi wale watafanya kazi zao kwa mujibu wa utaratibu, kwa sababu wale taratibu wanazielewa.

Sasa haya mambo katika Baraza la Manispaa yanafanywa kwa makusudi Mhe. Mwenyekiti, na ndio maana nikamuomba Mhe. Waziri kwamba kupitia taarifa ya Kamati Teule akafumue Baraza la Manispaa. Vyenginevyo tutakuwa kazi yetu siku zote kuchukua lawama na malalamiko ya Baraza la Manispaa.

Mhe. Mwenyekiti, pana vitu vingi vya kusikitisha na ninasema kwa kuwa ninapafahamu. Hivyo leo Mhe. Mwenyekiti, hatuoni aibu kazi za bustani aende akapewe mtu kwa kufunga mikataba wakati Baraza lina wataalamu, lina kitengo cha bustani, lina mtu mwenye elimu yake. Tuna kijana wetu Rajab Salum pale ni mtaalamu kabisa wa mambo ya afya na bustani, lakini tulichukua mtaalamu kutoka Wizara ya Kilimo, tumekwenda kumuomba Wizara ya Kilimo aje pale kusaidia utaalamu wa bustani lakini hawa wote waachwe akapewe mtu kufunga mkataba wa kutengeneza bustani kwa mamilioni ya pesa.

Mhe. Mwenyekiti, haya ni mambo ya makusudi. Lakini tuna *engineer* ndugu yetu Mzee ana digrii mbili kama sikosei. Lakini aachwe *engineer* Mzee na utaalamu wake na uwezo wake akapewe papasi tu kujenga masoko yote ya Manispaa. Hizi ni mbinu za kuficha maovu katika suala zima la ubadhirifu wa Baraza la Manispaa.

Mhe. Mwenyekiti, ninasema tutasema mengi, tutapiga kelele sana. Mimi kuna kitu kidogo tu katika Kamati Teule ambacho sijakipata na kwa kweli hiki kilikuwa kinanisikitisha sana au kama sijakiona, basi labda baadae baada ya kufungwa majumuisho kidogo hili ninaweza kusaidiwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sijaona hasa gharama halisi ya upotevu ndani ya Baraza la Manispaa. Nimeona vipengele, kama soko la Darajani sijui milioni hamsini, sijui labda Jamhuri *Garden* tumepoteza labda milioni ishirini, soko la Kwerekwe, sijaona *actual* kwamba kuna *figure* halisi ya kipindi cha karibuni labda miaka mitano ndani ya Baraza la

Manispaa kilichopotea. Hiki sijakiona, sijajua labda kwamba kuna bilioni mbili au bilioni tatu. Mhe. Mwenyekiti, sasa kama kipo labda tutapewa taarifa halisi ya kiasi gani ambacho kimepotea ndani ya muda wa awamu hii iliyopita.

Mhe. Mwenyekiti, ninasema taasisi ya Manispaa ni taasisi nzito, taasisi ambayo inatupotezea sifa mpaka wana siasa. Hufikia pahala tukaonekana kuwa hatuna uwezo, kumbe ni *demotion* ya watendaji.

Mhe. Mwenyekiti, Manispaa hakuna Meya aliyedumu vipindi viwili. Kwa makusudi na sio Meya tu, hata watendaji wenyewe hawadumu. Sasa mvutano ni mkubwa. Mimi ninaingia pale Kibanzi anaaga. Nimeanza na Ahmed Kessy, nimekuja na Mahabubu, leo yupo Khatib. Kila awamu anakaa Meya na kila Meya anaonekana anashindwa kusimamia kazi zake, hafahamu kitu, kumbe tatizo ni watendaji kutokana na ulafi wao, kutokuwa na kutokufuata sheria za nchi. Hili ndio tatizo Mhe. Mwenyekiti.

Hawa wakurugenzi ndio hawasemeki. Kila mkurugenzi akikaa ni mtihani. Hili ni tatizo sana. Kwa kweli kama kuna watu wa kuwaonea huruma Mhe. Mwenyekiti, basi tuwaonee huruma sana Waheshimiwa Madiwani kwa kazi wanazozifanya na kujituma lakini wanapelekeshwa na watendaji.
Mhe. Mwenyekiti, taratibu zote zipo. Ninasema nina uzoefu wa kutosha na sio kama nilikaa pale kama Diwani tu, sikuwa backbeacher Manispaa kabisa, nilikuwa nipo *frontline*. *I was a chairman for two periods*; *chairman of Town Plan* na *chairman of Social Service* ndani ya Manispaa. Kila kipindi nilikuwa ni mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, na kila tunalolieleza ukiondoka pale, watu wanaondoka wanakwenda kufanya kikao chengine kubadilisha lile ambalo mumelitaka. Mutaeleza taratibu za kutoa vibali lakini ukiondoka pale, vibali baada ya kutolewa afisini watu wanakwenda kutengeneza vibali majumbani. Hilo ndio tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, ulizuka mtindo pale Mhe. Salmin Awadh anaufahamu sana kwa sababu awamu yake yeye ndio ulikuwa mkubwa, lakini sisi baada ya kuingia tukaupiga vita. Ilikuwa taka hazizolewi Manispaa Mhe. Mwenyekiti, watu wanaziacha makusudi wapate sababu ya kwenda kukodi vijiko katika taasisi za watu binafsi.

La kuchekesha kwamba ndani ya taasisi za serikali kulikuwa kuna vijiko lakini pia vilikuwa havitakiwi. Watu wanakaa miezi mitatu unaambiwa taka zimekuwa nyingi, tunataka operesheni, wanaidhinisha milioni kumi na tano au kumi operesheni kwa muda wa siku tatu, mafuta yanayotumika sijui lita elfu mbili makusudi watu wanatafuta njia za kula tu. Lakini tulifika pahala hili tukalidhibiti.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninataka kumalizia kwa kumpa pole sana Mhe. Waziri, kama nilivyoanza kutangulia kusema na mwenyewe alikuwa hayupo, ninampa pole ana kazi nzito, wizara yake ina maeneo mengi sana na maeneo mengine kama tunavyozungumza yana manunda. Hii itampelekeshea pasipokuwa na umahiri mkubwa Mhe. Mwenyekiti, basi taasisi ile inaweza ikateketea. Kama nilivyozungumza Baraza la Manispaa ina watu wakorofi, watu walioshinda kazi katika maeneo mengine ndio wametupwa pale. Nasema pana mambo mengi sana na nishukuru kamati kwa kuyaona haya ambayo waliyoyaona na mengine sisi ambayo tunayaelewa, lakini ninasema bila ya kupigwa fagio la chuma katika Baraza la Manispaa basi hakuna liwalo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo na mimi niungane na wenzangu ya kuunga mkono ripoti ya Kamati Teule pamoja na maazimio yote ambayo yameandikwa na ninaimani kwamba kwa sababu tupo ndani ya mabadiliko ya kiutendaji na kishujaa basi pamoja na miezi mitatu aliyotoa sifikirii kwamba miezi itafika kwa kumfahamu Mhe. Waziri juu ya umahiri wake sana, basi nina imani ndani ya mwezi mmoja mabadiliko ndani ya Baraza la Manispaa yatapatikana. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*).

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu naomba na mimi nikushukuru kwa kunipa fursa hii kuchangia katika hoja hii ya taarifa ya Kamati Teule ya kuchunguza utendaji wa Baraza la Manispaa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, la pili na mimi naomba kwa dhati kabisa kuchukua fursa hii kuipongeza kamati, kwa kweli kwa kazi kubwa ambayo wamefanya na taarifa ambayo wameileta, lakini pia kwa mwenyekiti kutokana na uwasilishaji wake mahiri. Namna alivyowasilisha nadhani ni kielelezo kwamba walikusudia kwamba kila kitu ambacho kimeandikwa katika ripoti kiweze kufahamika kwa uwazi kabisa. Kwa hivyo mimi nawapongeza kwa dhati kabisa.

Lakini la pili niseme sababu ya kuwapongeza ni kwa sababu naomba nirejee tena kwamba hizi kazi za kamati za kudumu na Kamati Teule, kwa kweli inaisaidia sana serikali. Inasaidia kwa sababu kwanza zinasaidia kukuza uwazi, inatutanabahisha kwamba nchi yoyote haiwezi kuendeshwa kwa misingi tuliyokubaliana katika Katiba yetu bila ya kuwepo uwazi. Na taarifa hii ya kamati kwa kweli moja ambalo imesisitiza na moja ambalo imeliweka wazi ni kwamba haja ya kuwa na uwazi.

Mhe. Mwenyekiti, aliyekuwa ataipenda, aliyekuwa hatoipenda lakini mimi ninaamini moja ambalo limeimarika au litaimarika kutokana na ripoti hizi ni uwazi katika utendaji wa kazi za serikali. Lakini la pili ambalo naamini litaimarika ni uwajibikaji katika utendaji wa kazi za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu Wazungu wana msemo wanasema na mimi naomba niurudie na naurudia kila mara kwamba *failure is a process*. Yaani kule kufeli nako ni mchakato. Mhe. Ali Salum Haji kaeleza vizuri hapa, kwamba tulijenga Baraza la Manispaa katika misingi ambayo haikukusudia ufanisi na hili sio la leo wala sio la jana, maana yake kama uliwachukua wafanyakazi wote wa Bizanje ukawapeleka Manispaa. Nakumbuka kwamba Bizanje yenyewe iliwahi kuvunjwa na Mhe. Idrissa Abdulwakil kwa sababu ya vitimbi ambavyo vilikuwepo Bizanje na ikaundwa tena. Mimi nashukuru nilipata heshima ya kuwa Mjumbe wa mwanzo wa bodi ya Bizanje na Mwenyekiti wetu alikuwa Mhe. Ramadhan Haji Faki, na nilikuwa na wakongwe kina mzee Jamal Ramadhan Nassib pamoja na mzee Ibrahim Aman, hao niliwahi kufanyakazi nao.

Kwa hivyo, tulizijenga taasisi zetu nyingi huko tunakotoka katika misingi ambayo kusema kweli hatukuwa tukizingatia sana ufanisi. Kwa maana hiyo tulikuwa tunajenga mchakato wa kufeli, sasa haya tunayozungumza leo ni matokeo ya mchakato huo. Lakini hata tukitizama misingi ambayo tumejenga ya kisheria kwa mfano, kuna mambo mengi kama walivyosema Wajumbe ambayo yanahitaji kufanyiwa marekebisho. Serikali inao mpango huo, naamini Mhe. Waziri labda atakapokuja ataeleza hatua ambazo zinachukuliwa kuliimarisha. Lakini nasema ripoti hii imeimarisha uwajibikaji. Ukiipenda usiipende, lakini naamini kwamba mambo hayatokuwa tena kama yalivyokuwa baada ya ripoti ya Kamati hii Teule.

Pia imeimarisha utawala wa sheria. Kitu kimoja ambacho ripoti imekisisitiza ni kwamba taratibu zipo, kanuni zipo na sheria zipo lakini watu wameziacha na wanaamua kufanya wanayoyataka kwa sababu mbali mbali. Sasa tumefika hapa tulipofika kwa hivyo, sio tatizo ambalo ni la jana wala la juzi, lakini ni tatizo la muda mrefu na sasa nadhani aliyekuwa hajatanabahi anaweza akatanabahi kwamba sasa tumekusudia sote kufanya mabadiliko na kuleta uwajibikaji katika kuendesha nchi yetu. Hayo ndiyo yatakayosaidia katika kupata mafanikio na maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo labda niseme ya utangulizi. Mimi nataka kuzungumzia labda mambo mawili tu kuhusiana na hili. Jambo la kwanza, nianze na yale Mhe. Rashid Seif Suleiman kabla hajawa Waziri ilikuwa katika kipindi kile cha bajeti alikuwa anatuambia humu ndani kwamba mimi mara hii siipitishi bajeti ya Mawasiliano kama sijapata ahadi ya kutengenezwa taa za Uwanja wa Ndege wa Pemba, ndivyo alivyokuwa akituambia humu ndani. Alisema mara hii mtaimba na kufanya nini, lakini siipitishi bwana bajeti kabisa. Lakini ulipofika wakati wa bajeti yeye ndiye aliyesimama pale na kusimamia kupitishwa kwa bajeti, sikumbuki kama alitoa ahadi kuwa taa za Uwanja wa Ndege ataziweka au vipi.

Kwa hivyo, ninalotaka kusema tu ni kwamba hivi viti vya mbele havina hati miliki, na ndio maana Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak kasogea, Mhe. Mohammed Said Mohammed Mwakilishi wangu kasogea, ni kwa sababu huku mbele hakuna hati miliki ni utaratibu wa kutumikia nchi yetu. Sasa ninachofikiria mimi na ninadhani kwa kuwatanabahisha wenzangu ni kwamba tujenge misingi ya kuaminiana na kuwafanya wananchi watuamini kama hiki chombo kwa pamoja tuna nia ya dhati kabisa ya kuweza kuwatumikia. Lakini tukijenga *impression* ya kwamba huku mbele ndio watu hawana nia ya dhati ya kutumikia watu, mimi nadhani tutakuwa tunakosea, kwa sababu kesho utakuja huku huku au keshokutwa utakuja huku huku, mimi nadhani tuelekezane, tuambizane ili tuweze kuwatumikia wananchi na kuwajengea misingi ya kutuamini kama chombo, kwamba Baraza hili kama chombo na serikali yao kama chombo basi kwa dhati kabisa ina nia ya kuwatumikia.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili nalizungumzia katika mustakbali wa utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati. Mhe. Mwenyekiti, tunaposema utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati, yapo mengine ambayo yanahitaji kuyawekea utaratibu wake wa kuyatekeleza. Serikali isidhani kwamba ina pahala popote itakapokataa kutekeleza jambo ambalo

lina manufaa. Lakini katika kutekeleza yapo mambo mengi na ambayo wakati mwengine kwenye ripoti yenyewe inawezekana kuona pengine hatukuyaona na yanatokea hayo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nitoe mfano mdogo tu, kwenye ripoti yetu hii ambayo imeletwa mbele yetu. Katika ukurasa wa 64 kifungu cha 13 cha yale mapendekezo, yanasema kwamba Kamati inaliomba Baraza hili tukufu liitake serikali iyatekeleze mapendekezo ya ripoti hii kwa vitendo ndani ya miezi mitatu kutoka tarehe ya kuwasilishwa kwa ripoti hii, na hatimaye serikali iwasilishe taarifa ya utekelezaji wake ndani ya Baraza hili. Mimi sina tatizo lolote na hili kwa sababu huu ndio wajibu wa Baraza kutaka utekelezaji wa yale yaliyopendekeza na iarifiwe yametekelezwa vipi, ndani ya hiyo miezi mitatu.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, ukija kwenye ripoti hii katika mapendekezo haya haya, *item* nambari 5, inasema serikali ijenge soko kubwa ambalo litakidhi haja kwa wafanyabiashara wetu. Siamini kwamba Kamati inaitaka serikali ijenge soko kubwa ndani ya miezi mitatu, siamini hivyo kwa kweli.

Pia *item* nambari 12, sheria ya Baraza la Manispaa na kanuni za kudumu za Baraza hilo zifanyiwe mapitio ili ziendane na mazingira. Kwa hivyo, tukija baada ya miezi mitatu mkituambia sheria haijarekebishwa, kanuni hazijarekebishwa basi tunajua sote utaratibu wa kupitisha sheria. Sasa sidhani kama hilo limekusudiwa lifanywe ndani ya miezi mitatu, tukija jamani sheria tumeshairekebisha na soko limeshajengwa kubwa. Kwa hivyo, haya ndio mambo ambayo tunasema kwamba jamani katika kutekeleza yapo mambo ambayo ni vizuri tuje tuangalie kwamba suala hili serikali hebu tupe maelezo yenu mmetekeleza vipi, sisi tumelitekeleza hivi, kikwazo cha utekelezaji ni hiki, mmetuambia tujenge soko kubwa ndani ya miezi mitatu na bajeti ilikuwa imeshapitishwa, lakini maandalizi yetu ya kutekeleza hivi ni moja, mbili na tatu, nadhani hiyo ndio itakuwa njia sahihi ambayo tunatakiwa kwenda, kwa sababu hii ripoti yenyewe inaonesha kwamba kilichokusudiwa ni hicho, na ndivyo serikali ambavyo inafanya, maana tukizungumza serikali jamani sio Mhe. Mohammed Aboud wala Dk. Mwinyihaji, ni viongozi wetu wote wakuu na ndio wanaokaa wakatuelekeza namna gani ya kuyasimamia haya.

Kwa hivyo, kujenga *impression* kwa watu kuwa serikali imetia mpira kwapani, Mhe. Mwenyekiti, sidhani kama huu ni uwanja wa kubishana kwa tafsiri ya sheria. Huu ni uwanja wa Shura, kila mmoja anatoa rai yake ili tuwatumikie wananchi. Kama ingekuwa ni uwanja wa kujibishana kwa sheria basi mngetubakisha mimi na Mhe. Mshimba tu humu ndani. Lakini sio uwanja wa hili ni wa kujenga mustakbali wa kuwatumikia watu. Katika kufanya hilo, kanuni ya kwanza ya kuongoza watu ni busara. Sasa kama umeshajaza mawe uwanjani mpira huo utachezwa vipi, busara inahitaji tumalize hayo mawe ya barabarani kwanza kuyaondoa yaliyotupwa huko mitaani, halafu tena busara inahitaji kwamba tucheze katika uwanja ambao uko safi haukutupwa mawe.

Kwa hivyo, serikali ilichosema kwenye utekelezaji wa ripoti hii iliyozungumzwa ni kwamba tunaondoa hii ripoti, tukakae na hiyo Kamati Teule tusikilize mawazo yao, wapi na wapi. Sisi tunaona tumeleta maelezo ya kina ya utekelezaji kama hamjaridhika ni wajibu kutoridhika na lililotekelezwa, hiyo ni haki ya aliyewekwa kuwakilisha wananchi kuwatumikia. Kwa hivyo, sioni mimi hapo kama kuna ugomvi wala kuna tatizo, nasema la msingi ni kujenga kuaminiana.

Labda la pili nimalizie kuwa mimi siamini katika hili kama kuna lolote ambalo litaharibika, kwa sababu mimi naomba niwaambie kwa dhati kabisa, na mimi ni muumini wa mambo kwenda vizuri. Nina kumbukumbu ya hilo na wenzangu pia wengi humu ndani ni waumini wa hilo. Mimi nashukuru kwamba hizi ripoti zikija sasa zinaonekana kuwa wengine sio kwamba ni wakorofi, ndio misingi ya kuendesha nchi inavyotakiwa, ufuate sheria, ufuate taratibu na ufuate uwajibikaji. Kwa hivyo, kwangu mimi binafsi na naamini na kwa wenzangu vile vile na kwa viongozi wetu wakuu wote, hizi ripoti zinasaidia kueleza na kutangaza ile dhamira ambayo na wao wenyewe wanayo. Kwa hivyo, kwenye hili mimi sioni kama kuna tatizo lolote, ni suala la kukubaliana ni namna gani tutalitekeleza.

Lakini la pili nimalizie lile ambalo alitoa rai hapa Mhe. Omar Ali Shehe, nalo liko katika msingi ule ule nasema wa kuaminiana. Yeye alisema kuwa hii ripoti imekuwaje tena irudi iende kwenye vyombo vya kuchunguza pale ambapo panatakiwa kuchukuliwa hatua za kisheria. Lakini jamani huo ndio utaratibu tuliouweka sisi wenyewe, lakini hata kama ingekuwa hatukuweka utaratibu huo, hii ripoti kwa kweli ni pahala pazuri kwa mpelelezi yeyote au anayetaka kufungua mashtaka yoyote, hii itakuwa kama ndio kitabu chake cha kumuongoza. Lakini hiki huwezi kwenda kukitupa pale mahakakani, ukasema mimi nafungua mashtaka huyu mtu kaiba na ushahidi wangu ndio huu hapa. Hatuendi hivyo, kwa sababu humu, kwa mfano vielelezo vyote vilivyotolewa inabidi yapatikane maelezo ya

hao waliokuwa navyo na hao wengine watakuja mahakamani kuja kuwa mashahidi. Lakini katika kila kosa la jinai tunasema kuna viini vya kosa. Sasa kila kiini uhakikishe kwamba je kwa ushahidi huu nitaweza kuvithibitisha.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru nchi hii imenipa heshima ya kuwa Mkurugenzi wa Mashtaka wa mwanzo. Kuna wakati tulikuwa na kesi ya fumanizi kutoka Jimbo la Mhe. Ali Juma Shamuhuna. Sasa polisi wamefanya uchunguzi na sisi tukaona kuwa ushahidi ni mzuri kweli kweli tukaenda nao mahakamani, lakini mshtakiwa ana haki ya kuwa na Wakili. Moja katika kiini cha kosa la fumanizi ni kwamba lazima uthibitishe kwamba huyo mwanamme alijua kama huyu mwanamke ni mke wa watu au alipewa ruhusa na huyo mume. Sasa ushahidi wote ule uliokuwemo tulisahau kipengele hicho tu kuthibitisha kwamba huyu mwanamme alijua kama huyo mwanamke ni mke wa mtu. Kwa hivyo, katika mazingira hayo kila mtu atalalamika, kwamba aah! Ushahidi wote ule kakamatwa ndani. Ndio lakini hakuna ushahidi wa kuthibitisha kuwa huyu mwanamme alijua kuwa huyu mwanamke ni mke wa mtu. Pengine kadanganywa, bibi kasema mimi sina mume na yule mwanamme ni mgeni na yeye hakufuata ile busara ya kule kwetu. Maana kule kwetu wanasema hata akiwa mjane, *'mjane mjiningwa ni mkengwa*'. Ikiwa mjane katika mji wa watu ni mke wa watu.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hayo ndio matatizo ya tunaposema kuchukua hatua za kisheria kunahitaji kufanywe uchunguzi wa kina, kwa sababu kuna *interest* zake kama hizo na ndio maana jana nilitoa mfano hapa. Tuliunda Tume ya *Spice Islander* na iliongozwa na Jaji wa Mahakama Kuu, Katibu wake alikuwa ni *Prosecutor* mzoefu. Mimi mpaka naondoka pale ndio *in charge* wa *prosecutor* mahakama za mikoa, miongoni mwa wajumbe ni mwanasheria mzoefu. Lakini baadhi ya makosa walopendekeza zichukuliwe hatua za kisheria ulipofanyika upelelezi, ikagundulikana polisi na Mkurugenzi wa Mashtaka wakaona kwamba kweli katika hili jamani kuna vipengele hivi na hivi kule hatuwezi kumshtaki kwa hili, kwa sababu haya yamekosekana ambayo Tume haikuyaona.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, sio suala la kwamba Tume au Baraza limedharauliwa au Wajumbe wamedharauliwa. Lakini ndio utaratibu wenyewe na bahati nzuri hata hii sheria yetu nambari 4 ya mwaka 2007 yenyewe hii sheria inasema, ili kumshtaki mtu chini ya kifungu cha 42 chini ya sheria hii ni lazima upate idhini ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Sasa utaachaje kumrudishia tena Mkurugenzi wa Mashtaka, lakini hii Katiba ndio tuliompa Mkurugenzi wa Mashtaka mamlaka ya yeye kushtaki, na kushtaki maana yake ni kuamua kwamba je, hapa pana ushahidi wa kutosha na iwe kwa uadilifu, isiwe uadilifu ni kipimo cha kitu chengine. Lakini hatuwezi tena tukasema kwamba Baraza lichukue mamlaka ya ku-*exercise prosecutorial discretions* yaani ya kuamua kwamba huyu mtu ashtakiwe, itakuwa imefanya kazi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, tumuachie yeye. Huo ndio utaratibu tuliokubaliana katika nchi yetu, na nchi yetu ndivyo tulivyokubaliana tuiendeshe hivyo.
Mhe. Mwenyekiti, naomba sana niwasihi wenzangu tusishawishike kuchukua mamlaka ya vyombo ambavyo tumeviunda kwa kuviamini, tumeviweka kwa kuviamini na tukaviweka ndani ya Katiba yetu. Hapa hakuna mtu ambaye anakusudia kumlinda mtu wala hakuna mtu ambaye anakusudia kumtetea mtu. Lakini utaratibu ndio tunaousisitiza kwamba ufuatwe, sheria ifuatwe na tumeziweka wenyewe. Kwa hivyo, mimi ninachoomba tena niwaombe sana wenzangu Waheshimiwa Wajumbe kwamba tujenge misingi ya kuaminiana ndipo tutakapoweza kuwatumikia watu kwa ufanisi na kwa maelewano na wakapata faida ya yale ambayo wanayategemea kutoka katika chombo hiki cha Baraza la Wawakilishi.

Baada ya kusema hayo Mhe Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia taarifa hii ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi iliyoundwa kuchunguza utendaji wa Baraza la Manispaa Zanzibar.

Aidha, nimpongeze sana Mwenyekiti kwa uwasilishaji mzuri wa taarifa hii kwa umakini, taarifa ndefu lakini ameimudu kuiwasilisha vizuri. Pia niwapongeze Wajumbe wake na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wale wote ambao wameichangia taarifa hii.

Vile vile nimpongeze sana Waziri anayesimamia tawala za mikoa na vikosi vya SMZ Dk. Mwinyihaji Makame, kwa kazi kubwa anayoifanya ya kutafuta mabadiliko katika kuimarisha manispaa zetu, halmashauri zetu na kwa jumla utaratibu mzima wa tawala za mikoa. Anajitahidi kufanya kazi kwa bidii sana, ni kiongozi makini, kiongozi mvumilivu, kiongozi anayestahamili mengi, na mimi nampongeza sana na aendelee kushika uzi huo huo ili tufanye mabadiliko katika kuendesha gurudumu letu la nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuanza kutoa mchango wangu ninukuu kipengele cha Katiba kifungu cha 5(a) kama kilivyozungumzwa sana na Wajumbe wa Baraza jana. Nataka nivisome cha kwanza, cha pili na cha tatu. Katiba inasema hivi kuhusu mgawanyo wa madaraka. Zanzibar itafuata mfumo wa mgawanyo wa madaraka kati ya mamlaka tatu. Mamlaka ya utendaji, mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma na mamlaka ya kutekeleza utoaji wa haki.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu nambari mbili kinasema, mamlaka ya utendaji ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma ni Baraza la Wawakilishi na mamlaka ya kutekeleza utoaji wa haki ni mahakama.

Kifungu nambari tatu kinasema, hakuna mamlaka itakayoingilia mamlaka nyengine isipokuwa kama na kwa kadiri itakavyoelekezwa katika Katiba hii. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, Katiba imetufungulia vizuri, kila mmoja imempa mamlaka yake kwa ajili ya kutekeleza wajibu wetu wa kuwahudumia wananchi wetu na sisi sote nia na madhumuni ni kuwatumikia wananchi, naamini kwenye hili sote hatuhitilafiani. Kwa hivyo, wajibu wetu Mhe. Mwenyekiti, kila mmoja anapotoa mchango wake hasa unaohusu mamlaka inayomgusa basi huyo huwa anafanya wajibu wake, na huwa hadharau chombo chengine au kudhalilisha chombo chengine, au kukataa maamuzi ya chombo chengine. Lakini hufanya wajibu wake kwa mujibu wa Katiba, na hivyo ndivyo tulivyoelekezwa ili tufanye vizuri kwa manufaa ya watu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, leo ilipotoka michango baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe walitutaka Mawaziri nao wachangie kwenye hoja hii, wakiwa na maana yatakuwa ndio maamuzi ya serikali. Ni kweli sisi Mawaziri na kwa upande mwengine ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na tunayo haki ya kuchangia, lakini michango yetu hapa inawezekana ikawa ni kutoa ufafanuzi wa jambo ama kuelezea jambo linalogusa serikali. Lakini hapo tunapotoa ufafanuzi bado tunafungwa na utaratibu na Katiba na sheria kwamba ni watu wa upande wa serikali. Kwa hivyo, maamuzi ya serikali sisi kama Mawaziri humu ndani tunapaswa kuyatetea, lakini tunapotoa hoja zetu hapa bado tunafungwa na kwenda kufanya tena maamuzi yanayopaswa kufanywa na serikali kutokana na ushauri unaotolewa na Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, ukitizama taarifa zote hizi zinasema tunapendekeza kwa serikali. Kwa hivyo yale yanakuwa ni mapendekezo na baadae serikali inayafanyia kazi kwa nia njema kabisa ya kutenda haki kwa wananchi wetu. Kwa hivyo, mapendekezo yote ambayo yanatolewa na Baraza hili tukufu huwa tunayapokea na kuyafanyia kazi na msingi wetu wa kuyafanyia kazi ni kufuata misingi ya Katiba, Sheria na haki. Vile vile kuhakikisha kwamba tunaheshimu utamaduni wa nchi yetu na busara inatumika ili kuhakikisha haki, umoja na amani wa nchi yetu unaendelezwa.

Kwa hivyo, maamuzi yanayofanywa yanafanywa kwa kutumia busara kubwa na kwa mashirikiano makubwa ya serikali ili kuhakikisha nchi yetu inabakia katika hali ya salama na amani. Kwa hivyo, naomba Waheshimiwa watuelewe kwamba tunaposema tunayachukua mambo kwenda kuyafanyia kazi na serikali, basi yanafanyiwa kazi, na serikali ina vyombo vingi baada ya hapo, ina taasisi nyingi ambazo pia huulizwa ili kuleta majibu sasa hivi, ndio maana hufikia uamuzi wa hoja zile. Lakini kwa kiasi kikubwa hoja zetu huwa hazitofautiani sana na hoja ambazo Baraza hili tukufu inazozitoa.

Ninasema hatutofautiani sana kwa sababu tunaamini kabisa kuwa Baraza hili linafanya kazi nzuri, linaibua mambo mengi ambayo serikali inayaunga mkono. Serikali yetu haina nia hata kidogo ya kulinda maovu. Serikali yetu nia yake ni kupambana na maovu kwa nguvu zote, kuondoa maovu kwa nguvu zote, wala haina nia ya kuchakachua taarifa zinazokuja, wala haina nia ya kukataa mageuzi, bali serikali yetu ina nia ya kuleta mageuzi. Ndio maana unaona mara nyingi Kiongozi wetu mkuu, Rais wetu mpendwa anatuambia tusifanye kazi kwa mazoea basi sasa tufanye kazi ili tuhakikishe ufanisi na tija unapatikana.

Kwa hivyo, katika serikali isiwepo dhana hata kidogo kwamba tuna nia ya kuchakachua taarifa, kuna nia ya kuwalinda wanaofanya makosa, hatutaki mageuzi ama ni dhaifu katika utekelezaji. Mambo hayo ndani ya serikali hayapo, na nia yetu ni kushirikiana na chombo hiki, yale yote yanayokuja tunayafanyia kazi vizuri na kuhakikisha kwamba haki inatendeka bila ya upendeleo wa upande wowote kama huo ndio wajibu wetu.

Kwa hivyo, nataka nilihakikishie Baraza hili tukufu kwamba yote yanayofanyika yanafanyika kwa misingi ya kufuata taratibu zilizowekwa na sheria na Katiba yetu.

Vile vile kubwa hapa ambalo limejitokeza kutokana na taarifa iliyowasilishwa jana ya serikali kuhusu Kamati Teule, tuliambiwa kwamba serikali imetia mpira kwapani. *(Makofi)*

Kwa kweli serikali hatukutia mpira kwapani, tulieleza wazi wazi kwamba tulileta maamuzi ya serikali kifungu kwa kifungu na tukayasoma mbele ya Baraza hili tukufu, na maana yake utaratibu wa siku hizi kuna vyombo vya habari hivi na vinatoa habari umma wote unasikia na unapima. Kwa hivyo, hakuna la kificho wala la kupendelea, isipokuwa tumeyaleta pale baada ya kuyapitia na kuyafanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, ndipo tuliposema kwamba Baraza hili tukufu lilionesha baadhi ya vifungu hawakuridhika navyo. Lakini kwa sababu jana hatukuoneshwa kifungu kipi na kipi na michango yote ilikuwa ni michango ya jumla.

Kwa maana hiyo, tukasema serikali iko tayari kukaa tena na Wajumbe wale wa Kamati Teule, ili kupitia kifungu baada ya kifungu kwa lengo la kufafanua vizuri na wenzetu watuelewe, na pale watakapoona kuna sehemu ambayo tumeamua kinyume na utaratibu, sheria, Katiba ama hatukufuata busara, basi vizuri kuelekezana, hivyo tutatoa nafasi hii ili tuelekezane na sisi katika serikali tuko tayari wakati wowote.

Kwa hivyo, hapo mbele tuna Sikukuu, mara baada ya sikukuu tutawasiliana na Ofisi ya Baraza la Wawakilishi hapa tupange, tena ninavyoona ni vizuri kabisa tutafute mahala penye ukimya tukae pamoja na Wajumbe tuende kipengele baada ya kipengele na ufafanuzi tutoe, kwenye maswali tuulizwe, ili tuelewane vizuri.

Kwa kweli nia ya serikali yetu ni kufanya kazi kwa uadilifu, kuwatumikia wananchi, kuondoa maovu na kuhakikisha kwamba tunafanya kazi kwa bidii na nguvu zote na wala hakuna haja ya kuchakachua jambo lolote, isipokuwa nia yetu ni kuwatumikia wananchi. Kwa maana hiyo, ninawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe watuelewe kwamba nia yetu ni safi na tunafanya kazi kwa madhumuni ya kuhakikisha kuwa tunapata maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, serikali inajiamini sana na maamuzi yake, imeona maamuzi yake ni sahihi ambayo yamefanyiwa kazi kwa kina ndio yakafikia pale. Kwa hiyo, tunazo hoja za kutoa pale ambapo tutaulizwa, na pia pale ambapo panaonekana kwamba pametokea kasoro basi tutaeleza kasoro yenyewe ikoje. Hii ni serikali sikivu na wala haina matatizo yoyote ya kutekeleza wajibu ambao utawaletea manufaa wananchi wetu.

Baada ya kusema hayo, nataka niseme kwamba tumeisikia vizuri serikali taarifa hii ya Kamati Teule na ninaamini Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ataeleza zaidi, lakini kwa upande wetu kama serikali taarifa hii tunaipokea na tunakwenda kuifanyia kazi na majibu kupitia Waziri muhusika atayatoa vizuri, kwa sababu naamini ni Waziri makini, muadilifu, mwenye uwezo wa kuyafanyia kazi haya ambayo yametolewa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo nashukuru na ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kuna kitu naomba kukuombeni sifungwi na Kanuni kuweza kumruhusu Mjumbe yeyote kuchangia baada ya Mhe. Waziri kusimama. Lakini utaratibu wetu tuliojiwekea ni kwamba tunaanza kuchangia sisi *backbenchers* na baadaye tukianza kuwapa Mawaziri iwe tena tunaelekea kwenda kufanya majumuisho ya hoja yetu.

Lakini pamoja na utaratibu huo ningeliomba wale ambao walioleta *notes* hivi sasa, basi tuheshimu ule utaratibu ambao tunaokwenda nao na tumuache Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aendelee na halafu tumuite Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Kuchunguza Utendaji wa Baraza la Manispaa) kwa ajili ya kumalizia.

Vile vile tujitahidi kufuata zile taratibu kwamba kila anayetaka kuchangia basi afuate taratibu za kuleta maombi yake mbele, ili yaweze kuonekanwa na aweze kupewa nafasi. Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, tuendelee.

Mhe. Saleh Nassor Juma, kuhusu utaratibu.

UTARATIBU

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, nadhani mazoea katika Baraza hili si vyema kuyafuata, kwa sababu tumejitungia Kanuni zetu. Kwa hivyo, mimi nafikiri ni vyema tukafuata Kanuni zaidi kuliko uzoefu wa kuendesha shughuli. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, nadhani kama kuna wachangiaji basi waruhusiwe kuchangia kwa mujibu wa Kanuni ya 65, hivyo tuache uzoefu tuende kwenye Kanuni moja kwa moja, na kinyume na hivyo itakuwa huwatendei haki Mhe. Mwenyekiti Wajumbe wako, ambapo wako wengi wanaotaka kuchangia hii hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza Hassan Juma, kuhusu utaratibu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nizungumzie kuhusu utaratibu. Mhe. Mwenyekiti, hii tunayoijadili hapa ni ripoti ya Kamati Teule, na ripoti hii inatakiwa itiwe nyama aidha ikosolewe, iboreshwe au ifanywe jambo jengine.

Sasa Wajumbe waliochangia ni wachache sana kwa upande wa *backbenchers*, na ripoti hii serikali ndio yale mapendekezo yetu tutakayoyatoa, ndio serikali itakwenda kuangalia ni maeneo gani, licha ya kwamba tunabishana kwa mambo madogo, lakini bado kuna mambo ambayo serikali imeanza kuyashughulikia. Kwa hivyo, kama wapo Waheshimiwa ambao wanataka kuchangia ripoti hii na hawajapewa nafasi, basi malalamiko na manung'uniko yataendelea kuwepo. *(Makofi)*
Mhe. Mwenyekiti, nadhani kwa sababu hata Mawaziri kama umewasikiliza vizuri wale waliozungumza Mhe. Mwanasheria Mkuu pamoja na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais hawakuingia kwenye hii ripoti ya leo hata kidogo, wao bado wamejaribu kuweka sawa yale malalamiko ya ripoti iliyopita. Kwa hivyo, bado ripoti hii inahitaji kutiliwa nyama. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nafikiri ripoti hii tusiibane, kwa sababu imetoa mapendekezo mazito. Kwa maana hiyo, inawezekana mapendekezo haya pengine Waheshimiwa Wajumbe wengine wakasema ah! Mapendekezo sisi wengine haikuwa busara. Mhe. Mwenyekiti, nafikiri muda bado tunao na kama sikosei muda wa ripoti hii ni siku mbili. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, nafikiri ni vyema tukawapa nafasi Waheshimiwa Wajumbe waendelee kutoa michango yao, na katika kutoa michango ni kuzidi kuiboresha kwa kila mmoja. Kwa mfano, Mhe. Ali Salum Haji alizungumza vizuri sana pale, alizungumzia mpaka uzoefu wake wa Baraza la Manispaa na matatizo tangu huko nyuma, hivyo tumepata kujifunza mambo mengi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri hii ripoti wala haina suala la kubisha tena ripoti hii ina mambo machache sana, ambapo inahitaji kuboreshwa. Lakini ili hii ripoti iwe ya Baraza basi nadhani waachiwe Wajumbe wengi wachangie, ili hii ripoti kweli iwe ya Baraza na wala isiwe ya watu wachache. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, kuhusu utaratibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema awali kwamba katika Baraza kuna mgawanyo wa madaraka, kuna serikali na Wajumbe wa Baraza. Kwa msingi huo sisi tunapaswa kutoa ufafanuzi na haya tuliyoyatolea ufafanuzi leo yamezungumzwa leo katika Baraza hili kwenye ripoti hii.

Kwa hivyo, hata kama yaliyozungumzwa jana basi tulizungumza jana yamekwisha, lakini leo yamezungumzwa hapa. Kwa mfano, amezungumza Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Hamza Hassan Juma, kwa hiyo tumeyatolea ufafanuzi na kueleza kama serikali, kwa ajili ya kuonesha *commitment*, utayari pamoja na uwajibikaji wa serikali. Kwa maana hiyo, hatuwezi kunyamaza kimya wakati serikali inafanya kazi nzuri ya kutekeleza maamuzi mbali mbali ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, ahsante. Waheshimiwa Wajumbe, nafikiri mwanzo niliposema nilifahamika kwamba sifungwi na Kanuni isipokuwa ni busara kuweza kuona Wajumbe wanachangia mwanzo na baadaye Waheshimiwa Mawaziri wanasimama kwa sababu ya ufafanuzi.

Kwa msingi huo wale waliobakia ambao wamekuja kuomba dakika za majeruhi ni Mhe. Saleh Nassor Juma. Sasa nadhani tutumie hekima nyengine ya busara tumuombe Mhe. Saleh Nassor Juma hizo dakika tano alizoomba azungumze, na atakapomaliza aendelee Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ili tuweze kufikia pazuri na huo ndio utaratibu wetu.

Mhe. Saleh Nassor Juma, tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Omar Ali Shehe, kuhusu utaratibu.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu Kanuni ya 64(1)

Kanuni ya 64(1) inaeleza hivi:-

> "Endapo bado kuna Wajumbe wanapenda kuzungumza katika jambo lilioko katika mjadala, utaratibu utakaotumika kufunga mjadala ni kutolewa hoja itakayoamuliwa na walio wengi".

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa hivi sasa tuko kwenye mjadala na bado wapo Wajumbe walio wengi, hoja hii ni ya siku mbili. Mwenyekiti, nadhani tupe nafasi Wajumbe, ili tutumie haki yetu kwa ajili ya kujadili hoja hii, na baadaye serikali nayo ije ichukue nafasi yake katika kueleza mbele ya Baraza hili. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, suala hili hata tukitaka kufunga mjadala, kwa sababu kuna Wajumbe lazima itolewe hoja na lazima iungwe mkono. Kwa hivyo, hatuwezi kuufunga mjadala katika utaratibu wa kawaida.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, kuhusu utaratibu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe wako walizungumzia kuhusu suala la utaratibu na kufuata Kanuni, ni kweli kwamba Mjumbe yeyote anayo haki ya kuzungumza na kama mjadala kama alivyosema kwa mujibu wa kifungu cha 65 inaweza kutolewa hoja.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, naomba Wajumbe wako wajue kwamba utaratibu wetu na uliokubalika ni kwamba Mjumbe ambaye anataka kuchangia analeta kikaratasi, sasa pale ambapo huna kikaratasi unawajibika wewe kufunga mjadala. Sasa ukiacha Baraza lako kila mtu anapotaka kunyanyuka mara kwa mara baada ya kufunga au huna tena kikaratasi hiv+yo itakuwa si vizuri.

Kwa hivyo, mimi naomba tu kwamba baada ya kutoa *note* hiyo umruhusu Mjumbe azungumze, lakini tufuate utaratibu ambao tunao wa siku zote. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, ahsante. Pamoja na maelekezo ya pande zote mbili naomba mkisaidie kiti tumuache Mhe. Saleh Nassor Juma kwa dakika zake alizokusudia na baadaye Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Saleh Nassor Juma, tuendelee.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani kabla sijaendelea tungejikita zaidi kwenye Kanuni. Mhe. Mwenyekiti, mjadala ni wa siku mbili, na wewe na wala sitaki kusema Mhe. Mwenyekiti kwa heshima na taadhima kwamba ulikurupuka tu, aa! Hukukurupuka, lakini inaonekana ulifanya haraka kuwapa Mawaziri.
Kwa kweli utaratibu tulivyozoea hapa kwamba mjadala huwa Spika au Mwenyekiti ananadi hasa kwamba mjadala unaendelea ikiwa hata hakuna *notes*, yaani Spika anazunguka. Sasa leo Mhe. Mwenyekiti ukitufanyia hivi hukutufanyia haki, kwa sababu kuna watu kadhaa wameshazoea kwamba mjadala unaendelea. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kama ni dakika tano nizungumze mimi basi naomba nikae Mhe. Mwenyekiti na ni-*reserve* mawazo yangu kwa hili kwa sababu itakuwa hukututendea haki Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, mimi najua kwamba yaliyokuwa yamezungumzwa umeyafurahia na ndio maana ukawa umeyaunga mkono na sasa unamuachia Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aendelee na taratibu nyengine.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, tuendelee.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kupata wasaa huu wa kuchangia ripoti hii ya taarifa ya Kamati Teule ya Baraza, iliyoundwa kuchunguza utendaji wa Baraza la Manispaa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli ripoti imeandikika na mimi naipongeza sana Kamati. Vile vile niseme nawapongeza kwa nini, kwamba kwa kufanya kazi ya ziada kwenda nitatumia neno moja vichochoroni, yaani kuingia ndani kabisa kama zile hadidu rejea zao zilivyoagiza, kwa hiyo naipongeza sana. *(Makofi)*

Kwa kweli Waheshimiwa Wajumbe wengi wamempongeza Mhe. Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wengine, na wala si ajabu ile Kamati ukiitizama kweli hao Wajumbe waliowekwa humo wote wana sifa nzito. *(Makofi)*

Kwanza kuna mwenyewe Mhe. Salmin Awadh Salmin, ambaye ni Mwenyekiti mbali ya sifa zake nyengine lakini alisema mwenyewe kuwa aliwahi kuwa Diwani pamoja na uzoefu wake wa muda mrefu wa kulijua Baraza la Manispaa nafikiri imesaidia sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi lazima niseme ukweli kwamba mimi ni mgeni kidogo wa Baraza la Manispaa, haidhuru ni mwenyewe wa Mkoa wa Mjini Magharibi, lakini kupata uzoefu mkubwa sana wa Mhe. Salmin Awadh Salmin. Vile vile na Mwanasheria Mhe. Ismail Jussa Ladhu, ambaye ni mtu wa Mji Mkongwe na siku zote huniuliza maswali ya Mji Mkongwe. Mhe. Mwenyekiti, utakumbuka wakati mwengine huwa tunabishana.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, mnaotoka nje Mhe. Mwenyekiti hana muda mrefu katika kuhitimisha hoja hii. Mhe. Waziri tuendelee.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nilitaka kusisitiza tu au kuonesha kwamba Kamati imefanya kazi nzuri sana na tunaipongeza, na lazima niseme na wenzangu wengi walionitangulia wamesema kwamba huu ndio ukweli walioyaona wao. Kwa imani yangu mengi kabisa ni ukweli, kwa sababu si kitu cha mtu mmoja, wawili au watatu, lakini ni watu watano pamoja na makatibu wao wawili. *(Makofi)*

Sasa sisi hatuendi tena kuchunguza aa! Kwa hivyo, sisi tutakwenda kuyafanyia kazi, kwanza tunayapokea yale yote mapendekezo, halafu tunaingia ndani tuone vipi tunaweza kuyatekeleza kwa lengo moja tu la kuboresha au kufanya utendaji wetu uwe mzuri zaidi ndani ya Baraza la Manispaa.
Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi cha pili au niseme kikao cha pili cha Baraza maswali yote ninayopokea ni kuhusu Baraza la Manispaa, na wala sijapata maswali mengi. Hali hii inaonesha wazi vipi Waheshimiwa Wajumbe wanavyokereketwa au wanavyofuatilia na wanavyoona vipi Baraza la Manispaa liwe kulinganisha na miji mingine.

Kwa kweli nakiri kwamba kuna mapungufu tena makubwa, na mimi mara nyingi huwa ninakiri zaidi tuende kwenye vitendea kazi, kwani tuna mapungufu makubwa ya vitendea kazi. Lakini tumeoneshwa kwenye ripoti hii kumbe mbali ya vitendea kazi, lakini taratibu za utendaji wetu, sheria hatuzifuati, hatusimamii, na hayo yote yameoneshwa kwa uwazi humu.

Mhe. Mwenyekiti, nawahakikishia Waheshimiwa Wajumbe kwamba hayo waliyoyabaini nakiri yapo na wala sikatai, na wameniambia tulisafishe Baraza, tuweke sawa mambo, tuboreshe mambo. Kwa hivyo, tutaichukua ripoti hii na itakuwa kama ndio *working document* yetu au ni taarifa ya kuifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, Sera za Tawala za Mikoa. Waheshimiwa Wajumbe, wengi waliochangia walisema sababu moja wapo ya kutofanya vizuri Baraza la Manispaa na Mabaraza yetu ya Miji ni matatizo ya kutokuwa na Sera za Tawala za Mikoa. Nakiri ni kweli, lakini serikali imeliona hilo na tayari sera serikalini tumeshaipitisha, ilikuwa *weekend* ya tarehe 19/10/2012 ilikuwa tufanye semina kwa bahati mbaya kulikuwa na dharura nzito ambazo baadhi ya Wajumbe sisi tulikuwa kwenye uchaguzi kwa hiyo semina ile tuliakhirisha.

Kwa hivyo, naomba kukuhakikishia Mhe. Mwenyekiti pamoja na Waheshimiwa Wajumbe kwamba bado mnatudai deni la Sera hiyo ya Tawala za Mikoa tutakuja kuiwasilisha, ili tupate michango zaidi. Sasa baada ya serikali kuikubali sera yetu tuko kwenye hatua ya mbele sasa kwamba tunaanza kuandaa sheria, ambazo zitatupa nguvu kutekeleza na kuyarekebisha haya mapungufu mengi ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameyaona.

Lakini mtazamo wetu wa serikali ambao ndio wa kisasa uliopo katika hizo Serikali za Mitaa ni kwa kutumia utaratibu unaoitwa kwa kitaalamu. *Decentralization by Devolution* (*D byD*).

Kwa ufupi tunachosema tunataka kuyateremsha maamuzi wilayani au katika ngazi ya chini, na isiwe kama sasa tunapanga serikali kuu na halafu sisi wenyewe serikali kuu tunatekeleza na wale walengwa wananchi wa chini wao tunawaambia tekelezeni aa! Lengo letu ni kwamba mipango ile ipangwe chini, halafu watekelezaji ndio wenyewe tutatafuta fedha, tutasimamia mipango yetu na hilo ndilo lengo letu.
Mhe. Mwenyekiti, tatizo kubwa sana ni kwamba haya mambo yanahitaji matayarisho na hasa wataalamu, sasa hao wachache tulionao tutajipanga tuone kuwa tunawateremsha wilayani wataalamu wetu. Kwa mfano, tunazo wizara kama vile kilimo, elimu, wanawake na watoto, mifugo ambao wanao wataalamu walio chini, lakini wizara nyengine bado hatuna wataalamu hao.

Sasa lengo pamoja na mtazamo wetu Mhe. Mwenyekiti, ni kuona kwamba hizo Sera za Tawala za Mikoa itakuja au imeshachukua mfumo huo. Lakini sheria zetu ni kuwezesha Tawala za Mikoa zijiendeshe wenyewe na maamuzi yatakuwa yao wenyewe.

Kwa mfano, walisema Waheshimiwa Wajumbe masula ya usafishaji wa mji, *clinic* ndogo ndogo zilizomo, skuli za msingi, miji mingi mambo kama yale yanaendeshwa, masuala ya zimamoto, pia wanazo *ambulance* zao ni kama serikali kamili zilizoko kule. Kwa hiyo, sisi mtazamo wetu wa muda mrefu ni huo, lakini kwa sasa bado hatujafika huko na tunaelekea huko.

Mhe. Mwenyekiti, hili nataka kuwaambia Waheshimiwa Wajumbe kwamba hatukulisahau. Kwa hivyo, sisi tumeshaanza kupanga na tunaelekea huko. Kwa habati nzuri niseme Mhe. Mwenyekiti tulihisi labda kumbe tumeachwa, lakini hatujaachwa nyuma isipokuwa tumechelewa kidogo.

Kwa kweli hata wenzetu katika Mikutano ya Jumuia ya Afrika ya Mashariki tulifanya mkutano mmoja juzi wa *D by D*, na tuliona matatizo tuliyonayo kumbe tuna-*share* na wenzetu, kumbe vile na wenzetu wanayo matatizo ambayo yanalinga kama haya.

Vile vile juzi nakumbuka nilisema wengine wanafika kutumia nguvu, yaani vikosi vyao kama vile *FFU* na vyengine kwa ajili ya kuwaondoa wafanyabiashara mjini kwa ajili ya kuweka usafi kwa nguvu. Sasa sisi tukasema aa! Kwanza tuwaelimishe watu wetu wafahamu, na ikibidi tena kutumia vyombo kama hivyo na hiyo itakuwa ni hatua ya mwisho kabisa, hilo naomba nilisisitize Mhe. Mwenyekiti.

Jambo jengine ambalo naomba nilisisitize ni suala la kubadilika. Mhe. Mwenyekiti, sisi katika Serikali Kuu tumejipanga kubadilika na hili si jipya kulirejea mimi. Kwa kweli Mhe. Rais mara nyingi sana ametueleza watendaji sote mpaka mawaziri, yaani viongozi ambao tumo serikali kama mtu hawezi kwenda na *speed* yetu basi apumzike mwenyewe na wala asingoje kuambiwa bwana wewe pumzika, sasa hiyo ni changamoto nzuri sana tumepewa.

Mhe. Mwenyekiti, mbali ya hayo tumefanyiwa Semina Elekezi serikali nzima kuanzia Wakurugenzi, watendaji wakuu wale mpaka Mawaziri, yaani tumekaa mpaka tunaondoka saa 8 za usiku, kwa sababu zile *topics* zilizokusudiwa tupate *dose* zote, kama vile uendeshaji, ufuataji wa sheria, masuala ya ardhi na matumizi yake, na tulipata watoa mada wazuri tena wametuelimisha.

Lakini serikali ikaona kwa Tawala za Mikoa wapate *dose* yao ya peke yake, kwa hiyo na wao tukafanya Semina Elekezi mbili, moja Unguja na nyengine Pemba, ambapo ya Unguja tulifanya mwezi wa Juni na tukaenda Pemba juzi mwezi wa Septemba.

Madhumuni ya semina hizo ilikuwa pia kuwaelimisha juu ya taratibu za uendeshaji hizo Tawala za Mikoa, jinsi ya kufuata sheria, matumizi ya ardhi, nini wajibu wao, wajibu wa Sheha, Diwani, Katibu wa Halmashauri, Mkurugenzi wa Manispaa na hata wajibu wa Meya upo ni upi.

Semina hizo Mhe. Mwenyekiti kwa kweli zilifanikiwa sana, kwa sababu tulikaa pale mpaka saa 8:30 na sio suala la kukesha aa! Kwa kweli ni suala la *interaction*, yale maswali ambayo Wajumbe waliyokuwa wakiuliza na kupata kufahamu ama uelewa. Mhe. Mwenyekiti, haya naomba kusisitiza kwamba naelezea yale madhumuni ya serikali kutaka kubadilika.

Mhe. Mwenyekiti, hii michango ambayo Waheshimiwa Wajumbe ambayo mumetupa pamoja na maelekezo aliomo kwenye ripoti nafikiri yote yanalenga huko katika kubadilika.

Baraza la Manispaa siku zote ndio tunasema kioo chetu, mgeni yeyote akija akiona mji tu pale na wengine mnanitania mnaandika kwenye maswali anabana pua mji si msafi Marikiti mnanielekeza pale. Sasa haya yote mimi huwa ninayachukua na kuyafanyia kazi, yaani lile swali mnaponiuliza, basi natayarisha jawabu lakini na watendaji na wao nawapata. Lakini kuna matatizo ya kiutendaji, ambayo hayo kama wizara na serikali tunayafanyia kazi.

Sasa ninachotaka kusema Mhe. Mwenyekiti, sisi kama Mawaziri au hasa kwa hapa *very specific* kwa Wizara ya Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwamba hatuna malengo au azma ya kudharau hizi *observations* ama mapendekezo haya yaliyotolewa. Kwa kweli nafikiri yametolewa kwa nia safi ya kwenda kuyafanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, naahidi mbele ya Baraza lako najua Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ametupa kama miezi mitatu tu kwa ajili ya kuifanyia kazi ripoti hii. Kwa hivyo, ninachosema tutajitahidi na yale aliyosema Mhe. Ali Salum Haji kwamba tufumue kwa lengo safi tu au nia njema ya kujenga.
Kwa maana hiyo, naomba kusisitiza Mhe. Mwenyekiti kwamba haya mapendekezo mliotupa humu tunayapokea na tunayathamini sana na tunawashukuru, pia ninakuahidini kuwa tutakwenda kuyafanyia kazi na *Inshaallah* mabadiliko tutayaona na wala hayatachukua muda. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumalizia kwa kusema kwamba sisi katika Baraza la Manispaa na wizara kwa jumla, hii ni wizara ya watu unapozungumza Tawala za Mikoa una–*deal* na watu na mambo unayaona yapo nje nje, yako wazi hayana siri, uchafu mfano au usafi, mambo ya michirizi, mambo ya uendeshaji sokoni. Waheshimiwa mnapoyaona mimi nasema wakati mwengine tusingoje mpaka labda Kamati Teule ama tungoje Barazani, tuambieni.

Mimi nakushukuruni baadhi ya Waheshimiwa wanafanya hivyo, wananipigia simu bwana wewe kuna tatizo hili na hili na tunalirekebisha mara moja. Sasa naomba sana tushirikiane, kwa sababu haya mambo ukichukulia kwamba sote tupite tuzunguke ni wajibu wetu lakini inakuwa ni vigumu kabisa. Inakuwa vigumu hasa kwa nyenzo zilivyokuwa ni tatizo. Ninachotaka kuahidi Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe kwamba kama nilivyosema tutajipanga upya kama ilivyoshauriwa na hasa suala la uzimamizi bado tumeliona tatizo na kuendesha mambo kisheria. Haya yamejitokeza katika sehemu zote. Hayo tutaona vipi tunayatekeleza.

Nimalizie Mhe. Mwenyekiti, kwamba baadhi ya Wajumbe walizungumza kwamba labda kuna mivutano au kuoneshana misuli kati ya Waziri labda na Mkurugenzi au maafisa wengine. Hatufikii huko wala hatujafika huko, sisi tunajitahidi sana kutumia vikao ili tuone tunakwenda vipi. Mtu tena akiwa anaona taratibu zilizowekwa au sheria zilizowekwa haziwafiki na anafanya atakavyo, sasa huyo niseme labda ni mwenyewe tu anavyohisi. Lakini hatusuguani wala hatupigani, hilo naomba niwafikishie waheshimiwa wajumbe tunajitahidi sana kuzungumza mambo yetu, kufanya vikao, ili tuone tunakwenda wapi, tunaelekea wapi kuweza kutanzua hayo matatizo yaliyopo kwa mustakbali wa kuona kwamba Baraza linakwenda ipasavyo.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba ripoti nzuri, tumeipokea na sipendi kuchambua namuachia mwenyewe Mhe. Mwenyekiti. Niseme tu kwamba tutaifanyia kazi hilo nakuahidi Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe wote, tutajipanga upya tuone kwamba Baraza letu la Manispaa tunarekebisha mapungufu yote ambayo yamebainika.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Kuchunguza Utendaji wa Baraza la Manispaa): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ndogo ya kufanya majumuisho baada ya Waheshimiwa wajumbe kupata nafasi ya kuchangia ripoti yetu hii ya Kamati Teule ambayo imepewa kazi na Baraza hili kuchunguza utendaji wa Baraza la Manispaa la Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi hii kuwashukuru wote Waheshimiwa Wajumbe waliopata nafasi ya kuchangia ripoti hii. Ripoti yetu imechangiwa na Waheshimiwa Wajumbe tisa (9) Wajumbe wanane wamechangia kwa kusema na Mjumbe mmoja (1) amechangia kwa maandishi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niwataje Wajumbe hao.

(1) Mhe. Makame Mshimba Mbarouk

(2) Mhe. Omar Ali Shehe

(3) Mhe. Hamza Hassan Juma

(4) Mhe. Hija Hassan Hija

(5) Mhe. Ali Salum Haji

(6) Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali

(7) Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais

(8) Mhe. Waziri Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

(9) Mhe. Ashura Sharif Ali – amechangia kwa maandishi

Mhe. Mwenyekiti, karibu wajumbe wote wameipongeza ripoti yetu namna tulivyoiandika na jinsi ilivyopangika na mimi kwa niaba ya Wajumbe wenzangu wa Kamati nizipokee pongezi hizo kwa niaba yao. Naamini kwamba Waheshimiwa waliopata nafasi ya kuchangia wamechangia kwa kadiri ya upeo wao na muono wao.

Mhe. Mwenyekiti, naamii kama kungekuwa na nafasi ya basi Wajumbe wengi wangeweza kupata nafasi yakuchangia ripoti hii. Zaidi kwamba wewe mwenyewe ni shahidi bado kulikuwa kuna maneno ya hapa na pale kuona kwamba bado wajumbe hawajaridhika namna ya kikao hiki kilivyokwenda na namna halisi juu ya uchangiaji wa ripoti hii. Tunashukuru kwamba michango imetolewa na tunashukuru Wajumbe karibu wote wameunga mkono hoja hii wakiwemo pia Waheshimiwa Mawaziri.

Mhe. Mwenyekiti, nitataja baadhi ya maelezo yaliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe. Mhe. Omar Ali Shehe alitoa pendekezo wakati wa mchango wake kwamba kuongezwe pendekezo la kumi na nne (14) la kuitaka serikali kumalizia sera ile ya Serikali ya Serikali za Mitaa kabla ya kumalizika mwaka huu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubaliana na hilo na nakubali kuongeza pendekezo la kumi na nne (14) kati ya yale mapandekezo kumi na tatu (13) liongezwe. Pamoja na kwamba Mhe. Waziri ameweza kutoa ufafanuzi juu ya jambo hilo. Nadhani hii itabakia kama ni kumbukumbu pamoja na maelezo ambayo ameyatoa, sasa tunasubiri utekelezaji.

Mheshimiwa mwengine ambaye anahitaji kupata maelezo kidogo ni Mhe. Ali Salum Haji, yeye alipokua akichangia alizungumzia suala juu ya wizi wa nyaraka za manispaa na kusema kwamba kamati imepigwa changa la macho. Ninalotaka kusema kwamba kamati haijapigwa changa la macho na hii inatokana na kwamba kamati ilikuwa inahitaji baadhi ya nyaraka ili kupata ushahidi juu ya maelezo yaliyokuwa akitolewa na Mkurugenzi. Kwa bahati Mkurugenzi baada ya kumpa muda kuleta nyaraka hizo yeye ndiye aliyesema kwamba nyaraka hizo hazipo na pengine nyaraka hizo zimeibiwa na ametueleza haya kwa maandishi na barua rasmi hasa kwamba pana wizi wa nyaraka katika Manispaa na kusema kwamba baadhi ya wafanyakazi wanapofanya makosa katika Wizara zao wanaletwa pale Manispaa kwa hivyo pamekuwa na wizi wa nyaraka.

Sisi kimtazamo hatukukubaliana na lile. Zile zilikuwa ni mbinu za kukwepa ile kauli aliyoitoa kwamba kuna kumbukumbu fulani. Sasa tulipomwambia tuletee ushahidi juu ya jambo hilo, alishindwa kuwasilisha nyaraka zile kwa kisingizio kwamba kuna wizi wa nyaraka. Kamati haikupigwa changa la macho, tulijua tu kauli aliyoitoa Mkurugenzi ilikuwa haina mshiko au haina ukweli ndani yake, ndio maana akatafuta kisingizio kwamba nyaraka zimeibiwa. Kwa hivyo kamati haikupigwa changa la mamcho na tumejua dhahiri kwamba zile ni mbinu za kukwepa lile neno ambalo alilisema na kutotaka kutuletea ushahidi juu yake.

Jengine ambalo ninalotaka kusema juu ya hoja ya Mhe. Mwanasheria Mkuu. katika maelezo yake alizungumzia juu ya utekelezaji wa mapendekezo katika kifungu cha 13 ambacho tabaan amesema hakiwezi kutekelezwa ndani ya miezi mitatu, kama mapendekezo ya ripoti hii yalivyo.

Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kusema kwamba mapendekezo yale yako kwa jumla, yapo yanayoweza kutekelezeka kwa muda mfupi na yapo yanayoweza kutekelezeka kwa muda mrefu. Tunapozungumzia serikali kutoa taarifa ya utekelezaji ya mapendekezo yale ni kueleza ndani ya miezi mitatu namna ya hatua ambazo zitachukuliwa katika utekelezaji wa mambo yale, ili Baraza lijue. Hii inasababisha kuona ni namna gani serikali itakavyoweza kuchukua ripoti hii na kueleza namna ya utekelezaji wake. Pale ndani ya miezi mitatu kama serikali itatoa taarifa juu ya utekelezaji wake. Tabaan pale tutajua ni kweli serikali inadhamiri ya kutekeleza yale yaliyopo badala ya kuona kuna ukimya, tunakwenda na nakuna majibu. Ndio maana ripoti hii nasema ndani ya miezi mitatu basi serikali itoe taarifa namna ya utekelezaji wa yale maazimio ambayo yamepitishwa na Baraza hili.

Jengine ambalo linahitaji kidogo maelezo ni hili la Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais kuhusu kuchangia hoja Waheshimiwa Mawaziri ambapo Mhe. Omar Ali Shehe aliwaomba Waheshimiwa Mawaziri na wao wachangie hoja hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninachotaka kusema kwamba bado waheshimiwa Mawaziri wanayo nafasi ya kuchangia hoja hii. Kwa sababu mawaziri wetu katika mfumo huu tuliokuwa nao wanamaeneo mawili. Kwanza ni wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wengine wameteuliwa lakini wengine wanayo majimbo yao. Lakini pili wao ni serikali. Kwa hivyo kwa kutumia nafasi yao kama ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanayo haja au iko haja na Waheshimiwa Mawaziri kuchangia hoja hii ili kuisaidia kama kuna baadhi ya maeneo ambayo wanaweza kusaidia basi wakaweza kusaidia. Badala ya kukaa kwenda kusubiri kwenye *Cabinet* kwa kwenda kuchangia upande mmoja. Nadhani hilo litakuwa halisaidii.

Lengo la hoja hii ni kuona kwamba michango ya Waheshimiwa Mawaziri nayo inaonekana katika chombo hiki au katika sehemu hii ili iweze kusaidia kuiweka vizuri ripoti hii kwa ajili ya manufaa ya wananchi.

Mwisho ambalo Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame amelizungumzia juu ya suala la Serikali kujipanga kubadilika. Mhe. Waziri amesema kwamba kweli serikali ina dhamira ya kuona kwamba inabadilika na sisi tungeomba iwe hivyo. Lakini suala la kubadilika lisibakie kwenye kauli za maneno, ni lazima zifuatane na matendo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sioni kama kweli serikali inataka kubadilika. Kwa sababu kama serikali inataka kubadilika ndani ya miaka miwili hii tungeweza kuona kwa vitendo. Lakini bado tunapenda kuitumia lugha ya kubadilika lakini hatujawa tayari kubadilika na mifano iko hai.

Mimi nitumie nafasi hii kuiambia serikali lazima tubadilike. Zile kauli ambazo Mhe. Rais anazitoa ziwe kauli za dhati. Mara nyingi Mhe. Rais anasema kwamba tuache tabia ya k ufanya kazi kwa mazoea na mwenyewe anaita *business as usually*. Hii nayo ina maana na ina msingi, tukiacha kufanya kazi kwa mazoea huko tulikotoka basi mafanikio yatapatikana.

Niiombe sana serikali kauli hizi tunazozitoa za kubadilika basi tubadilike kweli. Lakini vyenginevyo ikiwa tunatoa kauli za maneno bila ya kuona vitendo badi tutabakia kila siku kuimba nyimbo hii tunataka kubadilika lakini mabadiliko wananchi hawayaoni. Tubadilike, tuanze kubadilika kutokana na mabadiliko yaliyopo. Ripoti zetu hizi ile ya kwanza na hii ripoti ya pili kama zingefanyiwa kazi vizuri na serikali basi wananchi wangeona mabadiliko. Lakini kwa kweli inasikitisha kuona kwamba ripoti yote iliyowasilishwa ile ya mwanzo, hakuna mtu aliyeingizwa hatiani. (*Makofi*)

Pamoja na kwamba Mwanasheria anasema hatua zimechukuliwa lakini mimi nasema si kweli. Kama ripoti imeeleza maelezo yote lakini kila kitu kinaambiwa hakuna kosa, huku hakuna kosa, huku hakuna kosa, kwa kweli dhamira ya mabadiliko ya kweli yanakuwa hayaonekani. (*Makofi*)

Mimi nimuombe sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais nimuombe sana, sana, sana, amshauri sana Mhe. Rais, juu ya mapendekezo ya Baraza hili na hatua zinazohitaji kuchukuliwa juu ya taarifa mbali mbali zinazotolewa na Baraza hili. Mimi siwezi kusema kubishana kwamba nani mwenye mamlaka katika mambo haya. Serikali ina mamlaka kwa upande wake na Baraza la Wawakilishi lina mamlaka yake kwa upande wake. Na sisi sote tunajenga nyumba moja, ikiswa sasa kila mtu anavuta upande wake, sasa nyumba hii itakuwa haisimami. Lazima tuwe na imani ya dhati, kutokana na sisi sote tunawatumikia wananchi. Wananchi wanahitaji maendeleo ya dhati kama tulivyowaahidi na wao wanatuangalia. Wakati wa kubabaisha umekwisha, tutakapo babaisha wananchi wanatuangalia. Iko siku watatuuliza. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo nichukue nafasi hiii niwashukuru sana Wajumbe wote waliopata nafasi ya kuchangia, niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri kwa ufafanuzi wa mambo mbali mbali. Niwashukuru wote waliochangia kwa namna moja au nyengine na niiyombe sana Serikali basi ichukue hatua juu ya utekelezaji wa mapendekezo yote yaliyotolewa katika ripoti hii ya Kamati Teule. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Ahsante (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa kuwasilisha na kufanya majumuisho ya maoni pamoja na maombi yote ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wajumbe.

Sasa niwahoji waheshimiwa wajumbe wale ambao wamepokea uwasilishaji wa ripoti hii pamoja na mapendekezo yake wanyooshe mikono. Waliokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja imetolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kukubaliwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia nikushukuruni na nyinyi Wajumbe wenzangu kwa kuniwezesha kuweza kuendelea na shughuli hii nzito hadi tukaweza kumaliza ripoti hii na kuweza kupokelewa katika taratibu zetu za kisheria kama ambavyo tulipaswa kufanya hivyo.

Kabla sijaakhirisha Baraza hili ningependa nitoe taarifa kwamba Wajumbe wote kesho mnatakiwa mje mapema, tuendelee na shughuli zetu kama kawaida ili baadaye tuweze kumsikiliza Mhe. Makamo wa Pili wa Rais katika hotuba yake ya kufunga Baraza hili katika nyakati za asubuhi.

Baada ya maelekezo hayo kwa heshima na taadhima naomba kuchukua fursa hii kuliakhirisha Baraza hili hadi kesho tarehe 24/10/2012, saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 12:46 jioni Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 24/10/2012 Saa 3:00 asubuhi)